# Nipashe

Jumatano Oktoba 23, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580056

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Fisi wavamia msibani na kujeruhi watu, wawili hoi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wadau wachambua rushwa, vurugu uchaguzi S/Mitaa

**NI** yaliyojitokeza kura za maoni CCM, wahofu uchaguzi unaofuata...*Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakishirikiana kupakia vyombo vya ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kwenye gari la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), jijini Mbeya jana, ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila kuhamisha ofisi hiyo ndani ya saa 24 na kuhamia eneo la Inyala. **PICHA: NEBART MSOKWA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## Makonda atengua agizo la DC Ilala

UKURASA 2

## HUDUMA DHARURA KIKWAZO HOSPITALI

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YACHANA MBAO KIRUMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Wadau wachambua rushwa uchaguzi mitaa

**Na Mary Geofrey**

BAADHI ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa wamepongeza uamuzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuchukua hatua dhidi ya rafu, rushwa na figisu figisu zilizojitokeza kwenye kura za maoni za uchaguzi wa serikali za mitaa ndani ya chama hicho.

Kura za maoni zilifanyika mwishoni mwa wiki kuteua wagombea watakaopeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi huo wa Oktoba 24, mwaka huu.

Mratibu wa Mtandao wa Utetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema lipo tatizo la watu kuamini kuwa kwenye siasa au wakati wa uchaguzi ndiyo wakati wa kuvuna fedha.

"Ni jambo jema kama CCM imeona hili na kuchukua hatua, ni hatua nzuri kuwa wameona mambo hayako sawa wanachukua hatua," alisema na kuongeza:

"Tatizo la watu wengi ni kufanya siasa kuwa sehemu ya kupata hela kutumia fedha au kutoa rushwa bado halijaondoka."

Alisema kumekuwa na historia ya muda mrefu kuwa wakati wa uchaguzi ndiyo wakati wa kuvuna na kwa chama kama hicho kutoa karipio kutawaweka watu sawa na kurudi kwenye mstari.

"Tunampongeza sana Dk. Bashiru kwa kukemea na kuchukua hatua, ameonyesha kuwa kipindi cha uchaguzi siyo kipindi cha kuvuna fedha au kutoa rushwa bali kuchagua viongozi sahihi," alisema Olengurumwa.

Mchambuzi wa masuala ya Siasa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Alex Benson, alisema zinaashiria kuwa bado jamii haina uelewa kuhusu maana ya dhamana.

Alisema vitendo hivyo vinaashiria kuwa bado watu wana tamaa ya madaraka kwa manufaa binafsi na siyo wanataka kuwania kwa lengo la kuhudumia jamii.

Benson aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, kuhusu malalamiko ya kuvunjwa kwa kanuni na mtizamo wa rushwa, upendeleo na kupanga safu kwa ajili ya uchaguzi ujao wa mwaka 2020 na maamuzi yaliyochukuliwa na CCM, yaliyoibuka kwenye kura za maoni ndani ya chama hicho.

INAENDELEA UK 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipewa mkate na chumvi ukiwa ni utamaduni wa kukaribisha wageni wa Warusi, alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Sicho nchini humo juzi, ambako anamwakilisha Rais John Magufuli katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Urusi. **PICHA: OWM**


## KUMBUKUMBU

**TAREHE 23/10/2018**

UMETIMIZA MWAKA MMOJA SASA TANGU UITWE NYUMBANI KWA BWANA INGAWA BABA YETU HAUPO NASI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA KATIKA SALA NA MAOMBI ULIKUWA NGUZO IMARA KATIKA MAISHA YETU, ***HEKIMA NA BUSARA ZAKO TUNAZIKUMBUKA DAIMA***. TUNASHUKURU MWENYEZI MUNGU KWA MAISHA YAKO KWETU HAKIKA PENGO ULILOLIACHA HALITAZIBIKA KAMWE.



MZEE DIONIS SEMINDU MSELE
1942 - 2018

UTAKUMBUKWA DAIMA NA
***MKEO, WATOTO, WAJUKUU,NDUGU, MAJIRANI NA MARAFIKI ZAKO.***

**RAHA YA MILELE UMPE EWE BWANA NA MWANGA WA MILELE AKUANGAZIE, UPUMZIKE KWA AMANI.**


## Makonda atengua agizo la DC Ilala

**Na Beatrice Moses**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza kutengua amri ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, aliyepiga marufuku ibada za katikati ya wiki, akitaka zifanyike siku maalum pekee.

Makonda amesema serikali haina dini na watu wana uhuru wa kuabudu wakati wowote bila kuvunja sheria.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa na mmoja wa waandishi wa habari waliohudhuria kwenye mkutano uliofanyika ofisini jana ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

"Upande wa imani serikali haina dini. Natengua kauli ya DC (Mkuu wa Wilaya) wa Ilala watu waendelee kwa imani zao bila kuathiri sheria za nchi. Viongozi tunapaswa kuwa makini tunapoingia kwenye mambo ya dini. Haya ni mambo ya imani, mimi mwenyewe hapa ni mlokole huwezi kunipangia muda wa kusali," alisema Makonda.

Alitolea mfano kutoka kwenye vitabu vitakatifu kuhusu habari za Daniel ambaye watu walimchongea na wakatengenezewa sheria za kumdhibiti kumwabudu Mungu, lakini aliendelea kumwabudu hadi mfalme akamfahamu Mungu aliye hai.

"Wapo watu wanakula kupitia madhabahu, asubuhi wanaamka wanaombea wengine wagonjwa, wengine wanatusaidia kukemea mapepo. Wengine wanatusaidia kuhakikisha ulinzi na usalama unaendelea kuwapo kwa hiyo hatuwezi kubeza. Ibada haina siku inahitaji moyo na utayari wa mwanadamu," alisema Makonda.

Alisema inawezekana kuna

INAENDELEA UK 8

## KESI YA ZITTO

### Shahidi adai majeruhi walichukuliwa kuhojiwa

**Na Hellen Mwango**

MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Morogoro (RCO), Mrakibu wa Polisi, Albart Kitundu (49), amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, kwamba hakuna majeruhi aliyechukuliwa na Jeshi la Polisi kwenda kuuawa bali walichukuliwa hospitali na kwenda kuhojiwa kuhusiana na tukio.

Kadhalika alidai kuwa aliwasiliana na RCO wa Kigoma kuhusu tukio hilo na alimweleza ukweli kuwa amewahoji watu mbalimbali na kuwa watu waliokufa kwenye tukio hilo ni wanne na si zaidi ya 100.

Ushahidi huo aliutoa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, akisaidiana na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Nassoro Katuga na Colonel Tesha.

Akiongozwa na Katuga, shahidi huyo alidai kuwa Oktoba 28, 2018 alikaimu nafasi ya RCO Mkoa wa Kipolisi Kinondoni baada ya bosi wake kuwa na udhuru.

Pia alidai kupata taarifa kwamba viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo watafanya mkutano na waandishi wa habari Makao Makuu ya Chama chao Kijitonyama, jijini Dar es Salaam.

"Nilijiridhisha kama wana kibali cha kufanya mkutano huo, nilibaini kwamba wanacho kibali," alidai shahidi.

Alidai kuwa aliteua makachero wawili kwenda kuhudhuria mkutano huo ili kuweka kumbukumbu zinazohitajika kama kielelezo katika jinai.

Alidai waliporejea makachero aliowaagiza aliona picha za video walizorekodi kwenye mkutano huo wakati mshtakiwa akitoa kauli za uchochezi kwamba watu zaidi ya 100 wameuawa na Jeshi la Polisi kitongoji cha Mpeta, Wilaya Uvinza na waliokwenda kutibiwa katika zahanati ya Nguruka mkoani Kigoma.

Vile vile, alidai Oktoba 29, 2018 bosi wake RCO Malulu alipofika ofisini alimwita na kumfahamisha kwamba amekuta kundi la watu likijadili hotuba ya Kabwe na kwamba wamechukizwa sana na serikali ikiwamo Jeshi la Polisi.

"Bosi wangu alinipa kazi

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA

# Huduma magonjwa ya dharura bado kikwazo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Kitengo cha Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Aga Khan, Dk. Sherin Kassamali, amesema bado kuna changamoto ya wataalamu wa kuhudumia wagonjwa wa dharura ikiwamo moyo kuacha kudunda ghafla.

Kassamali ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya dharura, alisema jana kuwa kutokana na changamoto hiyo, hospitali hiyo kiithibati imekuwa kituo cha mafunzo maalum ya magonjwa ya dharura kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Moyo ya Marekani (AHA).

Dk. Kassamali alisema ili kukabiliana na changamoto hiyo, hospitali hiyo imeamua kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalamu wa afya hospitali za serikali, binafsi na wadau wengine ili kukabiliana na matatizo hayo Tanzania.

Alisema matatizo moyo kuacha kudunda ghafla huweza kumtokea mtu muda na wakati wowote.

"Kwa mujibu wa AHA, takriban asilimia 90 ya watu wanaopata matatizo ya moyo kuacha kudunda ghafla, hufa wakiwa hawako chini ya uangalizi wa wataalamu hospitalini.

"Kituo hiki cha mafunzo kinawafundisha nini cha kufanya wakati moyo ukiacha kudunda ghafla, unapoacha kudunda maana yake hakuna mzunguko wa damu katika mwili na usipokuwapo inamaanisha seli katika mwili zinakufa. Seli zikifa maana yake mtu anafariki dunia," alisema.

Dk. Kassamali alisema seli zinaonyesha kwamba endapo mtu amepata tatizo hilo na akapewa mapema huduma ya dharura kitaalamu, inaweza kumwezesha kuendelea kuishi.

"Wako walioletwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na hapa Aga Khan wakiwa katika hali ya moyo kuacha kudunda wakapewa huduma ya dharura inavyotakiwa wakaondoka nyumbani na nafuu," alisema.

Mkuu wa Idara ya Biashara na Ubora wa Chama cha Watoa Huduma Binafsi za Afya Tanzania (APHFA), Denis Mosha, alisema uelewa wa magonjwa ya dharura au kuchukua hatua wakati wa matatizo hayo, umekuwa changamoto kwa hospitali nyingi na hata kama upo ni kwa kiwango kidogo.

"Si kwamba wataalamu wa magonjwa ya dharura hawana uelewa kabisa bali tunataka waendane na teknolojia ambayo imeletwa na taasisi hii ya AHA.

"Kunatofauti ya kusoma darasani na kufanya mafunzo kwa vitendo, tunahitaji kumwokoa mgonjwa kwa hiyo elimu hii itawasaidia zaidi waweze kuokoa wagonjwa wengi zaidi," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chogolo, akifungua mafunzo ya elimu kwa umma juu ya matumizi ya barabara wakati wa ujenzi, kwa waendesha bodaboda, bajaji na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zilizopo kando ya barabara ya Shekilango, eneo la Sinza, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Fisi wavamia na kujeruhi msibani

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

WATU wawili wamenusurika kifo baada ya kushambuliwa na fisi wasiojulikana idadi yao kuvamia kwenye nyumba iliyokuwa na msiba katika kijiji cha Kasahunga Bunda, mkoani Mara.

Daktari wa Hospitali ya Misheni Kibara, Samuel Paul, alithibitisha kupokea majeruhi David Robert ambaye amelazwa kutokana na kujeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo mikono yake.

Naye muuguzi mmoja wa kituo cha afya Kasahunga, aliyefahamika kwa jina la Happy, aalisema majeruhi mwingine Elizabeth mgeta (60) amelazwa kutokana na kujeruhiwa mkono mmoja.

Mashuda wa tukio hilo, walisema fisi hao walivamia majira ya saa 6:00 usiku wa kuamkia jana.

Walisema fisi hao walivamia msibani hapo na kuanza kushambulia waombolezaji hao waliokuwa wamekaa nje wakisubiri kulala, baada ya ibada kuisha.

"Tulipomaliza ibada tulitaka kulala, fisi walivamia katika eneo hilo na kujeruhi wenzetu," alisema shuhuda mmoja.

Katika hatua nyingine, wavuvi wanne wamepoteza maisha baada ya kufa maji kutokana na mtumbi waliokuwa wanavulia samaki kutoboka na kuzama katika Ziwa Victoria, eneo la mwalo wa Kibara, wilayani Bunda mkoani Mara.

Kwa mujibu wa polisi, mvuvi mmoja Doto Mufungo (18) mkazi wa kijiji cha Kenkombyo, alinusurika kifo baada ya kushikilia mtumbwi huo na kupiga kelele za kuomba msaada na hatimaye wananchi kufika na kumwokoa.

Wavuvi waliokufa maji wametambuliwa kuwa ni Kabenjulilo Magere (17), Godluck Yohana (15), Kaitila Julius (19) na Philipo James (17) ambaye alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kenkombyo, aliyefaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Juma Ndaki, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo usiku wa kuamkia jana majira ya saa 7:30 usiku.

Hadi jana, mchana miili ya wavuvi wote wanne ilikuwa imepatikana na kukabidhiwa kwa ndugu zao kwa ajili ya mazishi.

Daktari wa Hospitali ya Misheni Kibara, Dk. Samuel Paul, na muuguzi Nurie Mabele, walithibitisha wavuvi hao kufa maji.

# Agizo la Chalamila latekelezwa magari ya jeshi yahamisha h'shauri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

AGIZO la Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila aliloelekeza juzi kuwa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zihamishwe ndani ya saa 24 kutoka katikati ya Jiji la Mbeya kwenda mahali popote ndani ya mipaka ya halmashauri hiyo, limetekelezwa chini ya ulinzi wa vyombo vya dola.

Katika kuhakikisha kuwa ofisi hizo zinahamishwa, jana asubuhi Chalamila alitinga katika ofisi hizo akiwa na magari matano ya vyombo hivyo kwa ajili ya kufanya kazi ya kuhamisha nyaraka na mali nyingine za halmashauri hiyo.

Magari yaliyotumika ni makarandinga matatu, la Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), huku magari mengine mawili yakiwa ni aina ya Land Cruiser mali ya Jeshi la Polisi lililokuwa limebeba askari wa kikosi cha kutuliza ghasia (FFU), wakisimamia ulinzi.

Akizungumza baada ya kuwasili kwenye ofisi za halmashauri hiyo akiwa na magari hayo, Chalamila alisema hawezi kuchukua magari ya watu binafsi kutokana na kutofahamu miiko na maadili ya kusafirisha nyaraka muhimu za serikali.

"Tumechukua magari haya ya majeshi yetu ili yabebe na kusafirisha nyaraka na mali za serikali salama kwenda huko wanakohamia, tumefanya hivi kuhakikisha mali za serikali zinakuwa salama katika zoezi hilo la uhamisho," alisema Chalamila.

Alisema hata baada ya kuwasili kwenye ofisi mpya zinakohamia, vy

INAENDELEA UK 8


**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili **MC 990 BYN.** Chassis No.**MD2A21BY1JWAS91895,**.Engine **No.PFZWJM67506.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/354808/2019.**

115472202

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu : +255 26 2324455
Fax: 255 26 2323233
Barua pepe : ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470 Dodoma
**22/10/2019.**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 23/10/2019 Kampuni ya Mussa holdings itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Kingori kuelekea Moshi. Gari lenye namba za usajili T277ALQ.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0

3. Njia itakayotumika ni Kingori kupitia Bomangombe –Moshi gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:00jion)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115473802

**TANGAZO KWA UMMA**

**MATUMIZI MABAYA YA JINA LA**

**BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA KWA UDANGANYIFU**

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

**Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:**

- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya **barua-pepe: security@afdb.org.**

215468802

# Meneja adaiwa kutakatisha milioni 413/-

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo mpaka upelelezi utakapokamilika na itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu na Rushwa.

**Na Hellen Mwango**

MENEJA wa Kampuni ya Neelkani Salt Limited, Mohammed Alikhan (29), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo wizi wa katoni za chumvi 45,919 zenye thamani ya Sh. milioni 413.5.

Alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, aliyepangiwa kusikiliza kesi yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kati ya Januari Mosi, 2018 na Julai 29, mwaka huu mshtakiwa anadaiwa kutenda makosa hayo.

Wankyo alidai kuwa kati ya Januari Mosi, 2018 na Julai 29, mwaka huu katika mtaa wa Arusha Ilala, jijini Dar es Salaam, Alikhan akiwa Meneja wa tawi la kampuni hiyo aliiba katoni za chumvi 45,871 aina ya Neel, mali ya mwajiri wake yenye thamani ya Sh. 412,839,000.

Katika shtaka jingine, mshtakiwa huyo anadaiwa kuwa katika kipindi hicho aliiba kilo moja ya aina ya Neel Gold yenye thamani ya Sh. 720,000.

Jamhuri ilidai katika tarehe na miaka ya tukio la kwanza, mshtakiwa Alikhan alitakatisha Sh. 413,559,000, wakati akijiua fedha hizo zimetokana na zao la makosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na wizi akiwa mwajiriwa.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo mpaka upelelezi utakapokamilika na itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu na Rushwa.

Hakimu alisema kwa kuwa mashtaka ya kutakatisha fedha hayana dhamana, mshtakiwa atarudishwa mahabusu.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na mshtakiwa alipelekwa rumande. Kesi imeahirishwa hadi Novemba 5, mwaka huu.



Shule ya Al Madrasa Saifiya tul Burhaniyah (maarufu MSB), ya jijini Dar es Salaam imetoa msaada wa chakula katika vituo kadhaa vya watoto yatima katika kusherehekea Siku ya Chakula Duniani wilaya za Kinondoni na Temeke. Watoto wa shule hiyo walisambaza ujumbe wa kuacha kutupa chakula ovyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka mazingira wezeshi uchaguzi mitaa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wasioona Tanzania, kimeiomba serikali kuweka mazingira wezeshi kwa kundi hilo ili nalo lishiriki ipasavyo kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, baadhi ya viongozi wa chama hicho walisema mpaka sasa mfumo wao wa kupiga kura kuwachagua viongozi katika ngazi mbalimbali bado si wa siri.

Mratibu wa Wanawake na Watoto wa Chama hicho, Rehema Daruweshi, alisema katika uchaguzi mbalimbali wamekuwa wakishiriki lakini bado uamuzi wa kuamua kiongozi wanayemtaka uko mikononi mwa watu wengine.

"Unajua sisi ambao hatuoni bado hatuwezi kusema tunamchagua kiongozi tunayemtaka. Maamuzi yetu bado yako mikononi mwa watu ambao hasa ni ndugu zetu ambao wanakuwa wametusindikiza kwenda kupiga kura," alisema.

"Kwa mfano mimi nakwenda na mwanangu ananisindikiza kwenda kupiga kura. Nikifika katika sanduku la kura na mwelekeza amchague kiongozi ninayempenda, anaweza kunitikia. Lakini tukumbuke kwamba na yeye ana chaguo la mtu anayemtaka na mwisho wa siku yeye ndiye anayeona na ndiye mwenye uamuzi wa mwisho pale katika kuweka wino. Naweza kumwelekeza anichagulie kiongozi A lakini kwa mapenzi yake na kwa kuwa sioni, akachagua kiongozi B."

Kutokana na mazingira hayo, alisema ni vyema serikali ikaandaa mazingira ambayo hayatamlazimu mtu asiyeona kumhusisha mtu wa pili katika kupiga kura mwenyewe pasipo usaidizi.

Naye Mratibu wa Maendeleo ya Vijana na Chipukizi wa chama hicho, Kiongo Itambu, aliiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuanzisha utaratibu maalum wa kuwafikia watu wenye ulemavu kupitia katika vyama vyao kwa ajili ya kuwapatia elimu ya uraia.






# Shein ataja siri ya ardhi kwa maendeleo

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk.Ali Mohamed Shein, amesema matumizi mazuri ya ardhi na usimamizi bora wa mazingira ni misingi muhimu katika maendeleo ya taifa lolote duniani.

Dk. Shein aliyasema hayo jana katika mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Majaji na Mahakimu wa Nchi za Afika Mashariki unaofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni mjini Zanzibar.

Alisema mkutano huo umekuja wakati mwafaka wakati changamoto kadhaa zinazohusiana na ardhi na mazingira zimekuwa zikiibuka katika nchi za Afrika Mashariki.

Kuongezeka kwa idadi ya watu sambamba na kukua kwa uchumi, alisema kumeleta changamoto nyingi katika sekta ya ardhi na mazingira katika nchi hizo na kutolea mfano migogoro ya ardhi ambayo imeikumba miji na vijiji ambayo baadhi hujumuisha wananchi na wawekezaji.

Alisema iwapo hali hiyo itaendelea itakuwa tishio kwa maendeleo ya kiuchumi na usalama kwa nchi za Afrika Mashariki huku akieleza alivyovutiwa na maudhui ya mwaka huu yasemayo "Ardhi na Mazingira kwa Maendeleo Endelevu ya Afrika Mashariki".

Dk. Shein alielezea kuvutiwa na maudhui hayo ambayo yamekuja wakati mwafaka kutokana na nchi nyingi za Afrika Mashariki kuweka mikakati ya makusudi katika kuimarisha mazingira na matumizi mazuri ya ardhi.

Kutokana na mada zitakazojadiliwa katika mkutano huo wa siku nne, alisema ana matumaini makubwa kuwa mkutano huo utatoa mbinu na njia mbadala za kutatua changamoto zilizopo.

Kwa upande wa Zanzibar, Dk. Shein alieleza hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutatua migogoro ya ardhi huku akisisitiza kuwa Zanzibar ardhi yote ni mali ya serikali kama ilivyoelezwa katika sheria namba 12 ya mwaka 1992.

Kuhusu mazingira, alieleza changamoto mbalimbali zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu pamoja na athari za kimaumbile hasa mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Shein alieleza haja kwa jumuiya hiyo ikashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali katika masuala ya kimazingira hasa ikizingatiwa kwamba uchumi wa nchi za Afrika Mashariki unaendelea kukua katika sekta nyengine mpya ikiwemo sekta ya mafuta na gesi ambayo imethibitika kwamba imekuwa ikileta changamoto nyingi za mazingira katika nchi za Afrika pamoja na zile nchi za Mashariki ya Kati. alisisitiza kwamba taaluma ya sheria inahitajika katika kusimamia sekta hizo mpya ili kwenda sambamba na ukuaji wa sekta hizo mpya.

TANGAZO


MWANZO WA UBORA MPYA!
SERENGETI BREWERIES
2019
SERENGETI BREWERIES LIMITED
1988
Jiunge nasi tusherehekee pamoja tukizindua muonekano wetu mpya!
Daima tutaendelea kukupatia bidhaa zenye ubora!
JOHNNIE WALKER
Smirnoff
GUINNESS
BAILEYS
SERENGETI
TUSKER
SERENGETI LITE
Pilsner LAGER
215473102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi mitaa utuletee waadilifu

**KATIKA** harakati za kuchagua viongozi wa serikali za mitaa, tunaona kuwa taifa limejaa watu wengi wanaotamani kuwa viongozi wa kisiasa wanaotaka kubebeshwa jukumu la kuviongoza vijiji, mitaa na vitongoji.

Hilo ni bayana kutokana na ushindani mkubwa unaoonekana miongoni mwa wagombea.

Lakini, ni wazi kuwa si wanasiasa wote wanaofaa kuwa viongozi bora, wengi wanakosa vigezo muhimu kama uadilifu na uwajibikaji.

Kwa viongozi wengi ambao hawana vigezo hivyo, kinachojiri ni kila mmoja kuendeleza uzalendo wa kuchumia tumbo na kujinufaisha wenyewe wala si taifa.

Ndiyo maana wakati mwingine tunaungana na baadhi ya vyama tukiamini kuwa ni vyema kufuatilia mwenendo wa mchakato wa kuchuja majina na kufahamu wagombea walivyopatikana.

Na ikibidi kama kuna ujanja ujanja, uliofanyika wasio na sifa wanafutwa na zoezi kurudiwa upya, kama CCM ilivyofanywa kwa wagombea wote wa mkoa wa Dar es Salaam.

Si vyema kuhukumu lakini, kuna malalamiko mengi yanayotolewa dhidi ya wanasiasa kwa ngazi zote hata za serikali za mitaa.

Watu wengi wanawachukulia wanasiasa ambao ni viongozi muhimu kuwa ni wadanganyifu, wazushi na zaidi wasioaminika na wanaopata uongozi kupitia rushwa au kwa ujanja ujanja lengo lao likiwa kujinufaisha hasa kwa kusaka mali.

Tunapenda kuwaambia wapiga kura kuwa wanasiasa wote wakiwamo viongozi wa serikali za mitaa ni muhimu.

Tena wapo waadilifu na wawajibikaji, hivyo ni jambo jema kupiga kura ili kuwachagua kama ilivyo kwenye kura za maoni za kuwapitisha.

Kwa hiyo ni vyema kwa vyama vya siasa kuwa na mchakato makini wa kuwapata wagombea hao.

Zoezi hilo ni muhimu likafanyika kihalali na kwa taratibu na si kiubabaishaji hadi kusababisha matokeo kufutwa.

Ni vizuri kupata viongozi ambao si wala rushwa au 'wapigaji madili', kuwa na viongozi wa vijiji, vitongoji na mitaa wanaoingia madarakani kupitia njia za kiujanja ujanja, ambao si watumishi wa wananchi bali wanaojinufaisha, haikubaliki.

Tunasema haya kwa sababu wapo watu wanaopata uongozi kwa kutoa rushwa ya ngono kwa kamati za kuchuja majina ili wapitishwe.

Lakini, pia wapo wanaotoa rushwa ya pesa ili majina yao yapitishwe na kuna wanaowahonga wapiga kura ili wawachague, yote haya yanasababisha kupata viongozi wasio waadilifu wala wawajibikaji.

Viongozi wa kisiasa ni muhimu ambao ndiyo muhimili wa dolakwa maana ya serikali. Tunawahitaji kama walivyo wabunge na mahakama.

Hawa ndiyo watu muhimu kwenye ngazi za mitaa, vijiji na vitongoji wanaohusika na bajeti, mipango ya maendeleo na pia ndiyo wahusika wakuu kwenye utawala na uongozi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Tunapenda kuwakumbusha wanaoogombea kuwa uongozi katika ngazi hii ni muhimu kwa kuwa ndiyo unaohusika moja kwa moja na wananchi.

Viongozi hawa wanatakiwa kuwatumia wananchi na kulitendea taifa mambo mema kama kuleta umoja na mshikamano, kudumisha upendo, uelewano, uzalendo na utaifa pamoja na kuhimiza maendeleo ili kuondokana na umaskini.

Tunapenda kuwakumbusha wanaogombea uongozi kuwa viongozi bora ni wale mchanganyiko wa karama (charisma) na uadilifu na pia uwezo wa kuchanganua mambo na kufanya maamuzi yenye manufaa ya wengi na si ya mtu mmoja.

Tunapenda kuwakumbusha kuwa uwajibikaji ni muhimu na hilo ndilo liwe msukumo kwa viongozi wa serikali za mitaa. Wakubali kukosolewa na kurekebishwa na hata ikibidi wajiuzulu madaraka yao kutokana na makosa yaliyofanyika.

Tunawatakia kila la kheri wagombea serikali za mitaa watakaoleta uongozi bora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wapenda rushwa CCM wasome ishara za nyakati

Na Sabato Kasika

**CHAMA** Cha Mapinduzi (CCM) kimeagiza kurudiwa kwa kura za maoni kwa wagombea wa uongozi wa serikali za mitaa ndani ya chama hicho katika maeneo yote yaliyolalamikiwa kwa kukiuka kanuni za uchaguzi.

Miongoni mwa maeneo hayo ni mkoa wa Dar es Salaam, ambao unatajwa kuongoza kwa kukiuka kanuni za uchaguzi, na sasa wanachama wapo kwenye mchakato wa kurudia kura hizo.

Hatua iliyochukuliwa na chama hicho ya kuagiza kurudiwa kwa kura za maoni ni wazi kwamba inalenga kukomesha rushwa na kupata viongozi sahihi watakaosaidiana na wananchi kuleta maendeleo kwenye maeneo yao.

Ingawa wapo baadhi ya wanachama wanaoamua kuziba masikio ili wasisikie lolote kuhusu madhara ya rushwa, lakini ukweli rushwa ni adui wa haki na inapingwa katika ahadi za mwanachama.

Imani ya CCM ni kwamba binadamu wote ni sawa, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake, ujumaa na kujitegemea ndiyo njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru.

Ukienda kwenye ahadi za mwanachama, ile ya nne inasema: "Rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa."

Ahadi ya tisa inawataka wanachama wawe waaminifu, lakini hilo nalo bado ni tatizo kwa baadhi yao.

CCM kupitia kwa Katibu wake Mkuu, Dk. Bashiru Ally, kinasema vitendo hivyo na madai ya upendeleo ni dalili za kupanga safu kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao wa Rais, wabunge na madiwani.

Kwamba malalamiko yaliyopokelewa makao makuu yanagusa uvunjifu wa kanuni kwa mtazamo wa rushwa au upendeleo au kupanga safu, lakini tayari mchezo huo umeshazuiwa.

"Napenda kusisitiza haki itendeke, malalamiko tunayoyapokea yanavunja uvunjifu wa kanuni, kwani kanuni za kuchuja wagombea hazikuzingatiwa kwenye baadhi ya maeneo," anasema Dk. Bashiru.

Kimsingi hatua iliyochukuliwa na chama makao makuu ni dalili tosha kwamba kimedhamiria kupambana na vitendo vya rushwa, ambavyo vimekuwa vikikwamisha baadhi ya wanachama kupata haki.

Kwa mfano baadhi ya wanachama wa CCM wa kijiji cha Suguti, Musoma Vijijini, mkoani Mara, walidai kuuziwa fomu za kuomba uongozi kwa Sh. 20,000 na kusababisha baadhi yao kukwama kuzichukua.

> **"Napenda kusisitiza haki itendeke, malalamiko tunayoyapokea yanavunja uvunjifu wa kanuni, kwani kanuni za kuchuja wagombea hazikuzingatiwa kwenye baadhi ya maeneo," anasema Dk. Bashiru.**

Yanapokuwapo mazingira ya aina hiyo, ni wazi kwamba wasio nacho watashindwe kuwania uongozi ili wenye nia ya kupanga safu ya uongozi wapate upenyo, lakini bahati nzuri hilo limeshtukiwa na kuzimwa.

Hii yote inaonyesha aidha, wanafanya makusudi au hawajui kwamba CCM mpya ilishapiga marufuku michezo yote michafu kwa lengo la kuhakikisha kila mwanachama anashiriki katika uchaguzi iwe kuchagua au kuchaguliwa.

Hivyo ni vyema wapenda rushwa ndani ya CCM wakasoma ishara za nyakati na kutambua kwamba CCM mpya imejishajipambanua kwamba haitaki makandokando yakiwamo hayo ya rushwa.

Katibu Mkuu anasema kulikuwa na rafu za kuchomoa majina kwenye masanduku ya kura na masanduku kubomolewa na wengine wakitumia jina lake kuwa amewapa maelekeo ya kufanya walivyofanya.

Bashiru anasema tatizo lingine ni wasimamizi kuchelewa na kura za maoni kuanza kupigwa baada ya saa tisa alasiri, na sasa wagombea wote walioomba wanatakiwa kurudishwa ili wapigiwe kura.

Kura hizo ilikuwa zimalizike Oktoba 29 na sasa kimeongeza siku mbili hadi Oktoba 31, mwaka huu.

Niwakumbushe wanaCCM kuwa uhalali wa chama kuendelea kuongoza nchi unaweza kupimwa kwenye vipimo mbalimbali kuanzia utekelezaji wa ahadi na pia kumaliza makandokando yakiwamo hayo ya rushwa.

Ikumbukwe kuwa kuwapo kwa rushwa ndani ya chama ni kusababisha migogoro ambayo inaweza kukipasua, lakini nzuri viongozi wa juu wanapopelekewa malalamiko wanayafanyia kazi haraka ili yasilete madhara.

Lakini pamoja na hayo, bado kuna haja wanachama kuzingatia ahadi 10 za mwanachama ambazo ni msingi wa mwanachama kufanya shughuli za chama kwa uaminifu, vinginevyo malalamiko yataendelea kuwapo.

## TANGAZO


you've got
game
more 4 less
MORE EXCITING DEALS.
MORE VALUE.
More than you bargained for.
now available at game
2 for Tsh1880
Daigani Water 1500ml
2 for Tsh 37000
Noor Sun Flower Oil 3l
3 for Tsh 7800
Spidadoro Spaghetti Pasta
2 for Tsh10000
Twinsavers White Roller Towels 4's
2 for Tsh11000
Sensodyne Toothpaste 75ml
2 for Tsh9400
Pledge Furniture Polish 275ml
5 for Tsh50000
Royal Cashew Nuts Roasted 250g
All for Tsh85000
Canon MG2540 Inkjet Printer +
2 Free Packs Photo Paper
Both for Tsh55000
Logik Dry Iron and 1.7l Kettle
2 for Tsh40000
Trojan 3mm Yoga Mat
2 for Tsh30000
Sondico Balls Size 5
2 for Tsh1600
Shield Sheen Xtreme Nu Car Cherry, Xtreme, Musk or Strawberry 750ml
4 for Tsh2600
Alpenliebe Candy Assorted 36g
2 for Tsh90000
Contour Tuscony Black Chair
215472102
you've got
game
View this catalogue online at www.game.co.tz
01 | 14115 | DEALS VALID 24 October - 31 December 2019
ITEMS AVAILABLE WHILE STOCKS LAST
ALL PRICES LISTED ARE IN TANZANIAN SHILLINGS . ALL PRICES INCLUDE VAT.
TANZANIA, DAR ES SALAAM
SHOPPING HOURS
Walmart
Save money. Live better.

# Wadau wachambua rushwa uchaguzi mitaa

INATOKA UK 2

"Kinachotokea katika siasa za Tanzania ni ukosefu wa maadili ya uongozi, bado watu au wanachama wa vyama hawafahamu nini maana ya uongozi, ndio sababu ya kutumia fursa hizo kuwania kwa lengo la kujikwamua kimaisha," alisema Benson.

Alisema taratibu zipo na kila sehemu na zinazofahamika, lakini kama ikitokea watu wakaendelea kukengeuka inamaanisha kuna ukiukwaji wa maadili ndani ya chama au ndani ya jamii.

"Ninavyoona haya yote yanatupa taswira ndani ya jamii yetu kuwa bado watu hawajawa na uelewa wa namna ya taratibu za kumpata kiongozi ziko sahihi zibadilishwe au kama hazifai," alisema.

Alisema kizazi hiki ni cha kuhoji wenye mamlaka, hivyo yanapotokea mambo kama hayo yanaleta taswira ambazo zina tafsiri mbalimbali.

Alisema kinachotakiwa ni elimu kutolewa ndani ya vyama na nje kwa lengo la kujenga uelewa mpana wa namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kutokana na kuwapo kwa rafu hizo, juzi Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, akitoa salamu za mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli, aliagiza uchaguzi urudiwe bila wagombea kuchukua tena fomu na wagombea wote watapigiwa kura badala ya kupitishwa kwenye kura za maoni.

"Tunaelekeza maeneo hayo ya uchaguzi urudiwe, hakuna kuchukua fomu upya, hakuna mchujo bali wote walioomba wapigiwe kura. Kokote ambako uchaguzi utarudiwa wagombea wote wataruhusiwa mfano wilaya za Kawe na Kinondoni wagombea watakuwa wote na si wale waliokwishateuliwa," alisema Dk. Bashiru.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafuatiwa na uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani utakaofanyika mwakani.

# Makonda atengua agizo la DC Ilala

INATOKA UK 2

mambo yanakwenda kinyume cha taratibu zilizopo, hivyo wakuu wa wilaya wawaite wahusika na kuzungumza nao ili wasivunje sheria.

"Lakini huwezi kupanga siku ya kumwabudu Mungu, anaabudiwa siku zote. Kwa kuwa mimi ndiye Mkuu wa Mkoa ibada nazitaka sana kuliko kitu chochote kwa kuwa huko ndiko kwenye uzima," alisema.

Hivi karibuni, Mjema alikaririwa na baadhi ya vyombo vya habari (mitandao ya kijamii) alipokuwa akihutubia wananchi ambako aliwahoji wanaotumia siku za kawaida kusali wanafanya kazi muda gani.

Katika video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii, Mjema alisema wananchi katika wilaya hiyo wanatakiwa kufanya kazi na kuzitambua siku rasmi za kufanya ibada.

"Kuna watu wanapiga mapambio Jumatatu mpaka Jumatatu. Ukiingia huko ndani watu watano, wewe Jumatatu mpaka Jumatatu unaita watu, huna watu funga," alisema.

Aliongeza kuwa: "Sisi tunajua katika kuomba ni mara hizi tatu yaani Ijumaa (Waislam), Jumamosi (Wasabato) na Jumapili (Wakristo wengine). Hizi siku zingine hakuna, marufuku, ninyi kazi mnafanya saa ngapi Jumatatu hadi Jumatatu?" Alisikika Mjema katika video hiyo.

Mapema mwaka huu, Rais John Magufuli aliweka wazi asivyofurahishwa na migogoro iliyopo kati ya viongozi anaowateua.

Alibainisha kuwa amewaweka kiporo Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wake kutokana na matendo yao ya kugombana badala ya kufanya kazi, hivyo wasifikiri kwamba hafahamu.

Rais Magufuli aliyasema hayo wakati akihutubia baada ya kuapisha viongozi wapya, katika mabadiliko aliyoyafanya kwenye wizara mbalimbali yaliyohusisha makatibu wa wizara.

Rais alisema anafahamu kuwa kuna changamoto nyingi katika utendaji wa kazi, ingawa yako mengine mazuri wanayofanya.

# Agizo la Chalamila latekelezwa magari ya jeshi

INATOKA UK 3

ombo vya ulinzi vitaendelea kulinda mali hizo ili watumishi wafanye kazi yao kwa amani na utulivu mpaka hapo watakaporidhika kuwa mazingira hayo ni salama.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alimweleza Chalamila kuwa uamuzi uliofanywa na madiwani wa halmashauri hiyo ni kuhamisha ofisi hizo za halmashauri katika kata ya Inyala baada ya mvutano wa muda mrefu.

Awali walipendekeza maeneo matatu ambayo ni kata za Santiliya, Inyala na Tembela, lakini baada ya kuyakagua waliona sehemu inayofaa kwa kukidhi vigezo ni kata ya Inyala ambako ndiko wameamua kuhamia.

"Tulikwenda kuyakagua maeneo hayo na tukaketi kufanya uamuzi wa wapi tuhamie ilipofika saa nne usiku wote tulifikia uamuzi wa kuhamia Inyala," alisema Ntinika.

Alisema anaamini kata ya Inyala itafaa kwa kuhamishia kwa muda ofisi hizo kwa vile hata watumishi wa halmashauri watapata nyumba za makazi jirani na kata hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, alisema kabla ya kumalizika kwa muda wa saa 24 aliopewa na Mkuu wa Mkoa awe amehama katikati ya Jiji la Mbeya, atakuwa tayari ameshaondoka kuelekea Inyala, mahali walikokubaliana wahamie.

Kadhalika, maandalizi yote kwa ajili ya kuhama yamekamilika baada ya Mkuu wa Mkoa kuwapelekea usafiri na kusisitiza kabla ya muda aliopewa atakuwa amewasili eneo husika.

# Shahidi adai majeruhi walichukuliwa kuhojiwa

INATOKA UK 2

ya kufungua jalada la uchunguzi nikiongoza timu ya wapelelezi wenzangu wawili nilifungua jalada la uchunguzi, nilianza kupitia hotuba kupitia video iliyorekodiwa siku ya tukio," alidai na kuongeza:

"Kabwe alikamatwa nyumbani kwake na kuletwa ofisini kwangu nilizungumza naye kirafiki na baadaye nikamjulisha haki zake na kwamba nataka kuchukua maelezo yake kama mtuhumiwa, lakini alikataa na kudai atatoa maelezo yake mahakamani."

Akifafanua zaidi alidai kuwa aliwasiliana na RCO wa Kigoma akamweleza kwamba aliwahoji watu mbalimbali waliofahamu kuuawa watu wanne wakiwamo askari polisi wawili na raia wawili na si zaidi ya 100.

"Mheshimiwa hakimu, RCO Kigoma alieleza kwamba hakuna majeruhi waliochukuliwa hospitali na kupelekwa kuuawa na polisi bali walikwenda kuhojiwa kuhusiana na tukio hilo," alidai SP Kitundu.

Akihojiwa na wakili wa utetezi Peter Kibatala, shahidi alidai kuwa hakumbuki kama kuna kifungu cha sheria kinachowataka viongozi wa siasa kuomba kibali cha kufanya mkutano na waandishi wa habari.

Alidai kuwa bosi wake aliamuru lifunguliwe jalada la uchunguzi baada ya kusikia maneno ya chuki dhidi ya serikali kutoka kwa wananchi.

Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri leo.

Katika kesi ya msingi, Zitto anakabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi, anadaiwa kutenda makosa hayo, Oktoba 28, 2018 katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya chama cha ACT Wazalendo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI

KIVUKONI/KINONDONI

SHAURI LA MADAI NA.122 YA 2019

ACCESS BANK TANZANIA LTD ..................................MDAI

DHIDI YA

DEOCAR BAZIL CHACKY..................................MDAIWA

KUITWA SHAURINI

Kwa:

DEOCAR BAZIL CHACKY

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameainishwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika Mahakama hii kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **13/11/2019** saa mbili (2:00) kamili asubuhi mbele ya Mheshimiwa **H.Hudi- Hakimu Mkazi** kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIA:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe **16 mwezi Oktoba 2019.**

HAKIMU MKAZI

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI

KIVUKONI/KINONDONI

DAR ES SALAAM

215473702



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
KIVUKONI/KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA. 118 YA 2018/9

ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ..................................MDAI

DHIDI YA

GASO GROCERY LIMITED ..................................1ST MDAIWA

GASPER JOHN URASSA ..................................2ND MDAIWA

SOPHIA MUSSA SELEMAN ..................................3RD MDAIWA

STEPHEN JASON MBOSA ..................................4TH MDAIWA

Kwa: GASPER JOHN URASSA

DAR ES SALAAM

Kwa kuwa Mdai ameleta Madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika Nakala za Madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii. Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya Jumatano tarehe **06 Mwezi wa 11 Mwaka 2019 Saa 8.30 Asubuhi.**

Kwa Mujibu wa Madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukuta shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili yakujitetea katika shauri hilo.

ANGALIA:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 2 Mwezi 10 Mwaka 2019.

HAKIMU MAKAZI

KIVUKONI /KINONDONI

DAR ES SALAAM

215473702

# Wavuvi walia na sheria ya usajili

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WAVUVI na wadau wa sekta hiyo wameiomba serikali kubadili sheria ya kusajili, kuanzisha na kufungua akaunti kwa ajili ya vyama vya ushirika wa wavuvi.

Aidha, walisema wanaomba wapatiwe washauri pamoja na watalaamu wa kuwashauri kwenye miradi mbalimbali na kuitaka serikali pia iwahimize watendaji wa ushirika kuacha kukaa ofisini na badala yake wawafuate wavuvi katika maeneo yao ya kazi kwa ajili ya kuwapatia elimu ushirika.

Ombi hilo lilitolewa na wanachama wa Butuja Saccos ambao ni wavuvi wa ndoano wa mwalo wa Butuja uliopo wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wakizungumza na Nipashe jijini hapa.

Katibu wa Butuja Saccos na Mwenyekiti wa vikundi vya usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi (BMU) Butuja, Dickson Maila, alisema wana nia ya kuanzisha na kusajili chama chao cha ushirika lakini changamoto ni sheria yake ambayo inawataka kuwa na milioni tano hivyo kuiomba serikali kabadili sheria hiyo.

"Tuna nia ya kuunda ushirika wa wavuvi Butuja ila sheria ya ushirika ambayo inatutaka ili tusajili chama na kufungua akaunti ni lazima tuwe na Sh. milioni 5.0"

Alisema maelekezo hayo waliyapata kutoka kwa Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Ilemela hivyo hawajui kama ni kweli au aliwapiga changa la macho kwa vile yeye ni mtaalamu wa serikali hivyo kuwalazimu kuyafuata.

Aliongeza kuwa, fedha hiyo wameanza kuitafuta sasa ni mwaka, hivyo wakashauri ngazi husika kurekebisha sheria ya ushirika hata kama chama kitakuwa na milioni mbili kisajiliwe.

Alisema kama ingekuwa kusajili ni milioni mbili hata Butuja wangesajili na wameanza mchakato wa kutafuta hiyo milioni tano ili wasajili.

Alisema, ili wavuvi wahamasike kuanzisha na kusajili vyama vya ushirika katika maeneo yao hususani wanaotumia ndoano elimu juu ya ushirika inapaswa kutolewa na wataalamu hao.

"Shida ni elimu kwani wataalamu wa ushirika wanakaa zaidi ofisini nakusahau kuja kutoa elimu kwa wananchi wenye adhima za kujiinua kiuchumi," alisema.

Katibu wa BMU ya Butuja, Emmanuel Nyagwesi, alisema katiba imekamilika wanachosubiri ni kupeleka kwa mwanasheria kabla ya kuiidhinisha kisha wasajili ushirika wao muda wowote kuanzia sasa.

"Tunaomba tukishasajili ushirika wetu tuelekezwe ni wapi serikali itakuwa imetuwekea mkono yaani ni benki gani na sehemu ipi ambayo itaweza kutupatia mkopo kwani shida ni mtaji tukipata fedha tutapanua wigo wa biashara."

Kaimu Mwenyekiti wa Butuja Saccos, Khamisi Ramadhani, aliiomba, serikali iwaangalie kwa jicho la pili na iwasaidie kwa kuwaagiza walimu, wanao husika na ushirika wawatembelee.

# Uhaba elimu ya kisheria waongeza malalamiko

**Na Happy Severine, BARIADI**

ONGEZEKO kubwa la malalamiko na migogoro ya wananchi katika ofisi za viongozi wa ngazi ya mikoa na wizarani, limeelezwa kuwa ni matokeo ya ukosefu wa elimu ya masuala ya kisheria.

Akisoma taarifa fupi ya hali halisi ya utoaji huduma ya msaada kisheria jana, katika ufunguziwa Wiki ya Msaada wa Kisheria Kitaifa inayofanyika katika viwanja vya Halmashauri mjini Bariadi, Msajili wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria, Felister Mushi, alisema bado wananchi wengi wanakutana na changamoto za kupata haki zao kisheria.

Mushi alisema wananchi na wasaidizi wa kisheria hawana uelewa wa kutosha kuhusu msaada wa kisheria hali inayosababisha uwapo kwa malalamiko mengi kwa viongozi katika ngazi ya mikoa na wizarani.

"Wananchi wengi na wasaidizi wa kisheria hawana uelewa wa kutosha wanamnaya kushughulikia malalamiko yao yanayohitaji msaada wa sheria na cha kushangaza wasaidizi hao wanafanya kazi bila kujua wanatatua vipi malalamiko hayona hali hiyo imesababisha ongezeko la changamoto za mengi kutotatuliwa," alisema.

Naibu Waziri Ofisi wa Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Anthony Mavunde, alisema ni vema viongozi wa kisiasa wakatembea na wataalamu wa kisheria na sekta mbalimbali wanapofanya ziara zao za kikazi ili wawasaidie kutatua malalamiko yatakayojitokeza na kupunguza migogoro hiyo.

"Viongozi wenzangu wa kisiasa nawaomba mkiwa mnafanya ziara zenu za kikazi, mtembee na wataalamu wa idara mbalimbali pamoja na wanasheria ili wananchi wasaidiwe kutatua migogoro hiyo kuliko kutatuachangamoto za kisiasa zaidi."

Ofisa Ardhi wa Mkoa wa Simiyu, Grace Mgombera, alisema kuwa kwa mkoa huo kumekuwa na migogoro na malalamiko mengi katika masuala la ardhi dhidi ya ndugu kwa ndugu kugombania mashamba ya familia pamoja na kuuziana mashamba kienyeji.

Alieleza kuwa wengi wao hawana elimu ya masuala ya sheria hivyo wanakutana na tatizo la kutoeleweka pale wanapowaelimisha juu ya sheria inavyoeleza na kupelekea hata wengine kwenda kushitaki mahakamani na ngazi nyingine za juu zaidi.

Aliongeza kuwa ni vema vyama vinavyohusika na usaidizi wa kisheria kupitia serikali kuendelea kuelimisha jamii juu ya sheria ili watu waweze kuzitambua na kupata haki zao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema kuwa kupitia Wiki ya Msaada wa Kisheria, wananchi watapata fursa kupata msaada na ufafanuzi na kwa mabaraza ya ardhi ngazi zote kujifunza namna ya kutatua migogoro ya wananchi wanayokutana nayo. Wiki ya Msaada wa Kisheria inayofanyika kitaifa mkoani Simiyu itatoa fursa ya kuelimisha wananchi kuhusu kupata msaada wa kisheria pamoja na kusikilizwa kwa kesi mbalimbali zilizopo maeneo mbalimbali mkoani humo.



Msamaria mwema akimsaidia mwendesha baiskeli kuzuia mzigo alioupakia usianguke, baada ya kushindwa kukimudu chombo hicho, katika Barabara ya Uhuru, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Ulinzi wa misitu ndiyo chanzo nishati endelevu

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MRADI wa kuzalisha umeme kutoka Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP) utaweza kuwa endelevu endapo uhifadhi na utunzaji wa misitu hasa ya vijijini utakuwa endelevu na shirikishi.

Meneja wa mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania, (TTCS) Charles Leonard, alisema hayo kwenye mkutano wa maofisa mawasiliano wa wizara zinazohusika na misitu, uliofanyika mjini Morogoro.

Leonard alisema, ni vema serikali ikahamasisha jamii kuhifadhi misitu ya vijijini ili miradi ya maendeleo iwe endelevu.

Alisema, mradi wa TTCS umeshirikisha wananchi wa vijiji 30 kutoka wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro kwa lengo la kuhifadhi misitu kwa mfumo endelevu na matokeo yake yameanza kuonekana na mafanikio makubwa yamepatikana na faida lukuki zimeshuhudiwa.

"Mradi wa JNHPP hauwezi kuwa endelevu iwapo misitu itaisha na njia ya kuiendeleza ni serikali kushirikiana na sisi wadau na wanakijiji kuitunza misitu, itafanya asilimia 45 ya misitu yote kuwa endelevu," alisema. Alisema, faida za mradi huo ni nyingi ambapo tangu uanzishwe mwaka 2012 hadi sasa umewezesha vijiji kuingiza zaidi ya Sh. bilioni tatu sambamba na kuimarisha uhifadhi.

Akitoa mada kwenye kikao hicho Ofisa Uhusiano wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Bettie Luwuge, alisema lengo la kukutana na maofisa mawasiliano hao ni kujiandaa kuwa na kauli moja ya uhifadhi wa mazingira.

Alisema, ana inamani kupitia maofisa hao jamii inaweza kupata taarifa za haraka na za muhimu za utunzaji na uhifadhi misitu kwa dhana endelevu.

TTCS chini ya usimamizi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO) wamehamasisha uhifadhi endelevu wa misitu hivyo serikali inapaswa kuongeza nguvu.

# Tarura yajipanga kukabili maafa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKALA wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, umepatiwa Sh. bilioni 1.033 kwa ajili ya kuboresha na kufungua barabara yenye urefu wa kilometa 911.31 kwenye maeneo yenye changamoto ya mafuriko mvua za masika zinapoanza.

Maeneo hayo yenye changamoto ya mafuriko ni Kata ya Malunga, Majengo, Nyasubi Chini pamoja na Kata ya Muhungula.

Hayo yalibainiswha jana na Meneja wa Tarura, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Job Mutagwaba, wakati akizungumza na vyumbo vya habari na kusema kuwa, fedha hizo zimetolewa na serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20.

Mutagwaba alisema kuwa, katika fedha walizozipokea, asilimia kubwa zitapelekwa katika Kata ya Majengo na kujenga mitaro maeneo yote yanayozunguka kata hiyo ili kudhibiti janga la mafuriko kutokana na sehemu hiyo kuwa bondeni.

Aidha, alisema maeneo mengi katika halmashauri hiyo yana changamoto kwa sababu wananchi wamejenga kiholela kwenye mikondo ya maji bila kuwashirikisha maofisa wa mipango miji na hii imekuwa ikisababisha maji kukwama kwenye njia zake na kuleta mafuriko.

"Tumeshakaa na maofisa ardhi na wa mipango miji na kuainisha maeneo yote ambayo wananchi wamejenga kwenye mikondo ya maji na kuwapatia viwanja sehemu nyingine na tumefanya hivi kupunguza malalamiko wakati wa mafuriko," alisema.

Pia Mutagwaba alieleza kuwa wamekuwa wakitoa elimu na kuwakataza wananchi wasinunue viwanja kiholela bila kushirikisha ofisi ya ardhi na mipango miji ili kutambua kama eneo hilo linafaa kwa ajili ya makazi nakucha kujenga nyumba pembezoni mwa hifadhi za barabara.

Katika hatua nyingine Mutagwaba alisema kuwa, wamekuwa wakiwachukua hatua za kisheria makandarasi ambao wanafanya kazi chini ya kiwango kwa kuwakata fedha kwenye malipo yao na kuhakikisha kazi inakamilika.

Alisema kuwa, mpaka sasa makandarasi watatu wameshakatwa fedha za malipo kwa kutokamilisha kazi kwa wakati na kufanya kazi chini ya kiwango huku wengi wao wakiingia kwenye miradi wakati si wataalamu.

# Thamani ya uwekezaji EPZA yafikia bil. 144/-

**Na Mwandishi Wetu**

UWEKEZAJI wa kampuni 11 zilizosajiliwa na Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA), kuwekeza katika viwanda vilivyoko kwenye maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) wilayani Bagamoyo, umeongezeka na kufikia Dola milioni 62.84 ( takribani Sh. bilioni 144.53).

Aidha, mapato ya fedha za kigeni yanayotarajiwa kupatikana kutokana na mauzo ya bidhaa za kampuni hizo nje ya nchi ni takribani Dola milioni 76.96 (karibu Sh. bilioni 177) wakati huohuo, zikizalishwa zaidi ya ajira 1,614.

Mkurugenzi wa Uwezeshaji Uwekezaj wa EPZA, James Maziku, alisema haya mjini Kibaha, mkoani Pwani katika maonyesho ya viwanda na uwekezaji yanayoendelea mkoani hapa.

Alisema uwekezaji na ujenzi wa viwanda vya kampuni mbili zilizosajiliwa katika maeneo maalumu ya uwekezaji wilayani Bagamoyo, umekamilika na kuanza kazi na nyingine zimefikia katika hatua mbalimbali.

Kampuni mbili ambazo zimekamililsha ujenzi wa viwanda ni Africa Dragon Enterprises Ltd, ambacho kilianza kazi mwaka 2017 kikijihusisha na uzalishaji wa nyaya zilizopakwa madini ya chuma.

Kiwanda kingine ni Phiss Tannery Limited kinachozalisha wa ngozi na bidhaa zake tangu mwaka 2013.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa, alisema kampuni hizi zinakutana na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa miundombinu ya viwanda na usafiri na ugumu wa kuuza katika soko la ndani na la Afrika Mashariki.

Maziku alisema uwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji wa Bagamoyo upo katika hatua za mwanzo kabisa huku ukikumbwa na changamoto kama kukosekana kwa umeme, maji, usambazaji wa gesi katika eneo lote la mradi.

"Serikali ndiyo yenye jukumu la kuweka miundombinu hii katika maeneo maalum ya uwekezaji ya Bagamoyo ili kuongeza ufanisi na kuvutia uwekezaji zaidi. Kutokana na hii, wawekezaji wanaingia gharama zaidi ya kujenga miundombinu wezeshi," alisema Maziku.

Changamoto nyingine ni ubovu wa barabara katika eneo hili la uwekezaji ambao umekuwa ukikwamisha usafiri wa shehena kama malighafi kwa ajili ya viwanda na bidhaa kupelekwa sokoni.

Pia kampuni hizo zimekuwa zikikumbana na ugumu wa kuuza bidhaa zao katika soko la ndani na la Afrika Mashariki kutokana na kodi kubwa inayotozwa katika bidhaa wanazozalisha.

Kwa mfano, bidhaa zinazozalishwa kwenye maeneo maalum ya kiuchumi zinatozwa asilimia 23 ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ukilinganisha na asilimia 18 inayotozwa biashara ya kawaida nchini.



Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii nchini, Patrick Golwike (kulia), akiwa amebeba ndoo yenye zege pamoja na Ofisa Tarafa wa Wilaya Dodoma, Neema Nyalege, waliposhiriki ujenzi wa vyumba vya maabara vya Shule ya Sekondari Iyumbu mkoani Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wanavijiji jirani Ziwa Victoria kupata maji

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa MUSOMA**

VIJIJI 33 vilivyopo karibu na Ziwa Victoria, katika Jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara, vinatarajia kunufaika na mradi wa maji wa Ziwa Victoria, ambao sasa uko hatua ya pili kwenye utekelezaji.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, aliyasema hayo kwenye mahojiano na Nipashe, na kuongeza kuwa timu ya wataalamu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Wilaya Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa), wanapima maeneo ambayo miundombinu ya usambaji maji itapita.

"Wataalamu hao wameanza hatua ya pili ya utekelezaji wa mradi huu, ambayo ni upimaji wa maeneo ambayo miundombinu ya usambazaji wa maji itajengwa ndani ya vijiji 33 vya Jimbo la Musoma Vijijini," alisema Dk. Anney.

Vilevile, alisema, wataalamu hao wameanzia kwenye vijiji vya Kurukerege na Mkirira, Kata ya Nyegina na kisha wataendelea maeneo mengine ili kuhakikisha vijiji vyote vilivyo karibu na ziwa hilo vinapata maji.

"Vijiji vyote vya Jimbo la Musoma Vijijini vilivyoko karibu na Ziwa Victoria vimo kwenye mradi huu. Usanifu umefanyika na serikali inajipanga ianze utekelezaji wake," alisema.

Aliongeza kuwa maji yanayozalishwa na Mamlaka ya Maji Musoma (Muwasa) ni mengi, na matumizi yake kwa sasa ni takribani asilimia 50 ya maji yanayozalishwa.

Kwa upande wake Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, alishukuru serikali kwa niaba ya wananchi kwa kuanza utekelezaji wa mradi huo wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria.

"Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanatoa shukrani za dhati kwa serikali yao kwa kuanza kutekeleza miradi ya usambazaji wa majisafi na salama vijijini kwao," Prof. Muhongo alisema.

Alisema shukrani maalum zimetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, kwa kutimiza ahadi yake ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la maji la Mugango-Kiabakari-Butiama.

Mradi wa Mugango-Kiabakari-Butiama unaotoa maji Ziwa Victoria, utagharimu Sh. bilioni 70, umefadhiliwa na serikali ya Tanzania, Saudia Arabia na Benki ya BADEA na kwamba utakamilika ndani ya miaka mwili.

Aliongeza kuwa usanifu kwenye vijiji vya kata za Bugoji, Nyambono, Bugwema, Musanja na Nyamrandirira umefanyika na maombi ya fedha za utekelezaji wa mradi ya usambazaji wa maji katika vijiji hivyo yameshafikishwa serikalini na yanafuatiliwa kwa ukaribu sana.

Mbunge hiyo aliitaja miradi mingine ya maji kutoka Ziwa Victoria inayotekelezwa kuwa ni Bujaga-Bulinga-Bukima-Kwikerege, Chitare-Makojo na Suguti-Kusenyi-Chirorwe-Wanyere.

# CCM yachagua wawakilishi uchaguzi vitongoji na vijiji

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilayani Simanjiro, wamewachagua wagombea wa ujumbe na uenyekiti vijiji 56 na vitongoji 275 watakaokiwakilisha chama hicho kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wagombea wote waliochukua fomu kwenye wilaya ya hiyo, kupitia chama hicho walipitishwa bila kuchujwa likiwa ni agizo la Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Manyara.

Agizo hilo lilikuwa maalum kwa lengo la kuvunja makundi na kuepuka kupanga safu za uchaguzi wa ubunge kwenye jimbo hilo kwa mwaka 2020.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM wilayani Simanjiro, Sumleck Ole Sendeka, alisema upigaji wa kura wa kuwapata wawakilishi hao ulifanyika vizuri kwenye maeneo mbalimbali wilayani hapa.

"Hadi hivi sasa ninavyozungumza na wewe hali ni shwari na sijapata malalamiko yoyote juu ya uchaguzi tunatarajia tutamaliza salama," alisema Ole Sendeka.

Alisema upigaji wa kura za maoni si mwisho kwa kuwa kamati za siasa za matawi na kata ndizo zitateua wagombea rasmi watakaopeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Naye Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Manyara, Jacob Siay, alisema wilaya zote mkoani humo zinafanya uchaguzi wa kura ya maoni kuwapata wagombe watakaokiwakilisha chama katika uchaguzi.

Siay alisema Wilaya ya Mbulu Vijijini kutokana na jiografia ya eneo hilo, uteuzi wa kuwapata wagombea watafanya tofauti na wilaya zingine.

Alisema wilaya nyingine za Babati Mjini, Babati Vijijini, Mbulu Mjini, Mbulu Vijijini, Kiteto, Hanang' na Simanjiro, wameshakamilisha zoezi hilo.

**"Hadi hivi sasa ninavyozungumza na wewe hali ni shwari na sijapata malalamiko yoyote juu ya uchaguzi tunatarajia tutamaliza salama," alisema Ole Sendeka.**

# Familia bilionea Msuya yaondoa mirathi kortini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

FAMILI mbili za marehemu bilionea Erasto Msuya, zimekubaliana kuondoa mahakamani kesi ya mirathi na kurejea kwenye mazungumzo nje ya mahakama.

Wanafamilia hao wameamua kufanya hivyo ili kutafuta suluhu ya mgogoro wa kugombea mali uliodumu kwa takribani miaka sita tangu kifo cha mfanyabiashara huyo.

Familia hizo upande wa baba wa marehemu ukiongozwa na mama wa marehemu, Ndeshu Msuya na upande wa mke ukiongozwa na Steven Mbazi, umefikia maazimio hayo, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, katika kikao cha pamoja kilifanyika katika ofisi ya mkuu huyo wa wilaya.

Awali kikao hicho kilitawaliwa na mabishano ya pande zote, vilio na maombi ambayo yalichukua takribani saa tano kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, huku kukichagizwa na wanasheria wa pande zote mbili pamoja na mwanasheria wa ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo.

Pamoja na mabishano makali, upande wa watoto ulidai kukosa haki yao ya msingi ya mgawanyo wa mali za marehemu baba yao, wakati mali hizo zikiendelea kutafunwa na ndugu wa mke ambao walishindwa hata kuwalipia ada za shule watoto wa marehemu.

Dada wa marehemu, Dk. Esther Msuya, alimtuhumu mjomba wa watoto wa marehemu, Steven Mbazi, ambaye ndiyo msimamizi wa mali kwa sasa kuhusika kutafuna mali hizo na wanahusishwa kuwa kitu kimoja na mke wa marehemu, Miriamu Mrita.

Mbazi alituhumiwa kukataa kumlipia ada mtoto wa marehemu Glory Msuya, anayesoma nchini Canada na kusababisha binti huyo kukatiza masomo yake na kuanza kufanya vibarua ili apate fedha za kujikimu kimaisha.

Dk. Msuya anataka watoto wagawiwe mali za marehemu baba yao ili kila mmoja amiliki mali zake na kuendelea na masomo kwa kuwa hivi sasa mtoto mkubwa wa kiume, Kelvin, naye ameshindwa kuendelea na masomo nchini Australia baada ya kurejeshwa nyumbani na wajomba zake.

Dk. Msuya alimwonyesha mkuu huyo wa wilaya majibishano ya ujumbe wa simu yaliyokuwa yamechapishwa, kati ya Glory na mjomba wake Mbazi alivyokataa kulipa ada kwa maelekezo ya Miriam ambaye ndiye mke wa marehemu.

Akijibu tuhuma hizo, Mbazi alisema walikataa kulipa ada ya Glory baada ya kumtaka awatumie matokeo ya mtihani yanayoonyesha shule anayosoma lakini aliposhindwa kufanya hivyo, walimshauri arejee nchini aje kusoma vyuo vya ndani na alipokataa ndipo walipoamua kuacha kumtumia ada.

Dada mwingine wa marehemu, Antuja Msuya, aliangua kilio wakati akimweleza Muro kuwa serikali ikague akaunti za benki kwa pande zote mbili ili kubaini ndugu waliojimilikisha mamilioni ya marehemu kaka yake kinyume cha utaratibu, huku akitaka taarifa ya mapato na matumizi ya hoteli ya SG Resort itolewe tangu kifo cha kaka yake kilipotokea mwaka 2013.

Mama wa marehemu, Ndeshu Msuya, alisema wakiwa wazazi wa marehemu, wamekubali kuondoa kwa muda shauri hilo la mirathi mahakamani ili kurejea kwenye meza ya mazungumzo.

Alisema hakubaliani na mali za marehemu mtoto wake kusimamiwa na ndugu wa upande wa mke ambao wamejazana na kujimilikisha sehemu ya mali hizo ikiwamo hoteli ya kitalii.

Aliongeza kuwa wazazi hawana nia ya kupoka mali za marehemu ila wanachopigania ni haki ya urithi wa mali za watoto wanne walioachwa na marehemu ambazo hadi sasa hazijagawanywa huku ikidaiwa kuwanufaisha ndugu wa upande mmoja wa mke wa marehemu.

"Nitakwenda mahakamani na mwanasheria wangu tukaiondoe kesi ya mirathi kwa muda ili kurejea kwenye meza ya mazungumzo," alisema Ndeshu.

Awali mtoto mkubwa wa marehemu, Kelvin, alisema kuwa yuko tayari kukaa meza ya mazungumzo na upande wa wazazi wa baba yake na kuwataka ndugu hao kuwa na upendo na mama yake anayesota gerezani kwa kesi ya mauaji kama ambavyo wanavyodai wana upendo naye.



Mchuuzi wa dawa za kuua mende, akimhudumia mteja wake, katika eneo la chini ya Mti, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# RC Mnyeti azindua barabara ya mil. 300/-

**Na Allan Isack, KITETO**

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amezindua barabara za Wilaya ya Kiteto zenye urefu wa kilomita 19.14, zilizotengenezwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 300.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) Wilaya ya Kiteto, Mhandisi Edwine Magiri, akizungumza baada ya kuzinduliwa kwa barabara hizo, alisema zilifanyiwa matengenezo kuanzia Aprili hadi Julai, mwaka huu.

Magiri alisema barabara hizo zimewekewa changarawe na zingine zimefanyiwa ukarabati wa kawaida.

Hata hivyo, alisema ujenzi wa barabara hizo umefanyika kwa kiwango cha juu na kuwekewa makalavati 22 na madrifti mawili.

"Kazi zimefanyika kwa wakati kwa kiwango kinachotakiwa pia kwa kufuata vipimo vinavyotakiwa kwani tulisimamia ujenzi ipasavyo wakati kazi ikiendelea," alisema Magiri.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa barabara hizo, Mnyeti aliwapongeza Tarura kwa matengenezo ya barabara hizo.

Mnyeti alitoa wito kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara hizo, kuwa na utamaduni wa kusafisha mazingira ili barabara hizo ziwe safi kila mara.

"Kuna ule utaratibu wa kufanya usafi kila mwisho wa mwezi. Tumieni nafasi hiyo kuhakikisha mnaondoa uchafu uliopo pembezoni mwa barabara hasa katika mitaro ya maji," alisema Mnyeti.

Licha ya kuzungumza hayo, alitumia nafasi hiyo, kuwapongeza makao makuu na mkoa wa Manyara kwa jitihada zao za kutengeneza na kukarabati kwa wakati barabara za mkoa huo.

# Mchakato wa mbinu kuvutia utalii

**Na Godfrey Mushi, SAME**

SERIKALI imeanza mchakato wa kutafuta mbinu mbadala za kuvutia sekta ya utalii hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Msitu wa Hifadhi ya Asili wa Chome maarufu kama Shengena, baada ya kuita watu wa utamaduni na sanaa kutunga nyimbo za hamasa ili kuvutia utalii wa ndani.

Katika taarifa yake jana, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema uamuzi huo unalenga kuinua mapato ya hifadhi hizo na kuongeza idadi ya watalii au Watanzania wanaozitembelea kila mwaka.

"Tumetoa hadidu za rejea kuhusu aina ya nyimbo tunazozitaka kwamba ni lazima ziwe na maudhui ya utalii na mvuto wake uguse hisia za wasikilizaji au watazamaji wa mikanda ya video," alisema.

Pia, serikali imetoa mwongozo kama huo pia wa kutungwa kwa nyimbo za kuhamasisha uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Zimo pia nyimbo za kuhamasisha uwekezaji katika sekta mbalimbali, afya ya uzazi salama, kupiga vita mimba za utotoni, ukeketaji, ukatili wa kijinsia na umuhimu wa kuvutia watoto wa jamii za wafugaji kuandikishwa darasa la kwanza kupata elimu ya msingi.

Nyimbo zinazotakiwa kutungwa zinatakiwa kuwa katika miondoko ya muziki wa kizazi kipya maarufu kama bongo fleva, dansi, ngoma za asili au nyimbo zenye mahadhi ya dini.

Hivi karibuni, mfanyabiashara wa sekta ya usafirishaji mkoani Kilimanjaro, Hussein Abdallah maarufu kama Kilenga, alianza kazi maalum ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya Wilaya ya Same.

Wilaya hiyo ina vivutio adimu vya utalii katika kilele cha Msitu wa Hifadhi wa Shengena, vivutio vya asili na maisha halisi ya ndege aina ya tai na faru weusi ambao hawapatikani katika mbuga nyingine za Tanzania wanaoishi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Alipoulizwa dhamira yake ni ipi katika suala la utalii, Kilenga alisema: "Dhumuni kubwa la kuanzisha kikundi changu cha Lukungu Sanaa Group ni kuhakikisha naitangaza vyema Wilaya ya Same pamoja na vivutio mbalimbali vilivyopo, kuelimisha, kuburudisha, uhamasishaji utunzaji mazingira na kuuenzi utamaduni wa kabila la Kipare."

Katika kutekeleza adhima ya kuvutia utalii, Mkuu wa Wilaya hiyo, Senyamule, alitangaza kuwa ofisi yake itaitisha kongamano la wadau wa utalii, kujadili namna bora ya kuchochea hamasa itakayovutia wageni kutoka nchi mbalimbali duniani kuitembelea Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Msitu wa Hifadhi wa Shengena.

# Prof. Sife Makamu Mkuu mpya MoCU

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

SPIKA mstaafu wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa, amemthibitisha rasmi Prof. Alfred Said Sife, kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), baada ya kuwabwaga wenzake saba katika kinyang'anyiro hicho.

Msekwa ambaye ni mkuu wa chuo hicho, alitangaza jana uteuzi huo baada ya Prof. Sife kuwashinda wenzake katika mchakato wa kuwatafuta na kuwapima, wanataaluma wengine ambao ni maprofesa kutoka vyuo vikuu sita nchini.

"Sasa namtangaza rasmi Prof. Alfred Said Sife, kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na uteuzi wake unaanza leo (Oktoba 21, 2019).

"Mchakato wa kumtafuta ulikuwa ni shirikishi na ulihusisha wadau wote na matokeo yake mchakato huo umezaa matunda. Mchakato huu wa kumtafuta Makamu Mkuu wa Chuo ulianza rasmi Aprili 29, mwaka huu. Siku ambapo Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, George Yambesi alipounda kamati ya wataalamu kubaini wanataaluma ambao wanafaa mmojawapo kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushiika Moshi."

Prof. Sife aliwabwaga katika kinyang'anyiro hicho wasomi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Nafasi hiyo ya Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ilikuwa wazi tangu Prof. Faustine Bee, alipoteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Machi mwaka huu.

Aprili 2, mwaka huu, Msekwa alimteua Prof. Sife aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Taaluma), kukiongoza chuo hicho kwa muda wote ambao watakuwa wanamtafuta mkuu wa chuo atakayeshika mikoba ya Prof. Faustine Bee.

Wakati anatangaza uteuzi huo mbele ya wanataaluma, watumishi na serikali ya wanafunzi wa chuo hicho, Msekwa alisema:

"Kamati yangu iliyokuja na majina na mapendekezo yao ya nani anastahili kuwa Makamu Mkuu wa chuo chetu cha Ushirika Moshi, ilikuwa na wajumbe watatu ambao ni wanataaluma waliobobea, Profesa Lucian Msambichaka ambaye ndiye mwenyekiti wa kamati ile na wajumbe wake wawili ni Profesa Gerald Monela na Profesa Joseph Kuziwa."

Kwa mujibu wa Msekwa, kamati hiyo ilikubaliana kuwatafuta wanataaluma popote pale yaani ndani na nje ya nchi, lakini ilibidi wazingatie mwongozo uliotolewa katika kanuni husika na kamati hiyo ilifanikiwa kupata jumla ya wanataaluma wanane, wawili wanatoka MoCU na sita wanatoka vyuo vikuu vingine.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula (katikati), akipata maelezo kutoka kwa mhandisi anayesimamia ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Peter Mwaisabura, alipokagua mradi huo, juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya. **PICHA: WANMM**

# TaCRI yafichua athari matumizi ya GMO

**Na Godfrey Mushi, HAI**

TAASISI ya utafiti wa zao la kahawa nchini (TaCRI), imesema matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba maarufu zaidi kama uhandisi jeni (GMO), haukidhi matakwa ya kisayansi na huenda ikitumika ikaathiri ubora wa kahawa.

Mtaalamu wa uboreshaji wa kahawa kutoka katika taasisi hiyo,Dk. Damian Mtenga, alisema uhandisi jeni haufai kutumika katika zao hilo.

Alikuwa akizungumza jana, mbele ya Waziri wa Kilimo, Joseph Hasunga, aliyekwenda katika taasisi hiyo kuzindua vitabu vitatu vya kuelimisha wakulima na maofisa ugani wa kahawa.

Matumizi ya mbegu za GMO, yamekuwa yakipingwa mara nyingi na wadau, mashirika ya kiraia na taasisi binafsi zinazojishughulisha na kilimo kwamba zisiruhusiwe kutumika hapa nchini.

TaCRI imepinga vikali matumizi ya mbegu za GMO), ikisema kuwa mfumo huo haukidhi matakwa ya kisayansi na huenda ikaathiri ubora wa kahawa katika soko la Kimataifa.

Matumizi ya mbegu za GMO yalianza kupigiwa chapuo na mashirika ya kilimo ya nchi za kigeni, kutokana na kuwapo kwa mabadiliko ya tabia nchi yanayochagizwa na kukosekana kwa mvua.

Inaelezwa na baadhi ya wataalamu wa mazingira nchini kwamba mabadiliko hayo ya tabianchi yamekuwa yakiendelea kuathiri sekta ya kilimo nchini ambayo sasa inakabiliwa na ukame pamoja na wadudu waharibifu wa mazao.

Hata hivyo, mapendekezo ya wadau na tafiti za kisayansi zinadokeza kuwa matumizi ya teknolojia ya mbegu za GMO, huenda ikawa mwarobaini wa kuongeza uzalishaji wa mazao na hata kumaliza changamoto zinazowakabili wakulima.



Ukurasa 14

**Mila kizingiti wanawake mkoani kwenye uchaguzi**

Rushwa inavyokwamisha wanawake Zanzibar kuwania nafasi za uongozi



Ukurasa 18



Ukurasa 20

**Hali tete licha ya Marekani kuepusha vita ya Uturuki, Syria**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 23, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 17

**Rais Putin: Nchi za Magharibi zinalaghai mataifa ya Afrika!**

MIAKA 20 KUMBUKIZI YA MWALIMU NYERERE;

## Nakubali tusijikweze, tunyenyekee

**Na Dk. Felician Kilahama**

AWALI ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Tunaishi na imekuwa hivyo kwa rehema na mapenzi yake.

Sasa miaka 20 tangu kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Kimsingi alikuwa mtu wa pekee siyo tu kwa taifa letu hata kwa Bara la Afrika.


Mchango wake katika harakati za kuleta usawa unafahamika na kuheshimiwa na wengi waliopata fursa ya kuwa karibu naye.

Hakuwa mbinafsi wala wa kunyenyekea kirahisi kwa mantiki ya kunyenyekea tu, bali alisimama kwenye ukweli na akapigania uhuru wa Mwafrika ipasavyo.

Sasa ni miaka 20 tangu Mwalimu atutoke, yapo mengi aliyoyafanya kwa Tanzania na Bara la Afrika.

Hata hivyo, kupitia fursa mbalimbali ikiwamo makongamano, mikutano ya hadhara, mitandao ya kijamii na kwenye vyombo vya habari; tumekuwa tukikumbushwa Mwalimu alifanya nini kwa Tanzania.

**INAENDELEA UK.16**



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

**Yamefanywa makubwa kuibeba Tanzania na vizazi vya kesho** Ukurasa 15

# Mila kizingiti wanawake mkoani Shinyanga kwenye uchaguzi



Mbunge wa Ilemela ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Angelina Mabula, ni mmoja wa wanasiasa kutoka Kanda ya Ziwa, ambako mila kandamizi zinafifisha ndoto za wanawake kugombea nafasi za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UTAMADUNI ni mfumo wa maisha ambao makabila mbalimbali nchini yamejiwekea ili yaweze kuishi kwa kufuata utaratibu.

Hata hivyo, kuna mila zingine ambazo ni kikwazo kwa jinsia ya kike kwani zinawanyima sauti wanawake, hivyo kubaki kama wajakazi kwa waume zao.

Baadhi ya makabila yamekuwa yakimnyima fursa mwanamke kuwa sehemu yoyote ya maamuzi wala kutoa mchango kwenye vikao vya familia, ukoo, hata katika mikutano ya vijiji, na hivyo kubaki kuwa mtu wa kutekeleza maagizo anayopewa.

Hali hiyo ndiyo chanzo cha tatizo la mfumo dume inayosababisha wanawake walio wengi washindwe kugombea nafasi zozote za uongozi kwa kuhofia kuvunja miiko ya mila na desturi za makabila yao.

Ndiyo iliyoathiri mfumo mzima wa maisha ya mwanamke, kwamba pamoja na kupewa elimu ya ujasiri na kudai haki ya usawa wa kinjisia kwa asilimia 50 kwa 50 hata kwenye ngazi ya nafasi za uongozi, bado walio wengi wamekuwa ni waoga.

Waoga wa kuthubutu kugombea nafasi za uongozi kwenye chaguzi mbalimbali nchini.

Novemba 24, mwaka huu kuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuchagua wenyeviti wa vitongoji, mitaa, vijiji na wajumbe wao.

Aidha, kuna uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na rais mwakani huku wanawake wakihamasishwa kujitokeza kuwania nafasi hizo.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ni miongoni mwa makundi ya wanaharakati wanaohamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kwenye chaguzi hizo zijazo.

> “Wito wangu kwa wanawake wenzangu wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa Novemba 24 na uchaguzi mkuu mwakani…

Na ndiyo maana umezindua Ilani ya Uchaguzi ya Mwanamke ili kuwahamasisha washiriki kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Pamoja na hamasa hizo, bado wanawake wengi katika baadhi ya maeneo wanaogopa kufanya hivyo kwa sababu ya mila na desturi kandamizi za makabila yao.

## WAZEE

Sonda Kabeshi ni mzee wa kimila mkoani Shinyanga.

Anaeleza namna mila na desturi za kwao zilivyojenga mtazamo hasi kwamba mwanamke akiwa kiongozi, mume wake atadharaulika kwa kuonekana kwamba anatawaliwa na mkewe.

Anasema mila na desturi zinamtambua mwanamke kama mtu wa kutoa malalamiko, si maamuzi, hivyo akiwa kiongozi ataonekana amedharau wanaume wote ndani ya jamii.

“Mila na desturi zetu Wasukuma, hazimpatii nafasi mwanamke kuwa na sauti ndani ya jamii, kwani ni mtu wa kuolewa, kwenda kufanya kazi za familia anakoolewa na si kuwa mtu wa kutoa maamuzi...yeye ni wa kupokea maagizo na kuyatekeleza,” anasema na kuongeza:

“Hivyo mwanamke kuwa kiongozi, kwanza ni kuvunja miiko ya mila na desturi zetu pamoja na kuonekana hana heshima kwa wanaume, hana dharau kwa mumewe kwani mila haziruhusu awe juu ya mwanaume na kutoa maagizo.”

Aidha, anasema kama mwanamke akiwa kiongozi, hataweza kutoa huduma stahiki kwa wananchi sababu ya majukumu mengi ya kifamilia na hivyo kukosa muda wa kufanya kazi.

## DIWANI

Mariamu Nyangaka ni Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Kitangili, Shinyanga Mjini, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Anasema changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi, zinatokana na mila kandamizi zinazoendekeza mfumo dume, kutojiamini, pamoja na ukosefu wa fedha.

Anasema amekuwa akiwania nafasi ya viti maalumu badala ya udiwani wa kata, sababu ya hofu ya mfumo dume, kwamba akijitosa huenda akakosa nafasi zote.

Anabainisha kwamba kuna baadhi ya wazee ambao wameshamfuata wakimtaka agombee nafasi ya udiwani wa kata kwenye uchaguzi mkuu mwakani kutokana na uchapa kazi wake, lakini amekataa na kwamba ataendelea kugombea viti maalumu.

“Tunaiomba jamii iachane na mila kandamizi zinazoendekeza mfumo dume ili tupate fursa ya kushika nafasi kubwa za uongozi kama wanawake na si kuishia kwenye viti maalumu...tuna uwezo mkubwa wa kuongoza na kutatua matatizo ndani ya jamii,” anasema na kuongeza:

“Kwanza ni viongozi kuanzia ndani ya familia, hivyo tunapopata nafasi za kuongoza huwa ni viongozi wazuri sana...Chukulia mfano wa Mama Samia Suluhu Hassan, Ummy Mwalimu, Prof. Joyce Ndalichako na wengineo wanafanya vizuri kwenye uongozi wao.”

## MBUNGE

Azza Hilali ni Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, anawasisitiza wanawake kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la mpiga kura na kuchukua fomu za kugombea uongozi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Anasema wakati umefika wanawake kuonyesha uwezo wao wa kuchapa kazi, kwa kugombea nafasi za uongozi ili waonyeshe jinsi walivyo watendaji wazuri katika suala la kushughulikia matatizo ya wananchi.

## MTIA NIA

Habiba Jumanne ni mwanamke aliyejitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa wa Kitangili, Manispaa ya Shinyanga.

Anasema amewiwa kuchukua fomu hiyo baada ya kujiona anaweza kuongoza wananchi kushughulikia matatizo yao.

“Wanawake tusipojiamini kamwe hatutaweza kufikia 50 kwa 50 kwenye nafasi za uongozi, tunapaswa tusimame imara na ndio maana nimechukua fomu ya kugombea uenyekiti wa serikali ya mtaa na nina imani nitashinda,” anasema.

## UWT

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake CCM, Wilaya ya Shinyanga Mjini (UWT), Shambuo Katambi, anasema wao kama CCM, wameshaweka mkakati wa kuhamasisha wanawake kujitokeza kujiandikisha pamoja na kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, na uchaguzi mkuu mwakani.

Anasema katika mkakati huo wamekuwa wakitembelea wanawake maeneo mbalimbali na kufanya nao mikutano ya hadhara na ya ndani, lengo likiwa ni kutoa hamasa ili wajitokeze kujiandikisha na kugombea nafasi za uongozi kwenye chaguzi zijazo.

“Sisi kama UWT, tunatambua kuwapo kwa changamoto nyingi zinazomnyima fursa mwanamke kushika nafasi kubwa za uongozi, likiwamo suala la mila na desturi kandamizi zinazotokana na mfumo dume, rushwa ya ngono na ndio maana ya kupeana elimu,” anasema na kuongeza:

“Wito wangu kwa wanawake wenzangu wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa Novemba 24 na uchaguzi mkuu mwakani... wasiogopeshwe na changamoto zitokanazo na mila.”

Aidha, Katambi anawataka wanawake wapendane wenyewe kwa wenyewe, na kuacha tabia ya kusemana vibaya pale mwenzao anapojitokeza kuwania nafasi za uongozi, bali washirikiane naye kikamilifu pamoja na kumpigia kura nyingi za ndio ili ashinde na hatimaye awainue kidedea wanawake wenzake.

“Kuna tatizo kubwa vilevile la wanawake kusemana vibaya, kumtafutia visa mwanamke mwenzao, hasa pale anapojitokeza kuwania nafasi za uongozi, kumkalia vikao visivyo na maana ili ashindwe... nawaomba waache tabia hiyo, washikamane,” anafafanua.

## CCM

Katibu wa CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Agnes Gregory, anataja takwimu za wanaCCM waliojitokeza kuchukua fomu za kugombea nafasi ya uenyekiti wa vitongoji kuwa ni 172, huku mwitikio wa wanawake ukiwa ni mdogo.

Anasema Wilaya ya Shinyanga Mjini, ina tarafa sita ambazo ni Kolandoto, Kizumbi, Mwamalili, Old Shinyanga, Ibadakuli, na Mwawaza.

MIAKA 20 YA BILA MWALIMU:

# Yamefanywa makubwa kuibeba Tanzania na vizazi vya kesho



Moja ya miradi mikubwa tunaposherehekea miaka 20 ya bila Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ni ya ujenzi wa reli ya kisasa katika viwango vya kimataifa (SGR) kama inavyoonekana. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

KUMBUKIZI za Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa, aliyewaacha Watanzania miaka 20 iliyopita, zinaendelea kuadhimishwa, huku taifa likiwa katika harakati za kukihakikishia kizazi kijacho maisha bora na mafanikio makubwa.

Tumaini jipya linalokipa kizazi kijacho maisha mema ni ujenzi wa kisasa wa miundombinu ya reli, barabara, madaraja, bandari na viwanja vya ndege.

Miundombinu hiyo inalihakikishia taifa usafirishaji wa watu na shehena kubwa, tena kwa tija sasa lakini zaidi miaka ijayo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, kipande cha kilometa 300 za SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, kitaanza kutumiwa Desemba mwaka huu.

Huo ni mwanzo, reli hiyo ya kisasa yenye kutumia umeme kukokota mabehewa itajengwa zaidi ikiwa na kilometa 1,219 kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Ni kazi inayotarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitano na pia itaunganishwa na matawi ya Kigoma na Mpanda.

Aidha, Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam umejengwa kisasa na umekamilika ukiwa na sura mpya. 'Terminal Three,' ndilo jina la uwanja huo mpya, wenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni 3.5 na hudumia nyingine lukuki.

Hiyo ni kazi ya awamu ya kwanza, wakati awamu ya pili inatarajia kuuboresha ili kuhudumia abiria milioni sita.

Yote hayo ni mafanikio kwa kizazi kijacho ambacho kitakuwa na ajira zaidi, kuanzia waongoza ndege, marubani, wahudumu na wawekezaji uwanjani hapo.

Fedha zitakazopatikana kutokana na abiria wakiwamo watalii ni hakikisho la mapato makubwa ya serikali kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Kasi ya kuboresha miundombinu inakwenda pamoja na kusambaza umeme nchi nzima na kwamba mwaka 2025, kila kijiji cha Tanzania kitakuwa kimepata umeme kupitia mpango wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Mawasiliano hayo ya angani, ardhini na uwepo wa nishati ya umeme yanakuwa na tija zaidi kwa kuwa taifa limejizatiti kuimarisha mawasiliano ya simu na intaneti baada ya kujengwa na mkonga wa taifa.

Taarifa za mtandaoni zinaonyesha kuwa takribani Watanzania milioni 30 wanatumia simu za mkononi pamoja na intaneti, kufanikisha mikakati mbalimbali kama biashara, kilimo, masoko, uwekezaji na wanafunzi kujisomea shuleni na vyuoni.

**SERIKALI KUGHARAMIA ELIMU**

Miaka 20 bila Mwalimu inashuhudia serikali ikibeba mzigo wa kusomesha watoto wote kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne.

Katika majukwaa mbalimbali ya kisiasa Rais John Magufuli, anaeleza kuwa zaidi ya Sh. bilioni 24 hutumiwa kila mwezi kusomesha watoto hao jukumu lililoanza rasmi kutekelezwa Januari, 2016.

> "Fedha zitakazopatikana kutokana na abiria wakiwamo watalii ni hakikisho la mapato makubwa ya serikali kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Hatua hiyo inaongeza idadi kubwa ya wanafunzi vyuo vikuu na kuifanya Tanzania kuwa na wasomi wengi miaka ijayo.

Yote hayo yanatimiza azma ya Nyerere ya kufuta ujinga, aliyoitekeleza wakati wa uhai wake kwa kutoa elimu bure kuanzia ngumbaru (watu wazima), shule za msingi, sekondari hadi vyuo vikuu.

**KUREKEBISHA MIKATABA TATA**

Katika kipindi hicho cha miongo miwili bila Mwalimu, kizazi kijacho kimepewa nafasi ya kufurahia maliasili za taifa hasa madini, baada ya mikataba tata ya madini kufumuliwa upya ili ilinufaishe taifa.

Mambo mengi yamewekwa sawa na awamu ya tano ili madini yafaidishe Tanzania ya leo na ya miaka ijayo.

Mikataba ya madini ambayo kulikuwa na unyonyaji na uporaji wa mali za umma imerekebishwa na sheria mpya zimeandikwa zikitaka serikali kuwa na hisa ya asilimia 50 kwa kila uwekezaji wa madini unaofanywa na kampuni za kigeni.

Kazi hizo za kupambana na ufisadi na unyonyaji kwa kurekebisha mikataba tata iliyokuwa inalinda maslahi ya kibeberu imezuia usafirishaji wa dhahabu na mchanga wenye madini.

Jukumu la kuondoa vipengele 'vibovu' vya kinyonyaji na kuunda upya mikataba hiyo, vimeipa tija Tanzania hasa kizazi kijacho ambacho kitanufaika na maboresho hayo. Kizazi hicho kitaendelea kunufaika na madini ya tanzanite baada ya serikali kuweka ukuta na kudhibiti utoroshaji madini hayo ili uchimbaji na mapato yawe endelevu.

Ndani ya kipindi hicho vijana wa kizazi kipya wameona jinsi ya kuleta uadilifu na uwajibikaji ndani ya serikali.

Utendaji wa ovyo ovyo umerekebishwa na mikataba yenye walakini na uchukuaji wa fedha za mikataba ya kuzalisha umeme wa IPTL na kashfa ya akaunti ya ESCROW zimehojiwa mahakamani.

**VITENDAWILI VINAVYOSUMBUA BAHARI BILA TIJA**

Mwalimu ameiachia Tanzania bahari kubwa yenye samaki wa kila aina na utajiri wa rasilimali bahari, lakini tangu kifo chake hadi sasa licha ya kuundwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tanzania haijaweza kuwa na meli za kisasa za kuvua kwenye bahari kuu.

Ni wazi kuwa tangu Nyerere alipoondoka taifa halijaweza kutajirika na bahari hasa uvuvi wa maji ya kina.

Utajiri huo kuna madai kuwa unaliwa na wajanja wa kimataifa wenye meli kubwa na teknolojia za kisasa. Hili nalo ni vyema serikali ikalitazama. Kama inavyonunua ndege za kisasa iangalie uwezekano wa kununua 'trawlers' za kuvua maji ya bahari kuu.

Mamlaka ya Bahari Kuu ina deni kwani haijafanya vya kutosha kufanikisha juhudi za kuwafanya Watanzania kunufaika na rasilimali ya bahari.

Licha ya Tanzania kuwa ukanda mrefu wa bahari kuanzia Tanga hadi Mtwara na visiwa vyenye utajiri wa kutosha vya Mafia, Unguja na Pemba, bahari haijabadilisha hali duni ya wananchi wa ukanda huo.

Bahari ya kina kwa Tanzania ni maarufu kwa samaki wakubwa (big game fish) kama papa, jodari. Wengine ni barakuda.

**KILIO CHA AJIRA**

Licha ya taifa kuwa na vyuo vikuu na vingine vingi vikiwamo vya ufundi stadi, elimu imeshindwa kuwaandaa vijana kujitegemea kutokana na taaluma na maarifa waliyoyapata.

Vyuo vikuu vingi kama cha Nelson Mandela, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa MUCE na Dar es Salaam DUCE, na taasisi za elimu kama ya Dar es Salaam (DIT) ) vimeanza baada ya mwaka 1999.

Hata hivyo, licha ya utitiri wa vyuo vya elimu ya juu, vya kati na taasisi za kiufundi wahitimu wa Tanzania wana kilio cha kukosa kazi na kushindwa maisha yao kwani hawajaweza kujiajiri.

Mwalimu alitaka elimu ya Tanzania iwe ya kujitegemea ili watu waweze kumudu maisha yao, ndoto hiyo haijatimia jitihada zaidi zinahitajika kufanyika na kuchukuliwa kutatua tatizo hilo ikiwamo kuanzisha viwanda na programu nyingi zaidi za ujasiriamali.

**MTIHANI WA KILIMO**

Licha ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, kukienzi kilimo na kukitangaza kuwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, bado hakijaweza kutimiza azma hiyo.

Kilimo bado kinatumia zana za kizamani, hakijawa cha kisasa kinachotumia teknolojia. Mazao ya wakulima hayana masoko ya uhakika na wakati mwingine hukosa wa kuyanunua na hata kuuzwa kwa bei ya kutupwa.

Walanguzi wa mazao wanaendelea kuwanyonya wakulima na hata kuwalazimisha kuuza mazao yakiwa shambani.

Yote haya yataondoka baada ya serikali na wadau kuweka miundombinu ya kisasa kuanzia zana, teknolojia, masoko, maghala, viwanda na barabara zitakazokifanya kilimo kuwa rafiki badala ya mwenza 'msumbufu.'

Hata hivyo katika miaka 20 ya Tanzania bila Mwalimu, mengi yamefanyika ambayo yanaakisi mtizamo wa Mwalimu wa kuwa na Tanzania inayojitegemea na yenye maendeleo endelevu.

# Nakubali tusijikweze, tunyenyekee

INATOKA UK.13

Kikubwa kinachosisitizwa ni amani. Mwalimu alikazania sana utu wetu na amani kwa faida ya watu wote.

Hakuishia hapo pia aliamini kuwa baada ya kupata uhuru Desemba 9, 1961, hatutakuwa na amani kamili iwapo majirani zetu wataendelea kutawaliwa na kukandamizwa na wakoloni.

Hivyo, nguvu nyingi zikaelekezwa kuikomboa Afrika na suala la kunyenyekea halikuwapo.

Tulikuwa tunadai uhuru wa Afrika na alisema tutafanya hivyo kwa nguvu na uwezo wetu wote.

Mungu mwema, haikuchukua muda mrefu Afrika yote ikawa huru na kukomesha ubaguzi wa rangi.

Wakati akipigania uhuru wa Afrika, pia aliendelea kujenga Taifa lenye umoja, nguvu na mshikamano na Aprili 26, 1964 ikaunganishwa "Tanganyika" na Zanzibar ikazaliwa Tanzania.

Yeye akawa kiongozi Mkuu (Rais) wa kwanza wa Tanzania akisaidiana na Rais wa Zanzibar.

Muungano wetu ulilenga zaidi kuimarisha uhuru na ujirani wetu na kuhakikisha uwepo wa amani ya kutosha kwa kuzingatia taifa imara lenye nguvu kijeshi kuimarisha ulinzi na usalama.

Wakati huohuo kukawa na itikadi ya chama kimoja na sera ya kujenga "Ujamaa na Kujitegemea."

Tukajua kuwa "Ujamaa ni utu na Upebari ni unyama" na siyo hivyo tu hatua zaidi za makusudi zikachukuliwa tukataifisha baadhi ya mali (kama nyumba) ambazo zilipatikana kinyemela.

Katika kufanikisha hivyo, kulikuwa hakuna cha kunyenyekea na kama ilikuwa kujikweza sijui mradi nia ilikuwa kujenga taifa lenye haki na usawa kwa kupunguza nguvu za "wenyenavyo na wasionavyo".

Yawezekana serikali ya awamu ya tano kwa namna moja au nyingine inajaribu kumuenzi Mwalimu kwa kulifanyia kazi jambo hilo.

Vilevile, jitihada za makusudi zilifanyika tukaanzisha "Vijiji vya Ujamaa" sehemu mbalimbali nchini na 1967 Azimio la Arusha likawekwa kama muhimili wa kuiongoza Tanzania wakati wa utawala wa chama kimoja.

Zoezi la kuanzisha vijiji vya ujamaa (ambavyo sasa vinafahamika kuwa ni vijiji tu baada ya kuweka Sera na Sheria ya Ardhi ya Vijiji 1999); lilifanyika kwa lengo la kuweka Watanzania pamoja ili serikali iweze kuwapatia huduma za kijamii (elimu, afya, maji, kujenga miundombinu na masuala ya ugani) kirahisi kuliko ilivyokuwa watu wametawanyika, kila mtu na lwake kiasi cha kufanya kazi hiyo iwe ngumu sana.

Kwa mtazamo huo nia ya Mwalimu Nyerere ilikuwa nzuri kwa faida ya wote.

Hata hivyo katika kuanzisha vijiji vya ujamaa, hakukuwapo mkazo kwa unyenyekevu wala kujikweza (unajikweza au kunyenyekea kwa nani na kwa jambo lipi).

Tulihitaji watu wawe pamoja kwa faida ya wote. Sasa vijiji vipo na huduma za kijamii zinafanyika ipasavyo kwa sababu vilianzishwa bila malumbano.

Hatukuishia hapo kukateuliwa "Mameneja wa Vijiji" ili kusimamia maendeleo vijijini.

> Lazima tukubali kuwa kuna masuala muhimu ya kitaifa (kama hili la Muungano) ambayo ukiachia hisia na matakwa ya kila mtu yatawale, taifa litayumba.

Katika kufanikisha suala hili, kulikuwa hakuna kuulizana maswali. Mtaalamu alipewa barua nenda kijiji fulani wewe sasa ni meneja wa kijiji na ikawa hivyo.

Hakuna hata aliyethubutu kuuliza sasa naenda kufanya kitu gani huko wakati mimi sina utaalamu wowote kuhusu umeneja wa kijiji. Sasa siyo mameneja ni watendaji wa vijiji. Yapo kadhaa mengine yaliyofanyika lakini kwa nia njema ya kutafuta njia bora ya kuiendeleza Tanzania.

Mfano, kufuta mfumo wa halmashauri kama tulivyokuwa tumerithi kwa wakoloni na kuanzisha mifumo ya "Madaraka Mikoani" pia tukafuta "Vyama vya Ushirika" na kuweka Mamlaka za Mazao (crop authorities).

Nia ilikuwa nzuri lakini wakati wa kutekeleza yote haya, je, kulikuwa na kunyenyekea au tulijikweza?

Hakukuwa na fursa ya kufanya mashauriano na wakulima kuona kama wanaafiki kufuta ushirika na kuingiza mamlaka nyingine.

Ilionekana ni suala jema tutekeleze na ikawa hivyo kama tulijikweza hapo sijui.

Ndiyo miaka 20 bila Mwalimu imepita lakini ni kipindi cha mabadiliko makubwa kwa nchi yetu kiitikadi, kisera na kisheria.

Azimio la Arusha liko wapi? Tunu au miiko ya taifa iko wapi? Tumekumbwa na masuala tofauti na enzi ya Mwalimu: "Utandawazi"; siasa za vyama vingi; ubinafsishaji; teknohama na mitandao ya kijamii vimetukolea; mifumo ya elimu imebadilika sana; maadili ya kitanzania ndiyo hivyo.

Matokeo yake yamekuwa ni kushamiri rushwa na ufisadi, wizi wa mali za umma na kadhalika.

Ubinafsi ukaotesha mizizi na hivyo ujamaa na utu kubakia kwenye makaratasi na nadharia tu.




Rais John Magufuli akiwa katika moja ya mikutano yenye tija katika uchumi wa nchi.



Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere (aliyepunga mkono), katika moja ya mikutano yake enzi za uhai wake. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

Harakati zikawa za kila mtu kujijua na heshima ya utu wetu ikawa chini na upendo ukazorota. Unapendwa au kuheshimiwa kwa sababu ya kile ulichonacho siyo kwa utu au binadamu aliyeuumbwa kwa mfano na sura ya Mungu.

Isitoshe tunu/maadili kwa taifa tumevipiga teke sisi wenyewe. Likaanzishwa "Azimio la Zanzibar" sijui lililenga kufanikisha kitu gani kwa taifa na watu wake?

Tunaposema tusijikweze na tunyenyekee, nakubali kwa asilimia zote lakini najiuliza tunajikweza na kunyenyekea kwa nani na kivipi?

Tuangalie tulipo, wakati tunamuenzi Baba wa Taifa kwa mambo mazuri aliyotuachia.

Hata hivyo, tunafanya hivyo tukiwa kwenye hali gani kisiasa, kijamii na kimazingira?

Bahati nzuri Mwalimu alijitathmini, akajitambua mapema, akasema hapana siendelei "nang'atuka".

Baadhi yetu tulibisha kidogo lakini akasema kwa hili sinyenyekei kwa yeyote yule mimi nimeamua, naachia madaraka: Tukakubali ikawa hivyo.

Tuheshimu mawazo na kukubali hoja za wengine kama hatukubaliani tupingane kihoja: Ni sawa iwe hivyo. Lakini tuangalie pia tulipotoka mfano, kulitokea kutofautiana kimawazo na kwa mtazamo wa kitaifa kukazuka hoja ya "Tanganyika" na baadhi ya wabunge wakaunda kikundi (G55), je, kulikuwa na kunyenyekeana au kujikweza?

Mara nyingi viongozi wetu huwa wanatuasa kuwa: Suala la Muungano halina mjadala tutaulinda muungano kwa nguvu zote.

Je, kufanya hivyo ni kujikweza au kunyenyekea kunawekwa wapi?

Lazima tukubali kuwa kuna masuala muhimu ya kitaifa (kama hili la Muungano) ambayo ukiachia hisia na matakwa ya kila mtu yatawale, taifa litayumba.

Hata Baba wa Taifa wakati akiwa Rais, pamoja na kuheshimu mawazo ya wengine, alikuwa na msimamo thabiti kwa masuala yaliyohusu maslahi ya wengi, hakuruhusu watu wachache wajikakamue.

Wakati wa Azimio la Arusha walioona halina maslahi kwao walikuwa na uhuru wa kwenda walikotaka: Kulikuwa hakuna cha kunyenyekea bali kusonga mbele kwa faida ya wengi.

Mbali na hilo wakati fulani kulitokea tofauti ya mawazo na mtazamo kuhusu masuala ya wagombea urais.

Nakumbuka Baba wa Taifa aliona yataelekea kuleta mpasuko na mgawanyiko mkubwa kwa taifa letu, hivyo kupelekea kuhatarisha uhuru na amani kwa nchi yetu.

Mwalimu Nyerere alisimama kidete na wala hakuwa na subira bali alikemea kwa nguvu zote bila kunyenyekea.

Wakati fulani alitishia kurudisha kadi yake ya uanachama iwapo hatua stahiki hazichukuliwi.

Nani aliweza kusema rudisha, si tulikubali yaishe hata kama baadhi ya viongozi walikuwa hawakubaliani naye. Kuna wakati wa kunyenyekea na kujikweza, lakini siyo kwa kila jambo, lazima tuangalie mazingira yaliyopo na inakuwa hivyo kwa nia gani au kwa faida ya nani.

Tusipotoshe kwa faida binafsi bali maslahi ya wengi yatawale maamuzi, tunapokuwa viongozi.

Viongozi wanaandaliwa, hawaokotwi sawa, lakini wanaandaliwa kivipi na mazingira yapi?

Enzi za Mwalimu ilikuwa rahisi kuendesha mafunzo ya uongozi, sasa tunatofautiana kisiasa na kiitikadi ndiyo maana chuo husika kinafanya kazi tofauti na lengo lake.

Yawezekana tukarejesha hilo kwa nia ya kuwaandaa viongozi wa kesho ila iwe ni kitaaluma na siyo kisiasa.

Walengwa wakasome kulingana na mitaala itakayokubalika kwa misingi ya utawala bora. Vijana wahitimu na wawe na sifa ya kuongoza na iwapo mtu anateuliwa kuwa kiongozi mfano, Mkuu wa Mkoa au Wilaya iwe ni moja ya sifa zinazotakiwa kuwa nazo.

Serikali ya Awamu ya Tano inajitahidi sana kuwaletea Watanzania maendeleo kupitia uchumi wa viwanda na kupambana na umaskini wa miaka mingi.

Viongozi wake siyo malaika, watakuwapo wachache wa kujikweza au kukosa unyenyekevu; tuangalie hali halisi pia tukosoane kwa lengo la kuboresha isiwe ni kubeza na hali ya kuvumiliana iwepo.

Miaka mitano siyo muda mrefu wa kutekeleza ahadi ambazo wanasiasa huwa wanazitoa ili wapewe ridhaa ya kuongoza nchi.

Sasa mazingira ya kuongoza siyo yale ya enzi za marehemu. Ubinadamu umeyeyuka na hofu ya Mungu ni kitendawili. Zaidi tunajali fedha kuliko utu wala kumtii Mungu. Njiani tunapishana kama sisi siyo binadamu na baadhi wanaona jinsia moja kufunga ndoa ni jambo jema eti kwa "Misingi ya Haki za Binadamu."

Hapo kunyenyekea mbele za Mungu kupo au ndiyo kujikweza? Hali ya utii kwa sasa ni tofauti na ilivyokuwa enzi za Baba wa Taifa.

Tunataka watoto wetu shuleni walelewe na kufundishwa wanavyotaka wenyewe au kama baadhi ya wazazi wanavyopenda.

Mtoto siyo tena thamani ya jamii isitoshe hata wazazi hawana imani na baadhi ya ndugu zao wa karibu kwa kuogopa watoto kufanyiwa ukatili wa makusudi kwa maslahi binafsi. Watoto wa kike kuwa wajawazito wakiwa shuleni ni sahihi? Mwanafunzi kuwa na simu shuleni inaonekana ni bora kuliko kunyenyekea kwa walimu wao.

Maeneo kama Dar es Salaam utasikia eti wazee hawatakiwi kuwa mijini, tunaambiwa makazi yao ni Chalinze au Msata.

Je, kunyenyekea kuko wapi au ni kujikweza? Baba wa Taifa alikuwa akikemea sana udini na ukabila kwa nguvu zote, je, kiongozi akichachamaa na kukemea udini na ukabila atakuwa anajikweza?

Ndiyo maana inafika mahali viongozi wetu wanakabiliana na hali ngumu ya kukosa utii, kutowajibika na fikra za kupata fedha kirahisi bila kufanya kazi kwa bidii.

Mazingira kama hayo yanapelekea kutokuwapo kunyenyekea maana kiongozi atafanya linalowezekana ili maendeleo kwa wengi yapatikane.

Wakoloni walibeba nguvukazi na rasilimali nyingi toka Afrika. Walifanya hivyo ili wasonge mbele ipasavyo leo "tukakopi" na "kupesti" kutoka kwao bila kujiuliza walifanyaje hadi kufikia hapo walipo?

Historia inaonyesha mataifa yaliyoendelea miaka 150 mpaka 200 iliyopita watu wake waliumia na wengine kupoteza maisha katika harakati za kujiletea maendeleo waliyonayo sasa.

> Maeneo kama Dar es Salaam utasikia eti wazee hawatakiwi kuwa mijini, tunaambiwa makazi yao ni Chalinze au Msata.

Waliojikweza walifanya hivyo bila kunyenyekea lakini baada ya kupata maendeleo unyenyekevu, demokrasia na utandawazi vikafuata. Hali kama hiyo hata sisi hatutaikwepa iwapo tunahitaji maendeleo ya kweli, maana baadhi yetu tutaumia lakini tujipe moyo wajukuu na vitukuu wetu watafaidi matunda ya jasho letu.

Tumwombe Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima na busara ikiwezekana tunu na miiko ya taifa virejeshwe kwa faida ya wote na amani yetu idumu.

Huu ni wakati wa kushikamana kikamilifu na kusonga mbele mpaka kieleweke kuwa Tanzania ni namba moja Afrika.

***Mwandishi anapatikana kupitia, P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania.***
***fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050;***

## Rais Putin: Nchi za Magharibi zinalaghai mataifa ya Afrika!

RAIS wa Urusi, Vladmir Putin, amesema nchi yake inaweza kuisaidia Afrika bila masharti ambayo huambatanishwa kwenye misaada ya mataifa ya Magharibi.

"Tunaona jinsi mataifa ya Magharibi yanavyotoa shinikizo na vitisho dhidi ya serikali huru za Kiafrika, wanatumia njia hizo ili kurejesha nguvu ya ushawishi na utawala kwenye makoloni yao ya zamani na kulinyonya Bara la Afrika," anasema Rais Putin katika mahojiano na Shirika la habari la Urusi TASS, kabla ya mkutano na viongozi wa Afrika.

Urusi inatarajia kuwa mwenyeji wa viongozi 47 wa Afrika katika mkutano wa siku mbili Oktoba 23 hadi 24 unaofanyika mjini Sochi.

Rais Putin amesema uhusiano na Afrika umeimarika, akiainisha makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya silaha, ambapo Urusi imefanikiwa kushawishi mataifa zaidi ya 30 kusambaza silaha zake.

Rwanda ni moja ya nchi ambazo zimekuwa na uhusiano mzuri na Urusi.

Baraza la Mawaziri la Rwanda hivi karibuni liliridhia makubaliano na Urusi katika masuala ya matumizi ya nishati ya nyuklia maalumu kwa matumizi ya amani, limeripoti Gazeti la The East Africa.

Teknolojia hii itatumika katika uzalishaji wa nishati na utunzaji wa mazingira, ripoti inasema.



Rais Vladimir Putin wa Urusi. **PICHA: MTANDAO**

### USHAWISHI WA NCHI ZA MAGHARIBI KWA AFRIKA

Marekani imekuwa ikipoteza ushawishi barani Afrika, lakini mwanadiplomasia wa juu wa nchi hiyo kwa Bara la Afrika, anataka kubadili hali hiyo.

Rais Donald Trump alishawahi kuripotiwa kuyataja mataifa ya Kiafrika kuwa ni 'nchi chafu' na kuongelea Afrika kama sehemu ambayo marafiki zake wanakwenda kujaribu kutajirika.

"Kwa muda mrefu wakati wawekezaji walipokuwa wakibisha milango na Waafrika wakifungua, mtu pekee aliyekuwa hapo ni Mchina," Tibor Nagy, mjumbe wa masuala ya Afrika wa Marekani, aliiambia BBC.

Biashara ya China na Bara la Afrika imeifunika Amerika katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, na mwaka 2018 ilikuwa kubwa mara tatu zaidi.

Marekani imekuwa chanzo kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja barani Afrika, lakini mchango wake umekuwa ukipungua.

Mwaka 2018, China ilitangaza uwekezaji wa thamani ya dola za kimarekani bilioni 60 kwa ajili ya miradi ya miundombinu.

Ben Abdallah anasema kuwa biashara kati ya Marekani na mataifa ya Afrika imeshuka kwa sababu ya ongezeko la uhitaji si tu China, lakini nchi nyingine kama vile Urusi na Uturuki.

"Nafikiri ni kwa sababu ushindani kutoka kwa nchi nyingine umeongezeka katika kipindi cha muongo mmoja uliopita," anasema.

Ukuaji wa uchumi wa China umeonyesha dalili za kushuka hivi karibuni, hali ambayo itaathiri biashara na uwekezaji katika Afrika siku za usoni.

Lakini kutokana na ushindani kutoka duniani kote wa kufanya biashara na nchi za Kiafrika, Marekani inapambana kurejesha uhusiano na bara hilo kwa kujihusisha na nchi za uchumi unaochipukia. **BBC**

# Rushwa yakwamisha wanawake Zanzibar kuwania nafasi za uongozi



Wananchi Zanzibar wakipiga kura kwenye uchaguzi wa mwaka 2015. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

INAPOFIKIA kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, wanawake wengi hujitokeza kugombea nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi kupitia vyama vyao vya siasa.

Hata hivyo, wengi wao hushindwa kupata nafasi hizo kutokana na jamii kutawaliwa na rushwa.

Kutokana na uwezo mdogo wa kipato walionao wanawake, rushwa imekuwa ni kikwazo kwao kupata nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi.

Ili kuwa kiongozi kupitia jimbo lazima kwanza uteuliwe na chama cha siasa kuwa mgombea na wananchi wakupigie kura ndipo uwe mbunge, mwakilishi au diwani kwa upande wa kata/shahia kwa Zanzibar.

## MGOMBEA

Khuzaima Bakari ni mwanamke ambaye alishagombea nafasi ya uwakilishi kwa vipindi vitatu mfululizo kwenye chaguzi zilizopita lakini anasema amekosa nafasi hiyo kutokana na rushwa inavyotawala hasa katika kipindi cha uchaguzi.

"Rushwa inaanzia kwenye vyama vya siasa hadi katika jamii, maana wanawake tumekuwa tukidaiwa rushwa aidha ya fedha au ngono ili chama kiweze kukusimamisha kuwa mgombea na jamii iweze kukuchagua," anasema.

Anabainisha wanawake hawana uwezo wa kifedha, hivyo wanapojitokeza kugombea majimboni kuna mfumo umewekwa, kwamba ukitaka kupita katika kura za maoni, ni kutoa rushwa na wanawake hawana fedha za kutosha.

## WANANCHI MJINI NA VIJIJINI

Bahati Issa ni mkazi wa Kikungwi Kusini Unguja, anasema wanawake wanakosa nafasi za uongozi kutokana na rushwa na hivi sasa wamekuwa na hofu ya kugombea kwa sababu ya kushamiri kwa vitendo hivyo.

Anabainisha wapo wanawake wenye uwezo wa kuwa viongozi,

> Tunashindwa kusonga mbele katika harakati za kugombea si kama hatutaki...tunataka na tunapenda, lakini hatuna fedha na unapoenda kuomba nafasi na kulizwa kama una fedha, unaanza kuvunjika moyo.

lakini wanakosa nafasi kutokana na kudaiwa rushwa na kwa kuwa hawako tayari kuitoa, ndoto zao huishia hapo.

"Chaguzi zilizopita rushwa ilitawala, sasa tukiwa tunaelekea kwenye chaguzi zijazo, tunaviomba vyama vyote vya siasa na serikali kulisimamia hili, kwani sisi wanawake tuna hamu ya kugombea," anasema.

## TATU OTHMAN

Tatu Othman ambaye ni mkazi wa Magomeni, Mjini Unguja, ambaye ana ulemavu wa uoni anasema wanawake wanashindwa kugombea nafasi za uongozi kwa sababu hawana fedha.

"Tunashindwa kusonga mbele katika harakati za kugombea si kama hatutaki...tunataka na tunapenda, lakini hatuna fedha na unapoenda kuomba nafasi na kulizwa kama una fedha, unaanza kuvunjika moyo," anasema.

Kwa upande wake, Zaituni Bahorera, mkazi wa Kijiji cha Makunduchi, anasema kikwazo kikubwa cha wanawake kushindwa kugombea nafasi za uongozi ni rushwa kwani wapo wanawake wenye elimu nzuri ambao wakipewa nafasi wanaweza kuleta maendeleo, lakini rushwa ndiyo inawafanya washindwe kufikia ndoto zao katika uongozi.

"Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa) katika uchaguzi wa mwaka 2015, kilitoa elimu kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi, elimu ambayo ilitufikia hadi sisi vijijini, cha kushangaza ni wanawake watano tu ndio waliopata nafasi ya uwakilishi kupitia majimboni," anasema.

Anabainisha baada ya kutolewa elimu hiyo, wanawake zaidi ya 50 walijitokeza kugombea nafasi za uongozi kupitia vyama mbalimbali vya siasa, lakini ni wanawake watano tu kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ndio waliopata nafasi hizo.

## OMAR

Hassan Omar, Mkazi wa Kijiji cha Kizimkazi, anasema kuwa wapo wanawake wenye uwezo mzuri wa kuwa viongozi lakini wanakosa nafasi hizo kutokana na uwepo wa rushwa katika jamii.

"Asilimia kubwa ya watu wanaoingia katika uongozi hasa wanaume, wako kwa ajili ya maslahi yao binafsi na ndio maana, wanawake wanakosa nafasi za uongozi," anasema.

Kingine anachotaja kukosesha wanawake nafasi za uongozi ni kitendo cha wanaume walio wengi kupeana nafasi za uongozi ili maovu yao yasiweze kutambulika.

Anawaasa wanawake kutovunjika moyo, bali wapambane ili kutimiza ndoto zao za kuwa viongozi na kuiletea nchi maendeleo.

## TAMWA

Hawra Shamte, Meneja wa Sera na Utetezi kutoka TAMWA Zanzibar anaitaka jamii ifahamu kuwa rushwa ni adui wa haki na wanawake wana haki ya kugombea nafasi za uongozi.

Anasema wanawake kugombea nafasi za uongozi iwe urais, ubunge, uwakilishi au udiwani ni haki yao ya kikatiba na wala hawastahili kutoa rushwa.

Anaitaka jamii kuwapa fursa wanawake ya kugombea nafasi za uongozi na kuachana na masuala ya rushwa kwa sababu kiongozi anayetokana na rushwa hataweza kuwaletea maendeleo.

Aidha, anazishauri mamlaka za kuzuia rushwa kuweka mitego, kuwafuata wanasiasa kuzungumza nao kuhusiana na rushwa kwa sababu wengine wanaona ni jambo la kawaida kuombwa pesa, wakatoa. Aliitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa Zanzibar (ZAECA) kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na rushwa hasa wakati huu wa kuelekea chaguzi, kwani rushwa inaanzia ndani ya vyama katika vikao vya uteuzi wa wagombea.

## NAIBU SPIKA

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, anasema ni kweli kilio kikubwa cha wanawake katika kugombea nafasi ya uongozi ni rushwa ya fedha na ngono.

Anabainisha ni lazima wanawake kupaza sauti kukemea rushwa kuanzia ndani ya vyama vya siasa hadi katika jamii, kwani zimekuwa zikiwarudisha nyuma.

Mgeni anasema, wanawake si kwamba wanataka uongozi kwa kujionyesha bali kuna mambo wanataka kuyasema na kuyasimamia.

"Tumekaa kimya muda mrefu na mambo mengi tumekosa...tunafahamu nyumba nyingi maskini zinazoendeshwa na wanawake... sisi ndio tunaotupiwa watoto, tunaoingia leba...sasa nani ataiambia serikali kwamba tunataka hospitali zenye huduma bora, vifaa ili kupunguza vifo vya mama na watoto?" Anahoji na kuongeza:

"Hayo yote hayataweza kupatikana kama wanawake hatutapaza sauti zetu na kama hatutogombea nafasi za uongozi."

## ZAECA

Kwa upande wake Makame Khamis Hassan ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi na Operesheni wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa Zanzibar (ZAECA), anasema matukio ya rushwa katika maandalizi ya uchaguzi yamekuwa yakitokea katika hali tofauti, hasa ikizingatiwa kuwa uchaguzi unapita katika hatua mbalimbali.

Anasema hatua ambayo ZAECA inapokea malalamiko mengi ya tuhuma za vitendo vya rushwa ni ya kampeni za wagombea ndani ya vyama. Anabainisha kuwa malalamiko ya tuhuma za vitendo vya rushwa waliyopokea katika uchaguzi wa mwaka 2015 pamoja na ule wa marudio wa mwaka 2016 yalihusisha wagombea wa kiume kutoka vyama mbalimbali vya siasa.

Kaimu mkurugenzi huyo aliitaka jamii kufahamu kuwa inapochagua kiongozi ambaye ametoa rushwa isitarajie manufaa au maendeleo kutoka kwake kwa sababu atataka fedha alizowapa anazirejesha.

Anasema kuelekea katika uchaguzi mkuu mwakani, ZAECA imejiandaa kuhakikisha vitendo vya rushwa vinapungua na viongozi wanaingia madarakani kihalali.

## MSEMAJI MKUU WA SMZ

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, anasema vitendo vinavyoambatana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi, kamwe haviwezi kuvumilika mahali popote pale iwe ndani na hata katika uga wa kimataifa.

Anabainisha wapo baadhi ya watendaji na watumishi wa umma wasio waaminifu wanaendelea kuhujumu uchumi kwa kupokea rushwa na kuisababishia serikali hasara au wananchi wake kuweka katika mazingira magumu pale wanapohitaji huduma za kijamii.

Balozi Iddi anasema zipo tuhuma za uhujumu uchumi na upokeaji rushwa zipatazo 108, ambapo upelelezi wake haujakamilika zilizoripotiwa katika ZAECA kufikia mwaka 2018.

Anazitaka taasisi zinazohusika na ufuatiliaji wa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kisheria kuondoa muhali na kuharakisha upelelezi wake ili wahusika wafikishwe katika vyombo vya sheria ili haki ichukuwe mkondo wake.

# Kimiti amwona JPM kama Nyerere

Na Joseph Mwendapole



Mzee Paul Kimiti. **PICHA: MTANDAO**

OKTOBA 14 mwaka huu, Watanzania waliadhimisha kumbukumbu ya miaka 20 tangu kutokea kifo cha mwasisi wa taifa hili, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyefariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, kule London nchini Uingereza.

Mwalimu Nyerere, licha ya kustaafu urais mwaka 1985 na kufariki miaka 20 iliyopita, bado ameendelea kuishi katika mioyo ya Watanzania, wakikumbuka juu ya uzalendo wake, ubinadamu wake na hasa kwa kujitolea na kuipenda nchi yake kwa dhati ya moyo wake.

Ndiyo maana, kila mwaka, kila kona ya nchi, wananchi wa makundi mbalimbali, wakiwamo wasomi, wanasiasa, watafiti na wadau wa mambo mbalimbali, wamekuwa wakiendesha semina, makongamano, mijadala na tafiti mbalimbali zinazomhusu mwasisi huyo wa taifa.

Mwaka huu, ukiwa ni wa nne tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli, makongamano, midahalo na semina mbalimbali zimekuwa zikiendelea kuhusu kumbukizi hii muhimu ambayo ilifikia kilele chake juzi Jumatatu, tarehe ambayo kwa heshima yake, imepewa hadhi ya kuwa siku ya mapumziko kwa Watanzania wote.

Mwandishi wa makala haya, alimtafuta mwanasiasa mkongwe, ambaye alipata kufanya kazi kwa karibu na Mwalimu Nyerere, Paul Pater Kimiti na kufanya naye mazungumzo juu ya mambo mbalimbali kuelekea kumbukizi hii na hasa akichambua ndoto za mwalimu na utendaji kazi wa Rais John Magufuli.

Mzee Kimiti, ambaye enzi za Mwalimu alikuwa mwalimu wa siasa katika Makao Makuu ya chama, Mkuu wa Mikoa kadhaa na baadaye waziri, anazungumzia jinsi ambavyo ndoto ya kujitegemea ya Mwalimu Nyerere, inavyoshughulikiwa kwa kasi na weledi na Rais Magufuli.

"Sisi ambao tulifanya kazi kwa karibu na Mwalimu wakati wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, tunafahamu nini hasa ilikuwa ndoto yake. Mwalimu aliamini kwamba siyo jambo jepesi kwa nchi changa kama Tanzania wakati huo, kuweza kuamua kufuata aina moja ya siasa ikiwa tegemezi, ndiyo maana akaanzisha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, akiamini kuwa kama taifa litajitegemea, kwa mahitaji yake yote muhimu, ni rahisi kuamua aina ya siasa ya kuifuata," anasema na kuongeza:

"Ndiyo maana Mwalimu alipenda sana taifa lijitegemee, lisiwe ombaomba kwa sababu siku zote ukiwa ombaomba huwezi kuwa huru... ni lazima utafuata matakwa ya anayekupa kile unachokiomba. Angalia, katika wakati ambao taifa lilikuwa limejitoa kuzisaidia nchi zingine za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara zipate uhuru wake, lakini bado aliweza kujenga viwanda vya mazao mbalimbali karibu kila mkoa, nia yake kuu ikiwa ni kujitegemea."

Mwanasiasa huyu mwandamizi anabainisha kuwa kwakuiangalia kwa umakini dhana hii, japo Mwalimu alishindwa kuitimiza wakati wa uongozi wake, lakini ni wazi kuwa Rais John Magufuli anaelekea kuitimiza.

> Leo hii kodi inayokusanywa, mapato yanayopatikana kupitia rasilimali zetu mbalimbali, zinaonekana kwa sababu kila mmoja ni shahidi wa namna ambavyo taifa letu linasonga mbele.

Anasema, hiyo ni kwa namna anavyofanya kila njia kuhakikisha kuwa taifa linajikomboa kutoka utegemezi wa mataifa ya nje na kujijengea uwezo wa kuweza kufanya mambo yake yenyewe.

Mzee Kimiti ambaye ndiye aliyesimamia shughuli zote za mazishi ya Mwalimu Nyerere, yaliyofanyika kijijini kwake, Butiama mkoani Mara, anasema anamtazama Rais Magufuli kama kiongozi ambaye ameamua kwa makusudi kuhakikisha taifa linajitegemea kupitia rasilimali zake.

"Mambo anayoyafanya hivi sasa yasingewezekana kwa kutegemea fedha za misaada...siku zote watu wanaotukopesha hawapendi tujitegemee, wanatupa msaada wa leo ili kesho turudi tena kuwaomba na hivyo kuendelea kuwa tegemezi.

"Chukulia mfano ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere kule Rufiji, mradi huu ukikamilika, taifa litakuwa limepiga hatua kubwa sana kuelekea kujitegemea, kwa sababu viwanda vyetu vitakuwa na uhakika wa umeme kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali," anasema na kuongeza:

"Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ya kutumia umeme, maana yake taifa litaweza kusafirisha abiria na bidhaa kwa wingi ndani ya muda mfupi, na hivyo kuharakisha maendeleo ya taifa kwa watu kuwa huru kupeleka bidhaa kokote wanakotaka kwa wakati."

Mzee Kimiti anasema wahisani siku zote wanataka kuabudiwakwa kila jambo.

"Angalia jinsi serikali ya awamu ya tano inavyofanya jitihada za kujenga vituo vya afya, hospitali kubwa na vifaa tiba nchi nzima, hii inaondoa hofu ya kuwa na taifa ambalo haliwezi kuwapa tiba raia wake na hivyo kutegemea huduma hizo kutoka nje," anasema.

Anabainisha kuwa jambo la kufurahisha sana ni kuwa vitu vyote hivi vinafanyika kwa kutumia fedha zetu za ndani, kama ambavyo Mwalimu Nyerere alidhamiria.

Anafafanua kuwa Rais Magufuli amedhibiti mianya yote ya rasilimali za nchi kuchotwana watu wachache kwa faida yao.

"Leo hii kodi inayokusanywa, mapato yanayopatikana kupitia rasilimali zetu mbalimbali, zinaonekana kwa sababu kila mmoja ni shahidi wa namna ambavyo taifa letu linasonga mbele," anasema na kuongeza:

"Mwalimu alijua tunao uwezo mkubwa wa kujitegemea, ndiyo maana wakati wake hakuruhusu madini kuchimbwa, kwa sababu aliamini wananchi wake bado hawajaelimika, akatoa fursa ya wanafunzi wote kusoma bure kwa gharama za serikali kuanzia darasa la kwanza hadi Chuo Kikuu."

Anasema lengo lake lilikuwa ni kuzalisha wasomi ambao kwa elimu yao, wataweza kusimamia rasilimali za nchi kwa faida ya wananchi wote, kitu ambacho kinaonekana kwa Rais Magufuli hivi sasa.

Mzee Kimiti anabainisha, ujenzi wa reli, bwawa la umeme, hospitali na vituo vya afya vinavyoendelea kujengwa sehemu mbalimbali, vitaifanya Tanzania kuwa taifa la mfano miaka michache ijayo, kwani maana halisi ya maendeleo, ni namna ambavyo wananchi wananufaika na huduma zinazotolewa.

"Matajiri wote duniani hawafanyi kazi kwa ajili ya fedha bali wanafanya fedha ifanye kazi kwa ajili yao," anasema na kuongeza:

"Maana ya msemo huu ni kwamba ili tuweze kujua thamani ya fedha zetu, ni lazima fedha hizi ziwasaidie wananchi kupata kwa uhakika na kwa wakati kwa huduma zote muhimu ikiwemo elimu, afya na nyinginezo."

Mwanasiasa huyu mwandamizi anaongeza kuwa huo ndio msingi wa Ilani za Chama Cha Mapinduzi, kama mwongozo wa 1971, Ibara ya 28 inavyotamka kwamba:

"Kitendo chochote kinachompa mtu uwezo wa kuamua maisha yake na kutawala maisha yake, ni kitendo cha maendeleo, hata kama hakimwongezei afya wala shibe, lakini ni kitendo anachoamua mwenyewe."

Mzee Kimiti anaongeza "Sera ambazo Mwalimu Nyerere alizikazania sana ilikuwa tija, ajira, mishahara na bei za bidhaa. Katika bei, aliamini kwenye ujamaa wa kweli, bei za vitu ni lazima zifanane, zisiwe na tofauti kubwa na hii ndiyo ilipelekea kuanzishwa kwa kampuni za biashara za mikoa maarufu kama RTC."

Mzee Kimiti anasema Mwalimu vilevile hakutaka uwepo wa tofauti kubwa katika mishahara ya watumishi wa umma.

"Hii ni kwa sababu kungekuwa na unyonge miongoni mwa wananchi... kama utaona, Rais Magufuli amepunguza sana mishahara ya watumishi kwa sababu mtu mmoja hawezi kulipwa milioni 40 kwa mwezi wakati mwingine anapata laki tatu," anasema na kuongeza:

"Utaona pia dhana ya Mwalimu ya uanzishwaji wa viwanda, ilenga kutoa ajira kwa Watanzania kwa sababu ndizo huchukua watu wengi, kitu ambacho Rais Magufuli anakifanya hivi sasa akihimiza ujenzi wa viwanda kila anapokwenda, akiamini taifa linakwenda katika uchumi wa kati na viwanda."

Kwa sasa Kimiti ni Mwenyekiti wa Umoja wa wafuasi wa Mwalimu Julius Nyerere, ukihusisha wanasiasa mbalimbali waliopata kufanya kazi kwa ukaribu na mwasisi huyo wa taifa.

# Hali tete licha ya Marekani kuepusha vita ya Uturuki, Syria



Rais Recep Tayyip Erdo an wa Uturuki (kushoto) akiwa na Rais wa Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

MLIPUKO mpya umeepushwa Mashariki ya Kati baada ya Marekani na Uturuki kufikia makubaliano kuruhusu kusimamishwa mapigano Kaskazini ya Syria ambako majeshi ya Uturuki yameingia na kuteka maeneo mapana ndani ya ukanda wa kilomita 20.

Ilikuwa nusura wakutane na vikosi vya jeshi la Syria vilivyotumwa kutwaa maeneo hayo ambayo yalikuwa yanalindwa na kikosi cha Marekani kikishirikiana na wapiganaji wa ki-Kurdi, pale Marekani ilipoamua kuondoa kikosi hicho.

Rais Donald Trump alisita kusema waziwazi kuwa alimruhusu Rais Recep Tayyip Erdogan kuliteka eneo hilo, ila alionekana hajali.

Makundi takriban yote ya kisiasa nchini Marekani yalipinga hatua hiyo, kwani wa-Kurdi wanathaminiwa na wachambuzi na wanaharakati Marekani kwa kutoa msaada mkubwa katika mapambano na kundi la Islamic State (IS) lililotokea maeneo makubwa ya Iraq na Syria kuanzia 2013 hadi 2015.

Rais Trump alisisitiza kuwa alifanya kampeni mwaka 2016 na kushinda kwa ahadi ya kuondoa wapiganaji wa Marekani katika maeneo mengi yenye vita vya jadi ambavyo havina tija kwa maslahi ya Marekani.

Alisema makundi yanayopambana Mashariki ya Kati, hasa ya kidhehebu, yanawakilisha chuki na vita vya miaka 1000.

Uturuki ilivamia Syria Kaskazini kuendeleza mpango wake wa kuwa na eneo salama la kurudi wakimbizi ambao wengi zaidi ni

> Rais Donald Trump alisita kusema waziwazi kuwa alimruhusu Rais Recep Tayyip Erdogan kuliteka eneo hilo, ila alionekana hajali.

Wakurdi, lakini nchini Marekani na kwingineko walikuwa wanataka eneo hilo liwe chini ya ulinzi wa Marekani ikishirikiana na Wakurdi.

Marekani ilipoamua kuondoa kikosi chake ikawa kuna ombwe la mamlaka eneo hilo, Uturuki ikaingia kuhakikisha kuwa chama cha wapiganaji wa ki-Kurdi hakitawali eneo hilo kana kwamba ni mwanzo wa kuwa na taifa huru, au liwe kitovu cha kueneza vita ya ukombozi ya Wakurdi katika nchi za Iraq, Iran na hasa Uturuki. Nchini Iran wa-Kurdi ni dhaifu.

Kilichokuwa kinaleta wasiwasi ni kuwa Uturuki ilikuwa imepania kuwafyeka wa-Kurdi na isingezuiliwa na chochote endapo Marekani isingechukua hatua za kuiwekea vikwazo vya uchumi kama haitakubali kuacha mapigano.

Rais Erdogan kwanza akatoa ishara kuwa hatakutana na ujumbe wa Marekani ukiongozwa na Makamu wa Rais Mike Pence, 'labda aje Trump mwenyewe ndiyo nitazungumza naye.'

Trump hakwenda, akamtuma Pence na Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompe, wakajadiliana kwa muda wa saa tano ndiyo wakatia saini hati ya makubaliano kusitisha mapigano. Ila tafsiri zake ni tofauti kiasi.

Bado hakuna maelezo ya kina nini kiwango cha kuhusika kwa kila mmoja kati ya pande tatu zilizoko eneo hilo, yaani Uturuki, Syria na Wakurdi, kwani Syria haiwezi kuwanyang'anya Wakurdi kushika eneo hilo, na inachotaka Uturuki ni kuwa wapiganaji wa ki-Kurdi wasiwe huru kuendesha shughuli zao huko, kwani inapingana na maslahi ya Uturuki.

Chama cha PKK cha Wakurdi wa Uturuki kinaaminika ni cha kiharakati zaidi ya chama cha Syrian Democratic Forces (YPG kwa lugha za huko) kilichoshirikiana na Marekani dhidi ya Islamic State na sasa Marekani imekiacha solemba. Suala hilo liliudhi wanaharakati.

Akizungumzia uamuzi wake wa kuondoa kikosi cha jeshi la Marekani Kaskazini ya Syria, Rais Trump alisema ni mkakati hodari (strategically brilliant), yaani 'amewala chenga' maadui zake walioko wengi tu maeneo hayo.

Alisema Marekani imetumia zaidi ya dola trilioni moja tangu mzozo huo uanze na kuanza kupeleka vikosi vya Marekani eneo hilo wakati Marekani haina rafiki hapo. Kwa kiasi fulani aliona Uturuki inakaribia kuwa rafiki wa Marekani kama mshirika katika NATO na itawalinda vyema wa-Kurdi.

Mpangilio huo wa hoja ulipingwa kwa nguvu hata kati ya wanaomuunga mkono Trump kwa dhati ndani ya chama tawala Republican, kwani ni kutofautisha kati ya wapiganaji na raia.

Ni kana kwamba Uturuki inaweza kuwalinda raia wa Syria wa asili ya ki-Kurdi wanaokaa eneo hilo au walio katika makambi ya wakimbizi upande wa Uturuki, na huku inawafyeka wapiganaji wao.

Hata baada ya kufikiwa kwa ilani ya kuacha mapigano hali ilikuwa bado tete vile Russia haiwezi kuchukua nafasi ya Marekani iwatenganishe.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki alianza mapema kukana kuwa imefikiwa hatua ya kusimamisha mapigano na katika muda mfupi wakaendelea kutupiana lawama ya kutupa risasi kinyume cha ilani ya kuacha mapigano.

Hatua ya kuwa na eneo salama kwa ajili ya wakimbizi wanaokisiwa kuwa kiasi cha 300,000 walioko Uturuki inakubaliwa na nchi za Magharibi na za eneo hilo kwa jumla, na imekuwa ndiyo chembe muhimu ya majadiliano kati ya Russia, Uturuki na Iran kuhusu hali ya baadaye ya Syria.

Kwa mpangilio wa hoja za Trump, ingebidi Russia ichangie kulinda eneo hilo na nchi zilizobaki, ili Marekani isitumie fedha nyingi katika kutuliza migogoro ya watu wengine, ambao kwa sehemu kubwa ni adui zake.

Kwa upande mmoja ni nguvu za wanaharakati wa Marekani na hata ndani ya chama cha Republican ambako Seneta Lindsay Graham alimcharura Trump kwa undani na taarifa zake zilikuwa chachu kwa wanaharakati na vyombo vya habari kwa jumla kumlazimisha aingilie kati kwa njia nyingine.

Trump alikuwa amepuuza moja kwa moja tatizo la uvamizi wa Uturuki Kaskazini ya Syria akisema 'siyo mpaka wetu' na kuhusu kuwaacha washirika dhidi ya ISIS wateketee, akasema 'wapiganaji wa ki-Kurdi siyo malaika.'

Alielezea jinsi ISIS wanavyoiheshimu PKK, wapiganaji wa ki-Kurdi nchini Uturuki, na kuwa tatizo ni moja ya masuala ya jadi ya Mashariki ya Kati, hivyo Marekani isihangaike kulinda wasipigane.

Nje ya juhudi za Seneta Graham na wengine, hali mpya ilikuwa inazuka eneo la Mashariki ya Kati kwa uwezekano wa vita vya pande tatu ambavyo kwa jumla vingeinufaisha Marekani na Israel, kwa kuweka Iran na Uturuki katika kuangamiza sehemu isiyo ndogo ya uwezo wa kijeshi kupambana nchini Syria.

Utawala wa Rais Assad pia ungedhoofika na siyo ajabu Iran ingebidi kuitisha vikosi vya wapiganaji wa ziada kwa mfano Hezbollah nchini Lebanon kusaidia vita nchini Syria, dhidi ya Uturuki.

Pia nafasi ya Russia kama taifa kubwa eneo hilo ingepwaya kwani ina uwezo amani ikiwepo, vinginevyo Marekani inahitajiwa isimamishe mapigano angalau kwa vikwazo vya uchumi, hatua ambayo Russia haina uwezo.

Kwa upande mwingine, licha ya kiburi chake kujifanya anazungumza na ujumbe wa ngazi za juu wa Marekani kwa kujilazimisha tu, Rais Erdogan itabidi awashukuru wanaharakati wa Marekani kupaza sauti na kumlazimisha Rais Trump kurudi kinyumenyume kwa njia tofauti.

Bila hivyo kulikuwa na uwezo wa wa-Kurdi kuwafungulia kwa wingi wapiganaji wa ISIS waliotekwa ili waingie vitani na Uturuki kwa upande wa hao wa-Kurdi kama mshirika kwa vita hiyo, licha ya kuwa nchini Uturuki jeshi kama taasisi lina mapenzi makubwa na ISIS, kama ilivyo nchini Saudia, licha ya kuwa ISIS haitaki nchi hizo ziwe na ushirikiano na Marekani.

Kuna uwezekano Rais Erdogan awe hatarini kudidimizwa na wapenda ISIS katika Jeshi la Uturuki, ambao amekuwa akipambana nao kwa nguvu tangu mwaka 2017.



# RPC Mbeya atatua kero mtaa kwa mtaa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KAMANDA wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, ameanzisha utaratibu wa kuwatembelea wananchi kwenye kata zao kwa ajili ya kusikiliza kero zinazohusiana na jeshi hilo.

Matei alianza utekelezaji wa utaratibu wiki iliyopita kwa kutembelea kata za Jiji la Mbeya na kufanya mikutano ya hadhara na wananchi akiwa ameongozana na maofisa wengine wa jeshi hilo wakiwamo wakuu wa vitengo.

Baadhi ya vitengo ambavyo Matei anaongozana na wakuu wake ni pamoja na dawati la jinsia, kitengo cha makosa ya mtandaoni na maofisa wa upelelezi ambao wanawaelimisha wananchi mambo mbalimbali wanayohusika nayo.

Akizungumza na wananchi wa kata za Nzovwe, Kalobe na Itende kwa nyakati tofauti, Kamanda Matei alisema lengo la ziara zake hizo ni kuwasikiliza wananchi ili kujua changamoto zilizopo ndani ya jeshi hilo.

"Ninyi wananchi ndio mnaoishi na wahalifu kwenye makazi yenu na pia ndio waathirika wakubwa wa uhalifu, hivyo ni lazima tuwape elimu ili iwe rahisi kushirikiana kudhibiti wahalifu na kuufanya mkoa wetu kuwa na amani," alisema.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi James Chacha, aliwatahadharisha wananchi wa Jiji la Mbeya kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi kwa madai kuwa vitendo hivyo vinasababisha chuki miongoni mwa wanajamii.

Alisema endapo mtu yeyote atakamatwa mtaani kwa kosa lolote anatakiwa kufikishwa kwenye vyombo vya dola ili achukuliwe hatua za kisheria badala ya wananchi kuchukua hatua za kumpiga na kuua.

"Mtoto wa jirani anakamatwa halafu mnachukua mafuta mnamchoma badala ya kumfikisha polisi, vitendo hivyo vinasababisha uhasama, chombo pekee chenye mamlaka ya kutoa hukumu ni mahakama na hata sisi polisi hatuwezi," alisema Chacha.

Naye Mkuu wa Dawati la Jinsia, Butusyo Mwambela, aliwataka wazazi na walezi kuwa walinzi wa watoto wao ili kuepuka kukumbwa na vitendo viovu wanapokuwa kwenye maeneo hatarishi.

**"Mtoto wa jirani anakamatwa halafu mnachukua mafuta mnamchoma badala ya kumfikisha polisi, vitendo hivyo vinasababisha uhasama, chombo pekee chenye mamlaka ya kutoa hukumu ni mahakama na hata sisi polisi hatuwezi," alisema Chacha.**

# Walimu wamwagiwa zawadi kwa ufaulu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKURUGENZI wa Shule za St. Marcus za jijini Mbeya, Philipo Mulugo, amewazawadia walimu wa shule hizo kama motisha kutokana na kuwawezesha wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne.

Mulugo alitoa zawadi hizo juzi ambazo ni pesa taslimu na pikipiki huku akiahidi kutoa zawadi ya gari kwa walimu wawili ambao watawawezesha wanafunzi kufanya vizuri mwakani kwenye mitihani ya kitaifa.

Kiongozi huyo ambaye amewahi kuwa Naibu Waziri wa Elimu, alisema kazi ya walimu ni ngumu na wanatakiwa kutiwa moyo, hivyo aliamua kutoa zawadi hizo kama sehemu ya kuwatia moyo kwa kazi hiyo.

Alisema kutokana na mchango wa walimu hao, shule hiyo ilishika nafasi ya tatu katika Mkoa wa Mbeya na ya kwanza kwa Jiji la Mbeya katika matokeo ya darasa la saba ambayo yalitangazwa hivi karibuni na ilishika nafasi ya tatu kwenye matokeo ya mtihani wa majaribio wa kidato cha nne.

Mulugo ambaye ni Mbunge wa Songwe, alisema walimu waliopata zawadi ni wale waliowawezesha wanafunzi kufaulu kwa alama za 'A' na 'B' nyingi kwenye masomo wanayofundisha.

"Niliahidi mwaka jana kuwa nitatoa zawadi kwa watakaofanya vizuri na leo (juzi) ndio natimiza ahadi yangu. Niliahidi kuwapa hundi ya Sh. 500,000 kila mmoja lakini nimeamua nawapa pesa taslimu na wawili waliofanya ambao hata mwaka jana walifanya vizuri nawakabidhi pikipiki mpya," alisema Mulugo.

Baadhi ya walimu waliopata zawadi hizo, walimshukuru Mulugo kwa zawadi alizowapatia huku wakidai kuwa zitawaongezea hamasa ya kufundisha ili wafanye vizuri zaidi miaka inayofuata.

Mmoja wa walimu hao, Manase Daudi, ambaye anafundisha somo la Hesabu darasa la saba, alisema zawadi hiyo ya pikipiki aliyoipata itamsaidia kufika kwa wakati shuleni na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Alisema darasa la saba waliomaliza Septemba, mwaka huu, walikuwa 33 na 28 kati yao walifaulu Hisabati kwa kupata alama 'A' na watano pekee ndio walipata 'B'.

Alisema lengo lake ni kuhakikisha mwakani anawawezesha wanafunzi wote kufaulu kwa kupata alama 'A' ili kuendelea kujizolea zawadi kutoka kwa mkurugenzi wake huyo.

"Mwaka uliopita niliongoza na nilipata zawadi. Mwaka huu nimefanya vizuri pia ndiyo maana mkurugenzi amenipa zawadi hii lakini naahidi kuwa Mungu akitupa uzima mwakani nitapata zawadi ya gari," alisema Manase.

Naye Mwalimu wa Taaluma Sekondari, Renatus Mnyonga, ambaye pia alizawadiwa pikipiki, alisema zawadi hiyo ni changamoto kwake na kwa walimu wengine wa shule hiyo.

Alisema kwa sasa wana lengo la kuiwezesha shule kuingia kwenye orosha ya shule 10 bora kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa mwakani ili kuing'arisha shule hiyo na kuendelea kuzoa zawadi.

Aliwataka walimu wengine ambao hawakupata zawadi kuendelea kujibidiisha ili mwakani nao wapate huku akisisitiza kuwa matokeo mazuri ni sifa kwa shule na mkoa wa Mbeya.



Dereva wa gari la kubeba takataka akiwa ameliegesha vibaya na kuziba nusu ya barabara eneo la Bustani ya Jiji, jijini Mbeya jana, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria za usalama barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wasimamizi elimu wafundwa uongozi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WASIMAMIZI wa elimu kuanzia ngazi ya wilaya wametakiwa kuhakikisha walimu wakuu na wakuu wa shule nchini wanakuwa na nyaraka muhimu za miongozo ya usimamizi wa taasisi hizo ili waziendeshe kwa ufanisi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Elimu (Adem), Dk. Siston Mgullah, alisema hayo juzi wakati wa kufunga mafunzo ya usimamizi wa elimu kwa wakuu wa shule na walimu wakuu kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema endapo viongozi hao watakuwa na nyaraka hizo itakuwa rahisi kuziendesha taasisi hizo kwa kufuata sera, sheria na kanuni za uendeshaji wa taasisi nchini.

Pia alisema endapo wasimamizi hao watakuwa na nyaraka hizo muhimu itakuwa rahisi kujua mahitaji ya taifa kielimu ikiwamo uzalishaji wa wataalamu wa kuendesha uchumi wa viwanda.

"Moja kati ya nyaraka muhimu ya kuwa nayo ni Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo pia inaeleza mambo mbalimbali yanayohusu elimu na tukumbuke kuwa serikali iliyoko madarakani ni ya CCM," alisema Dk. Mgullah.

Alisema nyaraka zingine ambazo wanatakiwa kuwa nazo ni miongozo ya namna ya uendeshaji wa elimu, Katiba ya nchi pamoja na nyaraka zingine muhimu.

Meneja Mafunzo wa Adem, Lucas Mzelela, alisema ili kuendesha vizuri taasisi za elimu ni muhimu walimu wakuu na wakuu wa shule washirikiane na kamati na bodi za shule kwenye uendeshaji.

Alisema endapo pande hizo mbili zisipokuwa na uelewano kuna uwezekano mkubwa wakavuruga uendeshaji wa shule na kuifanya taaluma ianze kuporomoka.

Mzelela alisema mafunzo hayo yalikuwa yanawahusisha walimu kutoka shule za serikali na za binafsi ili kuwakumbusha baadhi ya misingi ya usimamizi wa elimu kwenye maeneo yao.

Alisisitiza kuwa mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa kushirikisha pia kamati na bodi za shule ili wawe na ajenda moja na wakuu wa shule na walimu wakuu.





## Vijana waonyeshwa fursa za kiuchumi

**Na Augusta Njoji, CHAMWINO**

VIJANA 212 wa Wilaya ya Chamwino wamehamasishwa kuchangamkia fursa zilizopo kwenye maeneo yao zikiwamo mikopo (fedha za mitaji), kilimo na ufugaji.

Wanachagizwa kuchangamka kutokana na mwitikio mdogo wa kuchangamkia fursa uliopo miongoni mwa vijana ikiwamo kuchukua mikopo inayotolewa na halmashauri.

Hayo yalielezwa jana na Mratibu wa Mradi wa kuwawezesha vijana kukamata fursa za kiuchumi wilayani humo, Emmanuel James, katika mafunzo ya ukamataji fursa.

Aliwaambia mradi huo unalenga kuwawezesha vijana kukamata fursa zilizopo kwenye maeneo yao na kuanzisha shughuli rafiki za kiuchumi ili kuboresha maisha yao.

"Pia kuwaunganisha vijana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kupata masoko ya bidhaa zao, tunalenga vijana wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 18-35," alisema James.

Kadhalika, alisema mradi unatekelezwa katika kata nne za wilaya hiyo na Mtandao wa Mazingira Dodoma (DONET) kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Serikali la The Foundation for Civil Society(FCS).

James alisema mradi huo unagharimu Sh. milioni 40 na utatekelezwa hadi Februari 2020.

"Pamoja na vijana 212 kuhamasishwa pia tumewezesha uundwaji wa vikundi saba vya vijana kwenye vijiji hivyo ili kuchangamkia fursa ikiwamo mikopo inayotolewa na halmashauri wajikwamue kiuchumi," alisema James.

Aliongeza: "Tumewaunganisha vijana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama taasisi za kifedha, kilimo, ufugaji na vyombo vya habari. Vijana waongeze ufahamu na ari ya kuthubutu kufanya kazi kwa namna yoyote yenye tija kwao," alisema.

Mratibu huyo alisema wamejipanga kuendesha elimu kwa njia ya vyombo vya habari kuhusiana na uwepo wa fursa za vijana zilizopo kwenye maeneo yao.

Aidha, watatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanufaika wote wa mradi yatakayoendeshwa na Shirika la Viwanda Vidogo (Sido).

"Pia tutaunda majukwaa ya vijana ili kuongeza uhamasishaji wa vijana wengine, kuwawezesha vijana wajasiriamali kushiriki maonyesho ya wiki ya Azaki kitaifa kwa lengo la kuongeza maarifa, ubunifu na stadi katika shughuli zao za ujasiriamali," James alisema.

# UDSM kutoa mitihani ya Kiswahili kimataifa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinatarajia kuanza kutoa mitihani ya kimataifa ya ujuzi wa lugha ya Kiswahili kwa watahiniwa mbalimbali duniani, kuanzia Januari mwakani.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Leonard Akwilapo, alipokuwa akizungumza na wanahabari kuhusu mitihani hiyo.

Alisema hatua hiyo ni jitihada za kuikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili duniani kwa kuwa ni miongoni mwa lugha 10 zenye wazungumzaji wengi duniani.

"Mtakumbuka kwamba Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alishafanya jitihada kubwa sana na za kukiendeleza na kukieneza Kiswahili pamoja na kusimamia ubora wake ndani na nje ya nchi. Lakini Marais waliofuatia katika awamu zote za uongozi wa nchi yetu pia walitilia sana mkazo suala hili," alisema.

Vile vile, Katibu Mkuu alisema mitihani itafanyika mara sita kwa mwaka ikiendana na kipindi cha masomo ya Kiswahili kwa kila ngazi na itafanyika kwa njia za kielektroniki katika vyuo na vituo mbalimbali vya Kiswahili duniani ambavyo tayari kuna makubaliano maalumu kuhusu mitihani hiyo.

"CKD au UDSM kinakuwa ni chuo kikuu cha kwanza duniani kutunga mitihani hii na kusimamia utahini na usahihishaji wake na kutoa cheti cha kimataifa kinachoonyesha kiwango cha ujuzi wa mtahiniwa," alisema.

Aliwaambia wanahabari kuwa chuo hicho kimechukua jukumu la kuanzisha mitihani ya Kimataifa ya Ujuzi wa Lugha ya Kiswahili sanifu ili lugha ya kimataifa ipate nguvu zaidi hutungiwa mitihani ili wanaojifunza waweze kutathminiwa na kupata vyeti.

"Ni ukweli ulio wazi kuwa CKD kina uzoefu wa kutosha na umahiri katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na vyuo vikuu vingi duniani vimekuwa vikipata uzoefu huo kutoka CKD," alisema.

Alibainisha kuwa tayari kuna makubaliano baina ya walimu wa Kiswahili wa CKD na walimu wanaofundisha Kiswahili katika vyuo vya nje kuhusiana na mitihani hiyo ambayo itaanza kutolewa mwakani.

"CKD kimejiandaa kuhakikisha kuwa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano iko madhubuti kuwezesha mitihani hii kufanyika kwa ufanisi na kwa viwango vya kimataifa kwani kuna wahitaji ambao watafanyia mitihani hii wakiwa katika nchi zao, sio lazima wasafiri na kuja kufanyia mitihani yao hao Tanzania," alisema.

Alibainisha walengwa wa mitihani hiyo ni watu wote ambao wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili au lugha ngeni katika ngazi mbalimbali ikilenga kupima usanifu katika kusoma, kuandika, kuongea na kusikiliza. Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, (Tataki) Prof. Aldin Kai Mutembei, alisema mitihani hiyo itaitwa kwa jina la Mkuki.

"Kuna wanafunzi wengi wanasoma Kiswahili huko nje na walitamani kuja kwenye nchi zinazozungumza Kiswahili lakini wangependa wawe na utambulisho kuwa wanajua Kiswahili hawa ndio tunaowalenga," alisema.



Baadhi ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tawi la Njedengwa, jijini Dodoma, wakiwa nje ya ofisi ya tawi hilo, ambalo halikufanya uchaguzi wa kura za maoni kwa ajili ya wagombea wa uchaguzi wa serikali za mitaa, juzi, kwa madai ya kuenguliwa kwa baadhi ya majina ya wagombea. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Agizo la RC lavuruga kura ya makao makuu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KIKAO cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kimevunjika baada ya wajumbe kutokubaliana na pendekezo la Mkuu wa Mkoa kutaka, Bukuru kuwa makao makuu ya wilaya hiyo.

Walisambaratika juzi wakati wa kikao hicho kilichokuwa kinalenga kuridhia mapendekezo yaliyokuwapo kuhusu makao makuu ya wilaya.

Akizungumzia na Nipashe, mmoja wa madiwani jina (linahifadhiwa), alisema sababu ya madiwani kukataa makao makuu ya wilaya kuwa Bukuru ni kutokana na eneo hilo kuwa nyuma, halijachangamka na halina watu wengi ikilinganishwa na Kijiji cha Pai.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gasper Mwenda, alikiri kuvunjika kwa kikao hicho na kwamba kulitokana na pendekezo lililopokelewa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, likiagiza makao makuu kuwa Bukuru.

"Ilipofika muda wa kupiga kura kati ya Bukuru na Pai ambayo ni maeneo yaliyokuwa yamependekezwa, ilitoka kauli kutoka kwa Mkurugenzi kwamba Mkuu wa Mkoa ameagiza makao makuu yaende Bukuru kwa hiyo kazi ya baraza ikawa imesitishwa," alisema.

Alieleza kuwa kutokana na hali hiyo kikao kilivunjika kwa sababu madiwani hawakukubaliana na pendekezo hilo wakati wao walikuwa katika hatua ya upigaji kura kufanya maamuzi.

"Baada ya kuvunjika tunatafakari hatua inayofuata kama umefuatilia tangazo la waziri zimebaki siku chache za kufanya uamuzi, tunaendelea kutafakari," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema Mkuu wa Mkoa aliagiza makao makuu ya wilaya yaende Bukuru wakati wao wapo kwenye upigaji kura.

"Mapendekezo hayo yaliyoletwa hayakuzingatia umuhimu wa kikao hicho na kusababisha mkutano kuvunjika kwa kuwa madiwani ndiyo walipaswa kutoa maamuzi kuhusu hilo," alisema.

Alifafanua kuwa kanuni za halmashauri zinaelekeza inapofika hatua kura za maoni katika kikao hakuna habari ya agizo fulani.

"Kutekeleza agizo ni kwenda kinyume na kanuni zinazotuongoza ambazo zinahitaji kura zipigwe, kwenye kifungu cha 28(1) cha Kanuni za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, kura ipigwe ili kufanya maamuzi," alisema Mwenda.



# Balozi Iddi aeleza umuhimu uzazi mpango

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema kila mtoto duniani ana haki ya kuishi, kuhudumiwa, kupata elimu pamoja na uhuru kama binadamu.

Amesema mtoto atazipata haki hizo kama jamii iliyomzunguka itaendelea kuzingatia uzazi wa mpango.

Alisema masuala ya uzazi wa mpango pia yanakubalika kwenye dini na ndio maana madhehebu tofauti yanaelekeza familia kumnyonyesha mtoto kuanzia siku moja hadi miaka miwili ili kukamilisha haki yake ya kupata virutubisho kutoka kwa mama.

Balozi Seif Ali Iddi alitoa kauli hiyo ofisini kwake wakati wa mazungumzo yake na ujumbe wa viongozi waandamizi wa Chuo Kikuu cha Al - Azhar cha Misri ulioongozwa na Sheikh Saleh Abbas Goma, ambaye ni Katibu wa Saleh Grand ya Imam wa chuo hicho.

Ujumbe huo upo Tanzania kwa mwaliko wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) chini ya Mwakilishi Mkaazi wake, Jacqueline Mahon.

Balozi Iddi alisema familia zinapaswa kuendeshwa kwa kutumia mfumo uliokubalika ndani ya vitabu vya dini ambavyo vimeshatoa mwelekeo wa malezi ya familia yanayokubalika hata kwenye mfumo wa kisasa wa kujali kukitunza kizazi.

"Uzazi wa mpangilio umekubalika katika dini ya Kiislamu na ndio ikasisitizwa mtoto anyonyeshwe miaka miwili ili kutoa muda kwa mwingine kupata haki yake ya msingi," alisema Balozi Iddi.

Aliushukuru uongozi wa UNFPA kwa jitihada zake za kuiunga mkono Tanzania na Zanzibar katika masuala ya malezi ya watoto katika familia nyingi nchini.

Awali Kiongozi wa Ujumbe huo wa Viongozi Waandamizi wa Chuo Kikuu cha Al - Azhar cha Misri, Sheikh Saleh Abbas Goma, alisema uislamu muda wote unazingatia na kusisitiza uwapo wa jamii yenye afya na nguvu.

Sheikh Goma alisema maandiko matukufu ya Quran yanampa muumini aliyeamini kitabu hicho mwongozo wa maisha yake ya kawaida yanayompa fursa ya kuishi kwa upendo na Taqwa.

Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA, Mahon, alisema masuala ya idadi ya watu na namna ya maisha yao yameshazungumzwa na kuandikwa katika vitabu mbalimbali.

Mahon alisema UNFPA kupitia wataalamu wake itaendelea kubeba jukumu la kutoa taaluma kwa taasisi na mbalimbali ulimwenguni ili kuona uwapo wa idadi ya watu duniani inakwenda sambamba na ukuaji wa uchumi.



Ng'ombe wakichungiwa kwenye eneo la Shule ya Msingi Kawe B, jijini Dar es Salaam juzi. Mkuu wa shule hiyo, Venance Mwasamakwela, alisema kukosekana kwa uzio kumesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Elimu madeni sugu yatakiwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WANANCHI wametakiwa kuitumia ipaswavyo elimu ya kukabiliana na madeni sugu ili kutatua changamoto katika jamii.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya kudai madeni sugu yalioshindakana (IRA), Issa Haji Khamis huko Marumbi Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kutokana na kuongezeka kwa tatizo hilo na uwelewa mdogo, aliwataka wananchi kuhakikisha wanashirikiana na kampuni hiyo ili kutatua tatizo hilo.

Alisema kuwa wamebaini kuwa kuna watu wengi waliodhulumiwa na wameshindwa kutambuwa wapi wanatakiwa kupeleka malalamiko yao ili kusaidiwa na kupata haki.

"Sisi IRA tukishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeamua kuanzisha ofisi ambayo itasaidia jamii madeni yote sugu yalishindikana," alisema.

Alisema matarajio yao ni kuona wananchi wanajitokeza katika ofisi zao kuripoti matatizo yao kwa kuwa lengo ni kusaidia na kuondoa tatizo hilo.

Omar Sheha Omar, mwanasheria wa kampuni hiyo, alisema wanashughulikia madeni yote sugu ambayo yameshindikana, ikiwamo nyumba, fedha, mashamba na madeni mengine na kwamba kinachozingatiwa ni ushahidi ambao utakuwa wa karatasi.

Kwa upande wake mratibu wa kampuni hiyo, Haidar Yahya Issa, alisema mategemeo yao ni kujitokeza kwa wananchi wengi ambao watakuwa tayari kutoa ushirikiano ili kusaidiwa kupatiwa haki zao kwa mujibu wa sheria.

Seif Omar akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake, aliwataka viongozi hao kuamini kuwa elimu hiyo imewapa mwamko na wako tayari kutoa ushirikiano juu ya hilo ili kupata haki zao kwa mujibu wa sheria.

# Ujenzi jengo Mahakama Kuu wanukia

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAHAKAMA Kuu ya Zanzibar imetiliana saini na kampuni ya Adent Construction Limited juu ya ujenzi wa jengo jipya la mahakama hiyo maeneo ya Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

Serikali ya Zanzibar iliwasilishwa na Mtendaji wa Mahakama Kuu, Kai Bashiri Mbaraka wakati Advent Construction Limited iliwashilishwa na Mkurugenzi wake, Druv Jog, ambapo shughuli hiyo ilifanyika katika Mahakama Kuu eneo la Vuga.

Baada ya utiwaji wa saini, Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Mwali, alisema kujengwa kwa jengo hilo ni moja ya mafanikio mkubwa kwa Mahakama ya Zanzibar kwa kuwa jengo la sasa ni la zamani na ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi.

Alisema kuwa katika kufikia malengo ya watendaji wa Mahakama Kuu, ni lazima wawe na majengo yenye nafasi na ubora wenye viwango ili kwenda na wakati uliyopo na watumishi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Amesema mahakama imekuwa ikifanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na kutoa haki kwa wananchi wote bila ya kuwabagua, hivyo ni vyema jengo lake kuwa na nafasi kubwa ili kutoa huduma zake kwa wananchi wanaofika hapo.

Hata hivyo, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na wigo mpana wa kujenga majengo ya kisasa hasa ofisi za serikali nje ya miji kwa kuwa inafahamu kuwa miji inakua kila uchao.

Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alisema kukamilika kwa jengo hilo kunazidisha ari ya kiutendaji kwa kuwa hivi sasa kuna ufinyu wa nafasi katika sehemu za kufanyia kazi.

Hata huivyo, alisema katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki, ni lazima sehemu ya kufanyia kazi iwe ya kisasa na watendaji kuwa wenye sifa katika taaluma yao, hivyo kukamilika kwa jengo hilo kutatoa fursa ya mahakimu zaidi kuongezwa katika mahakama.



# Agizo la JPM latekelezwa

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

KAZI ya usanifu wa ujenzi wa chujio la maji kwenye chanzo cha maji katika mradi wa Mbwinji unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi, Masasi-Nachingwea (MANAWASA) umekamilika kwa asilimia 100.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Devid Mwansojo, kuwa kazi hiyo imeshatekelezwa na kukamilika kama Rais John Magufuli alivyoagiza kuwa itekelezwe ndani ya wiki mbili na sio miezi sita.

Alisema sasa Wizara ya Maji iko mbioni kutuma timu maalumu kwa ajili ya kuanza kukamilisha kazi hiyo.

Mwansojo alisema utekelezaji huo unatokana na agizo la Rais Magufuli alilolitoa hivi karibu alipotembelea wilayani Masasi akitokea wilayani Nachingwea.

Alisema kwa muda mrefu mradi huo umekuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa chujio kwenye chanzo cha maji.

Mwasonjo alisema kutokana na changamoto hiyo, maji yanayozalishwa hasa kwa kipindi cha masika yanakuwa na rangi ya tope, hivyo kulazimika kusitisha huduma kwa muda kadhaa.

"Kwa mujibu wa taarifa nilizoletewa na wizara, kazi ya usanifu wa ujenzi wa chujio la maji imeshakamilika na muda wowote kuanzia sasa timu ya wizara itakuja kuanza ujenzi huu," alisema Mwansojo.

Alisema kukamilika kwa usanifu huo ni suluhisho la changamoto hiyo, kwa kuwa ujenzi ukianza na utakapokamilika adha ya wananchi kupata maji yenye rangi ya tope haitakuwapo tena.

# Wanaodanganya kutolipwa fidia ya ardhi waonywa

**Na Said Hamdani, LINDI**

WILAYA ya Lindi, imewaonya wakazi wa maeneo ya Zahanati na Mitwero Kata ya Rasbura, wanaotoa madai ya uongo kuwa hawajalipwa fidia ya ardhi iliyotwaliwa na taasisi ya Wama Foundation kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya wasichana.

Onyo hilo, limetolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga, kwamba taasisi hiyo iliomba eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo, hivyo, halmashauri iliwashauri wananchi wa maeneo husika kukubali kuondoka na taasisi iliwalipa fidia.

Taasisi ya Wama inayomilikiwa na Salma Kikwete, mke wa Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, iliomba eneo hilo kwa ajili ya kuwasaidia kielimu wasichana waliomaliza elimu ya msingi kutoka familia maskini.

Alisema kutokana na eneo alilopewa kuwa dogo, taasisi iliomba kuongezewa na kukubaliwa.

Mkuu huyo wa wilaya, alisema amepokea jumla ya malalamiko 102 kutoka kwa wananchi wa Mitwero Zahanati, wakidai kutolipwa fidia kwa eneo lao la ardhi waliyoitoa.

Alisema malalamiko aliyopokea kutoka kwa wananchi hao yapo katika sura mbili tofauti, likiwamo la kudai riba kutokana na kucheleweshewa kulipwa tangu uthamini hadi tarehe ambayo walilipwa kupita kipindi kirefu, lakini kuna eneo lingine la wakazi 17 wanaodai hawajalipwa kabisa na halina uhusiano na eneo lililoongezwa taasisi hiyo.

Ndemanga akasema mgogoro huo ni wa muda mrefu na kwamba yeye ameukuta alipohamishiwa wilaya hiyo akitokea Mwanga miaka miwili iliyopita na kuwa katika kushughulikia mgogoro huo yapo mambo ameyabaini na anataka mgogoro uishie shambani.

Pia alisema alichobaini ni uwepo wa idadi kubwa ya watu wanaodai hawajalipwa, tofauti na taarifa ya maandishi aliyonayo ofisini kwake, ambayo inaonekana watu wote walilipwa, hivyo kuibuka kundi lingine likidai limesahaulika.

Alifafanua kuwa katika hali ya kawaida inaleta mshangao kwamba ni wataalamu wa aina gani wa serikali ambao wanakwenda kutambua wananchi mahali wanapofanyiwa uthamini halafu wanawasahau 17 ambao ni wengi.

Ndemanga amesema ili kuumaliza mgogoro huo, anawataka wale wote wanaodai hawajalipwa wafike kwenye eneo linalolalamikiwa Novemba Mosi mwaka huu, ili kuumaliza mgogoro huo wakiwa na vielelezo vyao.

Pia alisema watahusishwa mtendaji wa kata, mtaa, Wama, wataalamu wa Manispaa wakiwa na nyaraka zao zikionyesha mambo yote yaliyofanyika.

Aliwaonya watakaobainika kujichomeka kwenye mgogoro bila kuhusika, kuwa watashughulikiwa.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kawe B, wakifurahia na wafadhili wao kutoka Shirika la Time To Help la Uholanzi shuleni hapo, jijini Dar es Salaam juzi. Shirika hilo, limekarabati madarasa matatu yaliyokuwa yamechakaa na ofisi ya mwalimu mkuu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Bodi ya Barabara yaazimia ukarabati barabara za mkoa

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

BODI ya Barabara mkoani Kagera, imeazimia kutatua kero za wananchi juu ya miundombinu mibovu ya barabara.

Kutokana na hali hiyo, bodi imetaka ukarabati wa barabara za wilaya zote za mkoa huo.

Maazmio hayo yalitolewa katika kikao cha bodi kilichoshirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa kujadili kero zinazowakwamisha wananchi.

Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliyabainisha hayo wakati wa kuhitimisha kikao hicho kwa kutoa mapendekezo sita.

Gaguti alisema kuna baadhi ya maeneo katika mkoa huo yana barabara korofi ikiwamo Mtaa wa Kyebitembe katika Manispaa ya Bukoba.

Alisema eneo la Kyebitembe lenye barabara ya kilomita 10 ambapo uhitaji ni wa haraka, hivyo iongezwe kasi katika ukarabati pamoja na nyingine.

"Uhitaji wa miundombinu ni wa haraka kwa wananchi, hasa barabara zilizo katika mpango ukichukulia uhitaji wa mtaa wa Kyebitembe ambapo kuna uharaka wa kuongeza kasi," alisema Gaguti.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mkoani Kagera, Mhandisi Andrew Kasamwa, alisema, kwa mwaka wa fedha 2019/20, serikali imetenga Sh. bilioni 13.7.

Kasamwa alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 2.7 zitatumika kulipa maboresho ya mwaka uliopita na kiasi cha Sh. bilioni 10.9 zitatumika mwaka huu.

Aidha, alisema kuwa mbali na bajeti hiyo zipo fedha ambazo ni za maendeleo Sh. bilioni 4.9, Sh. bilioni 3.4 zimetoka serikalini na Sh. bilioni 1.4 zimetoka mfuko wa barabara na kuwa kila mwaka lazima kuna matengenezo.

Naye Mbunge Jasson Rweikiza, alisema kuna haja ya kuzingatiwa kwa bajeti hiyo na barabara za Halmashauri ya Bukoba kuwekwa lami.

## HABARI KIMATAIFA

# Tembo 55 wafa kwa kukosa maji ya kunywa

**HARARE,** Zimbabwe

TEMBO 55 wamekufa njaa katika mbuga ya kitaifa ya Hwange, nchini Zimbabwe kutokana na ukame mkali uliokithiri kwa zaidi ya miezi miwili.

Taarifa iliyotolewa na msemaji wa mbuga hiyo, Tinashe Farawo ilieleza kuwa tembo hao walikutwa wamefariki kutokana na kukosa maji kulikosababishwa na ukame mkali.

**Hali ni mbaya, tembo wanakufa kutokana na ukame na hili ni tatizo kubwa.**

"Hali ni mbaya, tembo wanakufa kutokana na ukame na hili ni tatizo kubwa," alisema Farawo.

Alieleza kuwa ukame umepunguza kwa kiwango kikubwa idadi ya mimea nchini Zimbabwe.

Theluthi moja ya watu nchini humo wameripotiwa kukabiliwa na uhaba wa chakula wakati mgogoro wa kiuchumi ukiendelea nchini humo.

Agosti, mwaka huu Ripoti ya Shirika la Chakula Duniani (FAO) ilieleza kuwa watu milioni mbili wako katika hatari ya kukabiliwa na baa la njaa nchini Zimbabwe. Baadhi ya tembo walipatikana katika eneo la mita 50 (yadi) ya maji, kuashiria kuwa walitembea mwendo mrefu bila maji na hatimaye kufa muda mfupi kabla ya kuyafikia.

Farawo alisema tembo hao wamesababisha uharibifu mkubwa wa mimea katika mbuga ya Hwange.

Mbuga hiyo inawahifadhi tembo wapatao 15,000 lakini kwa sasa kuna zaidi ya tembo 50,000.

Farawo alieleza kuwa mbuga ya Hwange ambayo haijawahi kupokea ufadhili kutoka kwa serikali, imekuwa ikijaribiu kuchimba visima lakini inakabiliwa na changamoto ya fedha ya kuendelea na mradi huo.

Mizoga ya tembo hao ilipatikana katika mashimo ya maji yaliyokauka. **BBC**



Vikosi vya ulinzi vya Ujerumani vikiwa nchini Syria. **PICHA: REUTERS**

## Waziri, mkewe kuhukumiwa miaka miwili jela

**PARIS,** Ufaransa

MAHAKAMA ya jinai ya Nanterre nchini Ufaransa imemhukumu waziri wa zamani wa Burundi, Gabriel Mpozagara na mkewe, Candide kifungo cha miaka miwili jela na faini ya Euro 70.000 kwa kosa la kumtumia mfanyakazi wa ndani kwa kipindi cha miaka kumi nyumbani kwao.

Waziri huyo ambaye aliwahi kuongoza Wizara ya Haki na Uchumi nchini Burundi na mkewe wamekutwa na hatia ya kumpa kazi kwa kulazimisha, mfanyakazi huyo, na kumweka katika mazingira yasiyokuwa ya heshima.

Methode Sindayigaya, mkulima wa zamani wa Burundi mwenye umri wa miaka 39, aliiambia mahakama jinsi alivyokuwa mtumwa kwa muda wa miaka 10 nyumbani kwa wanandoa hao. Wawili hao wanashtumiwa kwa usafirishaji haramu wa binadamu.

Ofisi ya mashtaka jijini Nanterre inawashtumu wawili hao kwa kosa la kumnyanyasa raia huyo wa Burundi kwa miaka 10 kwenye makazi yao, magharibi mwa Jiji la Paris.



Methode Sindayigaya ambaye alifanyiwa madhila hayo, aliingia nchini Ufaransa akiambatana na mwanawe, huku akibaini kwamba alijaribu kuwaambia wanandoa hao kuwa alipoteza pasipoti yake. Awali Gabriel Mpozagara na mkewe walisema kuwa hawakutaka kumwachilia akazurura ovyo mitaani.

"Alikuwa kama mtoto wa nyumbani, rafiki ambaye wakati mwingine alisaidia na kazi za nyumbani. Alitaka kubaki katika makazi yangu, alisema Mpozagara.

Wakati akijitetea mahakamani, Sindayigaya aliieleza mahakama namna alivyotumiwa kuhudumia watoto kwa miezi mitatu. Miaka 10 alikuwa akifanya kazi kwa muda wa saa 19 kati ya 24, kulishwa vibaya na malazi duni. **RFI**

# Netanyahu ashindwa kuunda serikali

**YERUSALEM,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu ametangaza kushindwa kuunda serikali yenye wingi wa kutosha bungeni, hatua inayoashiria kikwazo kikubwa dhidi ya kiongozi huyo anayekabiliwa na matatizo mengi.

Kwenye taarifa yake, Netanyahu alieleza kuwa pamoja na kufanya kazi bila kuchoka ili kufanikisha uundwaji wa serikali hiyo ya mseto pamoja na mpinzani wake, Benny Gantz lakini hajafanikiwa.

Wakati leo ndio siku ya mwisho ya kukamilisha mchakato huo, Netanyahu alisema anarejesha mamlaka kwa Rais Reuven Rivlin ambaye atalazimika sasa kumwomba Gantz kujaribu kuunda serikali.

"Kila jitihada nilizofanya za kuunda serikali ya kitaifa na kuzuia uchaguzi mwingine hazikufanikiwa. Amekataa tu. Ninasikitika kwamba kukataa kwake kunaonyesha jambo moja tu kwamba anaendelea kuwa mateka wa Avigdor Lieberman," alisema Netanyahu na kuongeza:



"Anaendeshwa na masuala ya nje yanayohusiana na mambo yake ya kibinafsi ya Yair Lapid ambaye anafaidika na kushindwa kwake. Gantz, Lapid na Lieberman wanazungumza tu kuhusu umoja, lakini wanatekeleza kinyume kabisa," alisema Netanyahu.

Netanyahu ambaye ametimiza miaka 70 jana, hilo ni pigo kubwa kwake.

Kwenye uchaguzi wa Aprili, Netanyahu pia alishindwa kulishawishi bunge na kulazimika kuitisha uchaguzi mwingine uliofanyika Septemba 17.

Hivi sasa, ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipochaguliwa mapema mwaka 2009, taifa hilo linakabiliwa na uwezekano wa kuchagua kiongozi mwingine.

Hata hivyo, Gantz pia atakabiliwa na kizingiti kigumu, kwa kuwa bila ya chama cha Likud cha Netanyahu hataweza kupata wingi wa viti bungeni.

Kwenye taarifa fupi iliyotolewa na chama chake cha Bluu na Samawati alisema: "Sasa ni wakati wa kuchukua hatua. Chama hicho kimesema kimedhamiria kuunda serikali ya umoja ya iliyoongozwa na Benny Gantz, ambayo watu wa Israel waliichagua miezi michache iliyopita."

Gantz aliapa kuliunganisha tena taifa hilo baada ya utawala wa muda mrefu wa Netanyahu, ambao alisema umezidisha mgawanyiko wa kidini na kisiasa, lakini pia madai ya ufisadi yanayomkabili kiongozi huyo.

Wakati Mwanasheria Mkuu wa Israel naye akijiandaa kutoa maamuzi katika wiki chache zijazo kuhusu kumfungulia mashtaka ya mlolongo wa madai hayo ya ufisadi, Waziri Mkuu huyo huenda akakabiliwa na wakati mgumu zaidi kutokana na shinikizo la kumtaka ajiuzulu.

Kwenye uchaguzi mkuu wa mwezi uliopita, Netanyahu alishindwa kupata wingi wa viti bungeni. Lakini Rais Rivlin alimpa nafasi ya kwanza ya kuunda serikali kwa kuwa alikuwa na uungwaji mkono wa wabunge 55, kuliko Gantz aliyekuwa akiungwa mkono na wabunge 54. **DW**

# Mtaka ataka elimu ya sheria shuleni

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amesema ipo haja somo la sheria kuingizwa katika mitaala ya elimu kwenye shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha wanafunzi kuwa mabalozi wazuri katika kuelimisha jamii juu ya masuala ya kisheria.

Mtaka ameeleza hayo jana katika mahojiano na Nipashe, na kusema kuwa mabaraza ya ardhi ngazi ya kijiji, kata na wilaya hayana elimu juu ya masuala ya kisheria, hali inayosababisha ongezeko la mashauri na migogoro mingi ya ardhi.

Alisema Wizara ya Katiba na Sheria ione umuhimu wa kuingiza somo la sheria katika somo la uraia ili kuwajengea uelewa wa kutosha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili pindi wanapohitimu elimu yao, wakawe mabalozi wazuri wa kuielimisha jamii juu ya masuala ya sheria na namna ya kutatua masuala yahusuyo sheria.

"Ni vema Wizara ya Katiba na Sheria ikaliingiza somo la sheria kwenye somo la uraia, naamini litasaidia sana kwani mabaraza ya kijiji, kata na wilaya hawana kabisa elimu ya sheria na ndio maana malalamiko mengi na mashauri ya wananchi yanaongezeka," alisema Mtaka.

Costantine Kapagala, mkazi wa kijiji cha Ngulyati, alisema kumekuwapo na changamoto kubwa kwa viongozi na mabaraza ya ardhi ngazi za chini kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kile kinachodaiwa rushwa.

Kapagala alisema wajumbe wengi wa mabaraza ya ardhi wamekuwa wakilalamikiwa kupokea rushwa wakati wa kusikiliza mashauri yao na kusababisha migogoro mingi na uhasama baina ya walalamikaji na walalamikiwa.

Naye Mathias Gelald, mkazi wa Wilaya ya Bariadi, alisema kesi nyingi na mashauri mengi yanashindwa kufikia maamuzi sahihi kutokana na ukosefu wa elimu kwa wananchi pamoja na mabaraza ya ardhi.

Alisema ukosefu huo wa elimu ndio chanzo kikubwa cha watu kutoelewa maamuzi na hukuku za mashauri yao huku wakikimbilia suala la uwapo wa rushwa.

"Naamini kuwa endapo elimu hiyo ya masuala ya sheria ingekuwa inawafikia wananchi wote...hata kusingekuwa na ongezeko la mashauri yasikofikia muafaka...ni vema sana wizara husika kupitia wasaidizi wa kisheria wakasaidia kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya masuala ya kisheria.

Ezekiel Kasanga, Mkurugenzi wa Shirika la Kasodefu linaloshughulika na masuala ya utoaji wa msaada wa kisheria, alisema wasaidizi wa kisheria wamekuwa wakijitahidi sana kutoa elimu juu ya usaidizi wa kisheria, ila tatizo lipo katika mabaraza.

Alisema mabaraza mengi hayana uelewa kabisa wa masuala ya kisheria, hali inayopelekea kushindwa kufanya maamuzi ya haki katika mashauri wanayopelekewa.

Naye msajili wa watoa huduma wa msaada wa kisheria, Felister Mushi, alisema kuwa lengo la wiki ya maadhimisho ya msaada wa kisheria ni kukuza ufahamu na uelewa kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kuwafikia mawakili na kupata huduma za kisheria.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanywa (kulia), akipata maelezo ya huduma za Bank of Africa katika kuwezesha wananchi kutoka kwa Naibu Mkurugenzi wa benki hiyo, Wasia Mushi, alipotembelea ofisi yake mjini Mtwara jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## TADB, PASS kuwezesha ajira kwa vijana

**Na Enock Charles**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na sekta binafsi ya kuwezesha kilimo (PASS), zimeingia makubaliano ya kuwekeza katika miradi ya ubunifu ya kilimo kwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35 ili kuchangia ukuaji wa uchumi na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini, Japhet Justine, alisema lengo la makubaliano ni kukuza sekta ya kilimo nchini pamoja na kuwawezesha vijana, wanawake na wajasiriamali wadogo kupatikana kwa utoshelevu na usalama wa chakula nchini.

"Ili kuweza kumgusa mkulima mmoja mmoja wa chini na makundi mbalimbali yanayochangia katika Pato la Taifa na hasa katika sekta ya kilimo ikiwamo vijana wanawake na wajasiriamali wadogo ni vizuri kuingia makubaliano na kushirikiana na taasisi zenye malengo sawa," alisema Justine.

Alisema kwa kushirikiana na sekta binafsi ya kuwezesha kilimo (PASS) wamewezesha kuanzishwa kwa vituo atamizi kwa ajili ya kuwawezesha vijana, wanawake na wajasiriamali wadogo kwa kutoa huduma za kifedha kukuza miradi yao, kuyapa thamani mazao ya kilimo kwa kupitia mikopo na kuwakutanisha wawekezaji wakubwa katika sekta ya kilimo na vijana.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa PASS, Nikodemas Bohay, alisema tangu kuanzishwa kwake sekta hiyo, imeshaanzisha vituo atamizi vitatu na inatarajia kuanzisha vituo vingine vitatu kabla ya mwaka ujao kwa ajili ya kuwajumuisha vijana katika kilimo kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kitengo chake cha ubunifu yaani Kituo cha Ubunifu katika Biashara ya Kilimo (AIC), kinakusudia kuanzisha vituo vingi zaidi vya kuwasaidia vijana kwa kuzingatia kanuni za kilimo salama na shughuli hizo hufanywa kwa kuzingatia mazingira bora, matumizi kidogo ya nishati na nguvu kazi na njia endelevu za uzalishaji na usindikaji.

# Waziri ashangaa wamiliki wa ardhi kukataa kutambuliwa

**Na Munir Shemweta,** WANMM HAI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kaskazini kuwatambua wamiliki 2,019 wa maeneo katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambao hawataki kumilikishwa maeneo yao na kupatiwa hati.

Agizo hilo alilitoa jana baada ya kuelezwa na Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri hiyo, Jacob Muumba, kuwa pamoja na halmashauri hiyo kupima viwanja 2,019 wamiliki wake hawajajitokeza kumilikishwa jambo lililomshtua.

"Watu wana maeneo, lakini hawataki kumilikishwa, wanakwepa kitu gani maana hawalipi kodi," alisema Dk. Mabula.

Pia aliagiza wale wote wenye maeneo yaliyopimwa katika Wilaya ya Hai kutambuliwa na kujulikana wanamiliki maeneo yao toka muda gani na kusisitiza kuwa hakuna atakayeachwa na zitaangaliwa hatua za kuchukua.

Katika hatua nyingine, Dk. Mabula aliagiza kufuatiliwa kwa maeneo yote ya biashara ya hamashauri ya wilaya ya Hai ambayo hayalipiwi kodi ya pango la ardhi ili yalipiwe.

Alisema pamoja na halmashauri hiyo kuwa na maeneo ya kibiashara yaliyopimwa kama vile stendi na soko, hakuna hata eneo moja lililolipiwa kodi ya pango, hivyo mkurugenzi mtendaji wa halmashauri lazima ahakikishe analipia maeneo yake ya biashara.

"DED wa Hai hujawahi kulipia kodi ya pango la ardhi ya stendi na soko wakati maeneo haya yamepimwa. Kama halamashauri hailipi je, mtu wa kawaida itakuwaje?" Alihoji.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliagiza kupatiwa taarifa ya maandishi kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai kushindwa kulipia kodi ya pango la ardhi katika maeneo yake ya biashara.

Pia alimwahidi Naibu Waziri Mabula kuwa atalifanyia kazi suala hilo ndani ya muda mfupi pamoja na lile la wamiliki wa maeneo wasiotaka kumilikishwa.

Hata hivyo, Ole Sabaya alimweleza Dk. Mabula kuwa pamoja na changamoto mbalimbali katika sekta ya ardhi wilayani humo, ofisi yake kwa kushirikiana na idara ya ardhi, imezipatia ufumbuzi kero za ardhi za wananchi wa wilaya hiyo zipatazo 350 kati ya 432 zilizowasilishwa wakati wa siku maalum ya ardhi, maarufu kama Ardhi Day.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA VYETI



**MODESTER N. NDELWA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0289.0062.2012** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari SOLACE GIRLS, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.4193 kilichoctolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari HARRISON UWATA GIRLS.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: KW/RB/1782019**

215470002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: CHAMWINO (W) MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi No. 67/2019
Ombi la HASSANI SAIDI MANGACHI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu RAMADHANI SAIDI MANGACHI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 30/10/2019.


kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 11/10/2019

115471302

---

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP




**JACKLINE DAUD NONGA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba S.3822/0061 iliyotolewa na THE CATHOLIC DIOCESE OF SAME MOTHER TERESA OF CALCUTA GIRLS' SEKONDARY mwaka 2018.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/396559/2019.**

115472902

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON MARWA MALIMA**
Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na cheti Cha kidato cha Nne chenye namba S.0989/0050 Kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia Shule ya sekondari KIBARA Mwaka 2016.

Kwa atakae kiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo Karibu kwa Kumb. **KBR/RB/464/2018.**

115473902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**MAHALI;........ MOROGORO**
**MAOMBI NA:...141....MWAKA 2019**
**SILIM AHMED SILIM..................MUOMBAJI**
**EDGER MPOGORO.......................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA EDGER MPOGORO.**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe....28...mwezi...11....mwaka.....2019.Saa 2:30 Asubuhi mbele ya mwenyekiti....M. Khasim. Hivyo una amriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na nakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe ...22....mwezi...10...mwaka...2019.

115473502

---

### HATI YA KIWANJA IMEPOTEA

**PELES AMULIKE MWAIPOPO** anatangaza kupotelewa na hati ya umiliki wa ardhi yenye namba **39847.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polis.
Taarifa ya polisi:
**DAR/URA/RB/393964/2019.**

115472302

---


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KENNEDY KENAN LYOVA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 773 BHE TOYOTA CARINA.** Chassisi **No. AT2116073024.** Engine namba **7AJD62516.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/OST/RB/397927/2019.**

115472402

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**HUMPHREY SANGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0853-0104** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007 katika Shule ya Sekondari Kizwite . yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DOD/DOD/RB/356034/2019**

115471402

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH JONAS MWASHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1626/0132** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika Shule ya Sekondari Mukidoma . yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/URA/RB/400992/2019**

115471502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;211/2019

Ombi la ELIETI ELIHAZINA FUE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JANETH ELIAS LEBOI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 21/10/2019

215471602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**MAHALI;........ MOROGORO**
**MAOMBI NA:...141....MWAKA 2019**
**SILIM AHMED SILIM..................MUOMBAJI**
**PETER SEMLANGWA................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA PETER SEMLANGWA.**


Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe....28...mwezi...11....mwaka.....2019.Saa 2:30 Asubuhi mbele ya mwenyekiti....M. Khasim. Hivyo una amriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na nakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe ...22....mwezi...10...mwaka...2019.

115473502

---

### KUPOTEA KWA VYETI



**GOODLUCK JOHANNES OYOLLA**
anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0558-0037 kilichotolewa na MWANGA SEKONDARI mwaka 2013.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MD/B.I/I/VOL XIX/54/2019.**

115472702

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TA NZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MA WA SILIAN O

Simu : +255 26 2324455
Fax: 255 26 2323233
Barua pepe : ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,

40470 Dodoma

**22/10/2019.**

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 23/10/2019 Kampuni ya Mussa holdings itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Kingori kuelekea Moshi. Gari lenye namba za usajili T277ALQ.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0

---

### KUPOTEA KWA KADI


**EMMANUEL GODLOVE SALINGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ- BOXER yenye namba ya usajili MC 786 BTQ iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/MBA/RB/280992/2019**

115471802

---

### KUPOTEA KWA VYETI



**EMMANUEL GODLOVE SALINGO**
anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1535-0061 kilichotolewa na NAWENGE SEKONDARI mwaka 2009. Cheti cha Chuo kilichotolewa na TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE mwaka 2011.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/MBA/RB/280948/2019.**

115471702

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# STERLING KUWEKA REKODI YA MSHAHARA ENGLAND



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imeripotiwa kwamba, ipo tayari kuhakikisha winga wake, Raheem Sterling anabakia Etihad kwa kumpa mshahara mnono, kwa mujibu wa ESPN.

Taarifa kutoka ndani ya City ni kwamba, klabu hiyo imepanga kumwongeza mshahara Sterling hadi kufikia pauni 450,000 kwa wiki ili kumzuia asiondoke.

Awali kulikuwa na ripoti kwamba, Klabu ya Real Madrid ya Hispania ipo kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England na nyota wa zamani wa Liverpool.

Sterling alisaini mkataba mpya na City hivi karibuni tu, Novemba mwaka jana, dili ambalo linamfanya kupokea mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

Lakini kocha Zinedine Zidane ameripotiwa kuongeza presha katika harakati za kutaka kumsajili winga huyo ili akaimarishe kikosi cha Real Madrid kinachoyumba huko kwenye La Liga.

Hata hivyo, City hawako tayari kuona jambo hilo linatokea na wanataka kufanya kila linalowezekanalo kuhakikisha nyota wao huyo anabaki pale kwenye dimba la Etihad kwa miaka mingine mingi. Kama City watampa mshahara huo Sterling, maana yake ni kwamba, atakuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Katika mechi nane za Ligi Kuu England alizocheza Sterling kufikia sasa msimu huu, amefunga mabao sita na kutoa asisti moja.

## Lampard: Pulisic kwangu ni mzuri

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amekubali uwezo aliyouonyesha mchezaji wake Christian Pulisic katika mchezo wa Ligi Kuu England ambao waliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Newcastle United, mwishoni mwa wiki.

Bao la Chelsea katika mchezo huo, lilifungwa na beki wake wa kushoto, Marcos Alonso kwa shuti kali katika dakika ya 73, lililomshinda kipa wa Newcastle, Martin Dúbravka.

Mchezaji huyo wa timu ya taifa ya Marekani amekuwa na mwanzo mgumu katika klabu ya Chelsea tangu alipojiunga nayo kwa euro milioni 64 akitokea Borussia Dortmund ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

"Haitokuwa mwisho. Tumeona alivyotengeneza uwiano, amecheza vizuri, ni sehemu ya ushindi," alisema Lampard.

Pulisic ameshindwa kuanza kwenye kikosi cha kwanza katika michezo ya Ligi Kuu England, tangu Agosti ambapo Lampard alikuwa akiwatumia, Willian na Mason Mount kama washambuliaji wake wa pembeni.

Huku taratibu akianga kuingia kwenye kikosi chake, Callum Hudson-Odoi ambaye ametoka majeruhi.

Pulisic mwenye umri wa miaka 21, alitoka na machozi wakati alipotolewa katika mchezo ambao timu yake ya Taifa ya Marekani ilikuwa ikicheza dhidi ya Canada, kitu kilichozua maswali mengi juu yake huku ikianza kuzushwa kuwa huenda Januari akatolewa kwa mkopo.







# United watenga pauni mil. 300 za usajili mpya

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuandaa mkwanja pauni milioni 300 kwa ajili ya kufanya usajili kwenye dirisha lijalo la majira ya joto.

Kwenye dirisha lililopita, United ilikuwa moja kati ya klabu zilizofanya matumizi makubwa wakati iliponasa mabeki Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka kwa fedha nyingi pamoja na mshambuliaji kinda, Daniel James waliyemchukua kutoka Swansea City.

United imekuwa na mwanzo wa ovyo sana kwenye Ligi Kuu England msimu huu ikiwa ni mara ya kwanza tangu msimu wa 1989-90 jambo linaloifanya timu hiyo kuhusishwa na usajili ikiwamo orodha ya mastaa kadhaa wanaotajwa kwamba huenda wakatua Old Trafford kwenye dirisha la Januari.

Kwa mujibu wa Daily Mail, United itaanza harakati za kusajili mwanzoni tu mwa mwaka mpya 2020 baada ya kuhakikishiwa kwamba kutakuwa na kiasi kisichopungua pauni milioni 300.

Ripoti zimekuwa zikidai wachezaji wanaowindwa na United ni mshambuliaji wa Lyon, Moussa Dembele na kiungo mshambuliaji wa Leicester City, James Maddison na wengine ni kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez, beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly na Ousmanne Dembele wa Barcelona.

Kwenye dirisha la Januari ilidaiwa wababe hao wanaweza kuvamia Juventus kumsajili Mario Mandzukic, huku wakimtaka pia Paulo Dybala pamoja na kiungo Mjerumani, Toni Kroos.

# Klopp bado alia na VAR

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Juergen Klopp ameuponda mfumo wa maamuzi ya usaidizi kwa njia ya video (VAR), baada ya kikosi chake kulazimisha matokeo ya sare ya bao1-1 na Manchester United, juzi Jumapili.

Klopp amesema mfumo huo ambao ulibuniwa kwa ajili ya kumsaidia mwamuzi kujiridhisha baadhi ya matukio yenye utata kwa njia ya video, haukuleta maana yoyote kwenye mpambano huo, ambao ulishuhudiwa na mashabiki wengi karibu ulimwengu mzima.

Mjerumani huyo amelalamikia tukio la mwamuzi Martin Atkinson, kushindwa kutoa adhabu dhidi ya wapinzani wao, baada ya faulo aliyofanyiwa mshambuliaji wake Divock Origi, kabla ya Man United kupata bao la kuongoza.

Chombo kinachosimamia Ligi Kuu England, kilipitisha kanuni ya kutumika kwa mfumo wa VAR, ili kuondoa utata wa kimaamuzi, ambao misimu miaka ya nyuma yalikua yanaleta rabsha baina ya waamuzi, wachezaji, mameneja na mashabiki.

"Hili ni tatizo, tunapaswa kulijadili," alisema meneja wa Liverpool akiwa katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo huo kumalizika. "Nilikuwa na uhakika wa asilimia mia moja (100) VAR ingetumika, bao la wapinzani wetu lingekataliwa."

"Mwamuzi aliamuru mchezo uendelee, kwa sababu alitambua mfumo wa VAR upo uwanjani, lakini cha kushangaza hakuutumia baada ya malalamiko yaliyojitokeza... hatua hii haileti maana. Lilikuwa tukio la kutazamwa kupitia VAR, lakini ilishindikana kwa sababu anazozijua mwamuzi.

"Sina hasira kwa jambo hilo, lakini ninazungumza kwa kile nilichokiona na kilivyopaswa kuwa. Nina uhakika mwamuzi Atkinson alipaswa kupuliza kipenga kama kusingekua na mfumo wa VAR, lakini aliamuru mchezo uendelee."






# PEPE AWEKWA KIKAANGONI ARSENAL

**LONDON,** England

JUMBA bovu limemwangukia Nicolas Pepe baada ya juzi usiku klabu yake ya Arsenal kukumbana na kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Sheffield kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Arsenal ikiwa ugenini ilichapwa na hivyo matokeo hayo yamemweka kikaangoni Pepe, nyota kutoka Ivory Coast. Licha ya kununuliwa kwa bei mbaya ya pauni milioni 72, Pepe ameshindwa kutamba Arsenal tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea Lille ya Ufaransa.

Mashabiki wa Arsenal wametoa maoni yao wakidai kwamba, Pepe amekuwa hana msaada kwa timu hiyo tangu atue hapo.

Pepe aling'ara katika Ligi Kuu Ufaransa alipofunga mabao 35 katika mechi 74 alizocheza Lille kabla ya kujiunga na Arsenal katika usajili wa majira ya kipindi cha joto.

Winga huyo mwenye miaka 23, amefunga bao moja kwa penalti katika mechi tisa alizocheza Arsenal. Juzi alikosa nafasi za kufunga licha ya mara kwa mara kuingia ndani ya eneo la wapinzani wao.

Wakati Pepe akishindwa kutamba, kocha wa Arsenal, Unai Emery alidai timu yake ilistahili kupata matokeo mazuri kwa kuwa ilicheza kwa kiwango bora.

"Tulistahili kupata matokeo mazuri. Nadhani kipindi cha kwanza tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hatukuzitumia. Tulipata kona za kutosha pia hatukuzitumia,"alisema Emery.

Kocha huyo wa zamani wa Valencia na Paris Saint Germain (PSG) yuko kikaangoni baada ya mashabiki kuanza kumwandama kwa maneno makali wakimtaka ajiuzulu kutokana na mwenendo mbaya wa Arsenal msimu huu.

# *Carragher amwomba radhi Evra*

**LONDON,** England

BEKI wa zamani wa Liverpool, Jamie Caragher amemwomba radhi nyota wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra kwa kitendo cha kumbagua hapo mwaka 2011.

Caragher alikuwa miongoni mwa wachezaji wa Liverpool waliovaa jezi za kumkingia kifua Luis Suarez baada ya kumfanyia vitendo vya ubaguzi Evra katika mchezo dhidi ya Wigan. Suarez alimbagua Evra katika mchezo wao wa Oktoba mwaka 2011 kwenye Uwanja wa Anfield, lakini nguli huyo ameibuka na kusema walifanya kosa ambalo anajutia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alifungiwa mechi nane na faini ya Dola za Marekani 40,000 na Chama cha Soka England kwa kosa hilo.


Carragher na Evra walikuwa wachambuzi juzi usiku na beki huyo wa kati alitumia nafasi hiyo kuomba radhi.

"Naomba radhi hakuna utetezi wa jambo hili, tumefanya makosa kwa kitendo kile. Neno zuri la kusema ni kwamba tulikosea," alisema Caragher.

Mbali na wachezaji pia aliyekuwa kocha wa timu hiyo Kenny Dalglish alivaa fulana hiyo iliyokuwa na picha ya Suarez kifuani na mgongoni namba saba.

Evra alisema matukio ya ubaguzi katika viwanja vya michezo hayapaswi kufumbiwa macho kwa kuwa yanadhalilisha utu wa mtu.

"Sikupaza sauti ili Luis afungiwe hapana. Nilitaka kuionyesha dunia kuwa matamshi ya ubaguzi ni sumu katika soka. Unapofanya matukio kama yake pia unaiweka klabu katika hatari," alisema Evra.



# DONDOO ZA SO
## MAGAZETI YA




# RONALDO AGOMA KUWAZA KUSTAAFU

## ●●● Mreno huyo asema umri wake wa miaka 34 ni namba tu, kwa sababu...

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI Cristiano Ronaldo amewaambia mashabiki wa Juventus na wadau wote wanaomfuatilia kutoka sehemu mbalimbali duniani kuwa bado hayuko tayari kustaafu kucheza soka licha ya kuwa sasa ana umri wa miaka 34.

"Umri ni namba tu. Haina maana kwamba ukiwa na 34, 35, 36 umefikia mwisho wa kumaliza kucheza," Ronaldo alisema katika mkutano na waandishi wa habari, kuelekea maandalizi ya mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lokomotiv Moscow uliotarajiwa kuchezwa jana Jumanne usiku.

"Ninaweza kuonyesha kiwango changu kizuri, namna ninavyocheza, jinsi ninavyocheza, namna ninavojisikia nilivyo katika ubora, wepesi, kufikiria kuhusu mechi, zaidi nilivyopevuka, Hii inaonyesha utofauti."

Akiwa katika msimu wake wa pili kwenye mkataba wa miaka minne na Juventus, Ronaldo ameamua kuwaeleza mashabiki wa timu hiyo hisia zake anazoziamini katika kutoa mchango kwenye klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo alisema hayo katika mahojiano wiki kadhaa zilizopita, kwa kueleza namna alivyoanza kufurahishwa na maisha jijini hapo akiwa nje ya soka.

"Kutokana na hali hii, nani anajua nini kitatokea hapo mwakani au baada ya miaka miwili?" Mshambuliaji huyo aliuliza.

Tayari Ronaldo ameshafunga bao lake ya 700, tangu alipoanza kucheza soka huku akiwa pia kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ureno, ametajwa katika kikosi cha kuwania Tuzo ya Ballon d'Or. Mreno huyo ameweka rekodi ya kushinda tuzo hiyo mara sita, ambayo ilivunja rekodi iliyokuwa inashikiliwa na mpinzani wake, Lionel Messi wa Barcelona.

Lakini Ronaldo ameweka wazi kwamba bado anataka kuona anashinda mataji matatu akiwa na Juventus.

"Tunataka kushinda taji la Serie A, tunataka kushinda Kombe la FA, tunataka kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema nyota huyo wa zamani wa Manchester United.

"Juventus inatakiwa kufikiwa mambo makubwa. Tutapambana kuhakikisha tunashinda mataji, tunafahamu kuwa itakuwa ni jambo gumu, hasa kwenye ubingwa wa ligi ya Italia na Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini nafikiria kuwa inawezekana. Kila kitu kinawezekana.

"Kwa upande wangu binafsi, sina cha kusema kwa mimi binafsi, si jambo muhimu," aliongeza Ronaldo. "Jambo muhimu ni uwajibikaji wa pamoja. Kama unafanikiwa kupata mafanikio ya pamoja, unakuwa na nafasi nzuri ya kupata mafanikio binafsi. Mpira wa dhahabu upo kwa ajili yangu kwa mara ya pili."

Hata hivyo, suala la kustaafu bado haliko kwenye akili ya Ronaldo, ingawa kutenga muda kwa ajili ya familia yake, ni sehemu kubwa ya maisha ya mshambuliaji huyo.

"Kushinda mechi mbili, kufunga mabao, kufurahia binafsi, kurejea nyumbani na kukuta watoto wakiwa na furaha na wakasema, " Hongera baba kwa kufunga goli. Hii hunipa furaha sana," alisema. "Jambo hili huniongezea molari ya kufanya mazoezi zaidi, kwa ajili ya kushinda mechi, kuwaburudisha watu na mashabiki, ni sehemu ya maisha yangu ninayoyapenda."

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AJIHOFIA

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, amesema amekuwa na hofu ya kutimuliwa kwenye timu hiyo kutokana na kiwango kibovu kinachoonyeshwa na wachezaji wake. ***(Mirror)***

### BARCA, ATLETICO WAMALIZANA

BARCELONA imekamilisha mchakato wa kumsajili Antoine Griezman kwa kuilipa Atletico Madrid kiasi kilichobakia katika usajili wa mshambuliaji huyo cha majira ya joto cha Euro milioni 15. ***(El Mundo - in Spanish)***

### FRED: NIMEANZA KUSOMEKA

KIUNGO wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Brazil, Fred (26), amesema kuwa taratibu ameanza kuelewa mfumo wa soka la England. Nyota huyo alijiunga na United kwa dau la pauni milioni 47 akitokea Shakhtar Donetsk Juni mwaka jana. ***(Telegraph)***

### DERBY KUMPANGA ROONEY

DERBY inatarajia kumpa muda maalumu wa mazoezi nahodha wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Wayne Rooney (33), ili kurejea katika kiwango chake, endapo atakubali kujiunga na timu hiyo inayoshiriki Ligi ya Championship akitokea DC United.***(Mail)***

### ZINEDINE AFUNGUKA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kuwa anahitaji kuona anabakia katika klabu hiyo kwa muda wote. ***(Marca)***

### UPAMECANO AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inaongoza katika mbio za kuwania saini ya beki wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya vijana ya Ufaransa (U-21), Dayot Upamecano (20), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 50. ***(Mail)***

### JUVE, ATLETICO VITANI

JUVENTUS na Atletico Madrid zimeingia katika vita ya kuwania saini ya beki wa West Brom, Nathan Ferguson, ambaye ana umri wa miaka 19. Pia chipukizi huyo anawaniwa na Leeds United. ***(Sun)***

### GIROUD ANUKIA PALACE

STRAIKA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), anawindwa na Crystal Palace, na klabu hiyo inataka kufanya mchakato wa kumhamisha kwenye jiji hilo la London mapema Januari. ***(Sun)***

### MADRID KUUZA "MIZIGO"

REAL Madrid imeweka wazi kuwa haitamsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen (27), katika dirisha dogo la usajili la Januari lakini mchakato huo utafanyika endapo itawauza nyota wake isiyowahitaji. ***(AS)***

### ISCO, DIAZ SAFARI IMEIVA

REAL Madrid inajiandaa kumtoa kiungo, Isco (27), na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidominiki, Mariano Diaz (26), kwa Spurs ili kuhakikisha inapata saini Christian Eriksen. ***(El Desmarque - in Spanish)***

### TAMMY MAMBO SAFI

STRAIKA wa Chelsea, Tammy Abraham (22), anakaribia kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia Stamford Bridge baada ya kuifungia timu hiyo bao la nane kwenye Ligi Kuu England msimu huu. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

## Singida yaumizwa kuwakosa Simba

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Singida United FC umesema kuwa kitendo cha timu yao kushindwa kuutumia Uwanja wa Namfua katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba iliyopangwa kuchezwa Jumapili, "kimetikisa" uchumi wa mkoa wa Singida.

Uwanja wa Namfua ni moja ya viwanja vilivyofungiwa na Bodi ya Ligi kutokana na kuwa katika chini ya viwango.

Akizungumza na gazeti jili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Singida United, Festo Sanga, alisema kuwa wafanyabiashara wengi walikuwa wanaisubiri mechi hiyo ili waweze kujipatia kipato kutokana na idadi kubwa ya wageni waliotarajiwa kwenda kushuhudia mchezo huo.

Sanga alisema kuwa mchezo huo ambao sasa utachezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha utakuwa mgumu, lakini wamewataka mashabiki wao kutokata tamaa.

Aliongeza kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo wa raundi ya tano yanaendelea vema na wanashukuru mashabiki na wadau wa Arusha kuwapa mapokezi mazuri.

## Ndayiragije bado asubiri mkataba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Azam FC imetangaza kuachana na Etienne Ndayiragije, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limesema kuwa bado halijakamilisha mchakato wa kupata Kocha Mkuu mpya atakayekinoa kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema hayo juzi na kuongeza kwamba bado wanasubiri ripoti ya Taifa Stars kutoka kwa Ndayiragije, ambaye amefanikiwa kuipeleka kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).



Karia alisema kuwa Watanzania hawapaswi kuwa na haraka juu ya uamuzi wa kocha mpya kwa sababu jambo hilo hutekelezwa kwa umakini.

Kiongozi huyo amekanusha uwepo wa taarifa kuwa TFF inatarajia kumpa mkataba rasmi kocha huyo, baada ya kuachana na klabu ya Azam FC.

"Nawaomba Watanzania wawe na subira, sisi bado hatujamtangaza kocha mpya wa Stars, Watanzania wanapaswa kuwa na subira, kama Azam walisema ni wao na si sisi, subirini," alisema Karia.

Aliongeza kuwa bado wanaendelea kupokea maombi kutoka kwa makocha mbalimbali, na baada ya mchakato huo kukamilika, wataweka wazi mrithi wa Mnigeria Emmanuel Amunike.

# MICHUANO YA CHALENJI KUANZA DES.1 KAMPALA

**Na Somoe Ng'itu**

BARAZA la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), limesema kuwa mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji yamepangwa kufanyika kuanzia Desemba 1 hadi 19 mwaka huu jijini Kampala, Uganda, imefahamika.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema jana kuwa maandalizi kuelekea mashindano hayo yameshafanyika na kuzitaja nchi zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo ni 11.**

Musonye alizitaja nchi hizo wanachama kuwa ni pamoja na wenyeji Uganda, Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), Kenya (Harambee Stars), Burundi, Somalia, Djibouti, Zanzibar (Zanzibar Heroes), Eritrea, Sudan, Sudan Kusini na Ethiopia.

"Tunafuraha kusema kuwa Cecafa imepokea maombi kutoka katika nchi tatu ambazo zinataka kushiriki mashindano haya kama wageni na tutayafanyia kazi maombi yao," alisema Musonye.

Kiongozi huyo alisema kuwa ratiba ya mashindano hayo itatolewa ifikapo Novemba Mosi mwaka huu, baada ya kufunga dirisha la nchi wanachama kuthibitisha ushiriki wao.

"Tunawashukuru wanachama wetu ambao wamekubali kuwa wenyeji wa mashindano haya, pamoja na nchi zilizokubali kushiriki kwenye michuano hii mitatu, ambayo itakamilisha kalenda ya matukio kwa mwaka huu," Musonye alisema.

Aliongeza kuwa pia baraza hilo liko katika hatua za mwisho za maandalizi ya mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 14 hadi 23 mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam.

Alizitaja nchi zilizothibitisha kushiriki mashindano hayo yatakayofanyika kwa mara ya tatu kuwa ni pamoja na wenyeji Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Uganda, Burundi, Djibouti, Zanzibar, Kenya, Ethiopia na Sudan Kusini.

"Ratiba ya mashindano haya ya Kombe la Chalenji kwa wanawake inatarajiwa kutolewa kesho (leo), tayari maofisa wa Cecafa walifika Dar es Salaam wiki iliyopita ili kuangalia maandalizi yalipofikia, tunafuraha kusema kuwa, kila kitu kimekwenda vema, TFF iko tayari kuandaa michuano hii," aliongeza kiongozi huyo.

Pia alisema kuwa Uganda itakuwa mwenyeji wa mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 17, ambayo pia yatachezwa kuanzia Desemba 1 hadi 19 mwaka huu nchini humo.



Balozi wa Tanzania nchini Sudan, Silima Kombo Haji (wa pili kulia), akiwaongoza wachezaji na viongozi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kukata keki kusherehekea ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji wao. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Nikitas kurejesha heshima MRFA*

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti katika Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), Aristotles Nikitas, amesema kuwa endapo atafanikiwa kurejea madarakani atahakikisha heshima na upinzani uliokuwa katika mkoa huo unarejea.

Uchaguzi Mkuu wa MRFA unatarajiwa kufanyika Jumapili mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nikitas, alisema kuwa lengo lake ni kuona Morogoro inafanya vizuri katika soka la vijana, ambapo miaka ya nyuma ulikuwa ndio "kiwanda" cha kutoa wachezaji wanaong'ara katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali hapa nchini.

Nikitas alisema kuwa akiingia madarakani atahakikisha wanashirikiana kwa karibu na serikali ili kuendeleza vipaji vya wachezaji chipukizi na hatimaye ndoto ya Morogoro kupata bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara nyingine inatimia.

"Heshima ya mkoa kihistoria kama ilivyokuwa inajulikana imekufa, wanasoka wengi waliofanya vizuri katika ngazi ya mkoa na Taifa huko nyuma walitoka Morogoro, ninataka hili lirejee, michezo ichezwe kuanzia shule za serikali hadi za binafsi," Nikitas, Katibu Mkuu huyo wa zamani wa MRFA alisema.

Aliongeza kuwa kwa kushirikiana na viongozi wenzake, watahakikisha wanaboresha miundombinu ya mkoa huo, pamoja na kuwashawishi wadau kusaidia maendeleo ya mchezo huo.

Wakati huo huo, Kamati ya uchaguzi wa MRFA, imewatema wagombea wawili kati ya 17 waliokuwa wanawania nafasi za uongozi katika chama hicho, imeelezwa.

Waliotemwa katika mchakato huo baada ya kumalizika kwa usaili ni Emmanuel Kimbawala aliyekuwa anawania nafasi ya Katibu Msaidizi na Boniface Kiwale, aliyekuwa anagombea cheo cha Ujumbe wa Kamati ya Utendaji wa chama hicho.

# Michezo

Jumatano Oktoba 23, 2019

Nipashe



Ronaldo agoma kuwaza kustaafu UKURASA 30



Mshambuliaji wa Arsenal, Bukayo Saka (kushoto), akifanyiwa faulo na beki wa Sheffield Untied, John Egan, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ililala bao 1-0.
**PICHA: MTANDAO**

## Simba, Azam FC mechi ya kisasi

**Na Somoe Ng'itu**

MUDA utaongea! Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kuwakabili Azam FC katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Simba itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-2, walioupata katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii iliyochezwa mapema Agosti mwaka huu. Akizungumza jana jijini, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na kila kikosi kuundwa na wachezaji wenye uwezo na uzoefu katika ligi hiyo.

Aussems alisema kuwa amewaandaa vema wachezaji wake na kuwakumbusha kuongeza utulivu wanapokuwa na mpira ili waweze kutawala mchezo huo na hatimaye kufunga mabao.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tunaifahamu Azam, wanatufahamu, kwa ujumla niseme tuko tayari kwa mchezo huo, ni mchezo muhimu na unaotarajiwa kuwa ushindani, si mechi rahisi," alisema Aussems.

Naye Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa wako tayari kwa mchezo huo na wamejiandaa kuendeleza kasi ya ushindi.

"Lengo letu ni kupata pointi tatu, tunajua Azam ni timu nzuri, yenye uzoefu na yenye uwezo, ila hii haitufanyi tuwe na hofu, tumejipanga kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema meneja huyo.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema kuwa kikosi chake hakina hofu na kitaingia uwanjani kwa lengo moja la kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo muhimu.

Cheche alisema kuwa kikosi chake hakina mchezaji ambaye ni majeruhi na amewataka mashabiki wao kujaa kwa wingi ili kuwaongezea morari ya kupata matokeo mazuri. Simba itaingia katika mechi hiyo bila ya kupata huduma kutoka kwa nahodha wake, John Bocco wakati wachezaji wa Azam waliokuwa majeruhi, akiwamo Suleiman Ndikumana, Donald Ngoma na beki, Aggrey Moriss wamerejea kikosini wakiwa imara.

# Yanga yachana Mbao Kirumba

**Na Adam Fungamwango**

## Ushindi huo waongeza molari ya kuwakaribisha Pyramids hapo Jumapili...

BAO pekee lililofungwa na Mnamibia Sadney Urikhob liliiwezesha Yanga kuibuka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbao FC, iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

**Kwa matokeo hayo, Yanga ambayo imecheza mechi nne, imefikisha pointi saba sawa na Mbao FC, lakini imepanda hadi katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo huku wenyeji wao wakibakia katika nafasi ya 13.**

Urikhob alifunga bao hilo akiwa ndani ya eneo la hatari, akiwa amezungukwa na mabeki watano wa Mbao, ambao walizembea kuokoa mpira au na kumfanya mfungaji huyo wa Yanga kugeuka na kuupiga mpira kwa mguu wake wa kushoto ambao kipa, Abdallah Makangame, alishindwa kuudaka na kutinga wavuni.

Kipindi cha kwanza, Mbao FC haikufanya shambulizi lolote la maana, badala yake ilijaza viungo kati na mabeki nyuma kwa ajili ya kulinda zaidi lango kuliko kushambulia, huku wakimwacha Said Hamisi mbele bila ya kuwa na msaidizi.

Badala yake Yanga ambayo tena haikuwa na Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, katika benchi, ilikuwa ikijitahidi kupeleka mbele mashambulizi lakini, washambuliaji wake walishindwa kutumia vema nafasi tatu za wazi walizozitengeneza kwa kukosa utulivu.

Dakika ya nane tu ya mchezo, Feisal Salum alipiga shuti kubwa juu, alipopata nafasi safi iliyotokana na kutokea kizaazaa kwenye lango la Mbao FC huku dakika ya 11, David Molinga akiwa kwenye eneo zuri, aliachia shuti kali lililodakwa na kipa Makangame.

Dakika ya tatu ya nyongeza, kabla ya kukamilika kwa kipindi cha kwanza, mpira wa kichwa uliopigwa na nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi, uligonga mwamba wa juu kutokana na krosi safi iliyopigwa na Juma Abdul na kuikosesha Yanga bao la kuongoza kabla ya mapumziko.

Kipindi cha pili mpira ulichangamka zaidi na pamoja na Urikhob kuipatia Yanga bao pekee, lakini alikosa magoli mengine mawili, dakika ya 49 kabla ya kufunga goli, na dakika ya 72.

Mbao ilipoteza nafasi mbili za kusawazisha bao dakika za mwisho wa mchezo, 82 na 86, lakini straika wake wa kutegemewa, Said Hamisi alikosa utulivu na Frank Shikalo kuokoa hatari hizo.

Pamoja ya Mbao kumwingiza straika wa zamani wa Toto African, Azam FC na Biashara United Waziri Junior, lakini hakuwa na msaada wowote hadi dakika 90 zilipomalizika.

Katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, JKT Tanzania ilitoka suluhu dhidi ya KMC FC, zote za jijini hapa.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena leo kwa mabingwa watetezi, Simba kuvaana na Azam FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam huku Polisi Tanzania wakiwakaribisha Mwadui FC kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika mjini Moshi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002